MODULI

# Misingi ya Lugha na Isimu ya Kiswahili

# KIU 07105

Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima
Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu
Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi – Kwa njia ya Masafa

# Hakimiliki

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuzalisha, kunakili, wala kusambaza sehemu yoyote ya kazi hii kwa namna yoyote ile bila kibali cha maandishi kutoka Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima isipokuwa kwa kunukuu matini fupifupi zinazoweza kutumika kwa ajili ya utafiti na mapitio ya maandiko.

© Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, 2022

**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

**Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelezi – Kwa Njia ya Masafa**

S. L. P. 20679,
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed
**Dar es Salaam**
Simu: +255 22 2150838
Baruapepe: info@iae.ac.tz
Tovuti: www. iae.ac.tz

# Shukurani

Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima, Dkt. Michael Ngumbi anapenda kutoa shukurani za dhati kwa watu mbalimbali ambao wamechangia kwa namna moja au nyingine katika kukamilisha kazi hii. Wafuatao ambao ni wafanyakazi na wasio wafanyakazi wa TEWW wanastahili kutajwa kipekee kwa kuongoza mchakato huu hadi kukamilika kwake:

| | |
|---|---|
| Julius E. Challigha: | Mkuu Idara ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu |
| Scholastica Kileo: | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mwandishi) |
| Mary Charwi: | Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (Mpitiaji) |
| Eric Samba: | Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima (Mhariri) |

................................
Dkt. Michael W. Ng'umbi
**Mkurugenzi**
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

................................
Dkt. Michael W. Ng'umbi
**Mkurugenzi**
**Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima**

# Yaliyomo

**Kuhusu moduli hii** 1

Muundo wa moduli hii ... 1
Marejeleo ... 1

**Maelezo ya jumla kuhusu moduli** 3

Karibu katika moduli hii ... 3
Umahiri wa Jumla ... 3
Mbinu za usomaji ... 3
Je, unahitaji msaada? ... 4
Mazoezi ... 5

**Namna ya kutumia moduli hii** 6

Ishara za pambizo ... 6

**Somo la Kwanza** 7

Kufafanua Dhana ya Lugha ... 7
Utangulizi ... 7
Matokeo ... 7
Maana ya Lugha ... 7
Sifa za Lugha ... 8
Kidokezo ... 10
Tafakuri ya Somo ... 17
Zoezi la Somo ... 17

**Somo la Pili** 19

Kuchunguza Historia ya Lugha ya Kiswahili ... 19
Utangulizi ... 19
Matokeo ... 19
Kidokezo ... 23
Kidokezo ... 26
Tafakuri ya Somo ... 28
Zoezi la Somo ... 28

**Somo la Tatu** 29

Kuchambua Isimu ya Lugha ya Kiswahili ... 29
Utangulizi ... 29
Matokeo ... 29
Maana ya Isimu ... 29
Matawi ya Isimu ... 30
Matawi ya Isimu Fafanuzi ... 32
Isimu ya Lugha ya Kiswahili ... 33

Tafakuri ya Somo ... 36
Zoezi la Somo ... 36

**Somo la Nne** 37

Kutumia Fonolojia ya Lugha ya Kiswahili ... 37
Utangulizi ... 37
Matokeo ... 37
Dhana za Msingi katika Fonolojia ... 37
Dhana ya Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili ... 39
Fonimu za Lugha ya Kiswahili ... 52
Uainishaji wa Fonimu za Lugha ya Kiswahili ... 53
Tafakuri ya Somo ... 57
Zoezi la Somo ... 57

**Somo la Tano** 58

Kuchambua Mofolojia ya Lugha ya Kiswahili ... 58
Utangulizi ... 58
Matokeo ... 58
Dhana ya Mofolojia ya Kiswahili ... 58
Dhana za Msingi katika Mofolojia ... 60
Kuchambua Aina za Maneno ... 67
Mbinu za Uundaji Maneno ... 80
Dhana ya Mofofonolojia ... 83
Tafakuri ya Somo ... 87
Zoezi la Somo ... 88

**Somo la Sita** 89

Kutumia Sintaksia ya lugha ya Kiswahili ... 89
Utangulizi ... 89
Matokeo ... 89
Kufafanua Dhana ya Sintaksia ... 89
Dhana za Msingi Katika Sintaksia ... 91
Mjadala ... 92
Tafakuri ya Somo ... 112
Zoezi la Somo ... 112

**Somo la Saba** 113

Kutumia Semantiki na Pragmatiki ... 113
Utangulizi ... 113
Matokeo ... 113
Dhana ya Semantiki na Pragmatiki ... 113
a) Maana ya Semantiki 113
b) Maana ya Pragmatiki 114
Dhana za Msingi katika Semantiki na Pragmatiki ... 114

Uhusiano na Umuhimu wa Semantiki na Pragmatiki ........................................ 115
a) Uhusiano 115
b) Umuhimu wa Semantiki na Pragmatiki 115
Viwango vya Maana ........................................................................ 116
a) Maana Katika Kiwango cha Neno 116
Aina za Maana ............................................................................ 120
a) Maana ya Msingi 120
b) Maana ya Ziada/Maana ya Kimatlaba/Ashirifu 121
c) Maana ya Kimtindo 121
d) Maana Akisi/ Mwangwi 121
e) Maana Dhamirifu 121
f) Maana Hisia 122
g) Maana/Tangamano/ Endefu 122
Nadharia za Maana ........................................................................ 122
a) Nadharia ya Maana kama Kitajwa au Kirejelewa 122
b) Nadharia ya Maana Kama Dhana/ Taswira 123
c) Nadharia ya Maana kama Mwitikio wa Msikilizaji 123
d) Nadharia ya Maana Kama Matumizi 124
e) Nadharia za Masharti ya Ukweli za Maana 124
Tafakuri ya Somo ............................................................................ 125
Zoezi la Somo ................................................................................ 125

**Somo la Nane** **126**

Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Miktadha Mbalimbali ........................................ 126
Utangulizi ................................................................................ 126
Matokeo .................................................................................... 126
Dhana za Lugha ya Mazungumzo na Maandishii .............................................. 126
a) Maana ya Lugha ya Mazungumzo 127
b) Maana ya Lugha ya Maandishi 128
Stadi za Lugha ya Mazungumzo na Maandishi................................................. 129
a) Stadi za Lugha ya Mazungumzo 129
b) Stadi za Lugha ya Maandishi 129

Mada za Lugha ya Mazungumzo na Lugha ya Maandishi.................................. 129
a) Mada za Lugha ya Maazungumzo 129
b) Mada za Lugha ya Maandishi 130
Alama za Uandishi ........................................................................................ 134
Tafakuri ya Somo............................................................................................ 137
Zoezi la Somo ................................................................................................. 137

**Marejeleo 138**

# Kuhusu moduli hii

Moduli hii ya kutumia Stadi za Uandishi katika Maisha imetayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli zote zilizotayarishwa na Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima zina muundo linganifu, kama ilivyoelezwa hapa chini.

# Muundo wa moduli hii

## Maelezo ya jumla kuhusu moduli

Maelezo ya jumla kuhusu moduli hutoa utangulizi wa jumla wa moduli. Habari zinazopatikana katika maelezo ya jumla kuhusu moduli zitakusaidia kuamua:

- Kama moduli hii inakufaa;
- Kile unachohitaji kukijua;
- Unachoweza kutarajia kutoka katika moduli; na
- Muda utakaohitaji kutumia ili kukamilisha moduli.

Maelezo haya ya jumla pia hutoa mwongozo juu ya:

- Mbinu za usomaji;
- Mahali pa kupata msaada;
- Mazoezi ya nyumbani na tathmini ; na
- Ishara za vitendo mbalimbali.
- Masomo.

Tunatilia mkazo kuwa usome maelezo ya jumla kuhusu moduli hii kwa makini kabla ya kuanza masomo yako.

## Yaliyomo kwenye moduli

Moduli hii imegawanywa katika masomo manne. Kila somo lina:

- Utangulizi wa yaliyomo kwenye moduli;
- Matokeo ya somo;
- Maudhui ya kimsingi ya somo pamoja na mazoezi mbalimbali ya kufanya;
- Muhtasari wa somo; na
- Mazoezi na tathmini, kama inavyohitajika.

## Marejeleo

Kwa wale wanaopenda kujifunza mengi juu ya mada hii, tunawapa orodha ya marejeleo ya ziada mwishoni mwa Moduli hii. Marejeleo haya yanaweza kuwa vitabu, makala au tovuti.

## Maoni yako

Baada ya kukamilisha Moduli ya Stadi za Uandishi katika Maisha, tutashukuru ikiwa utatenga muda wako kutoa maoni yako kuhusu kipengele chochote cha moduli hii. Maoni hayo yanaweza kuhusu:

- Yaliyomo kwenye moduli na muundo wake;
- Makala za kusoma kwa moduli na marejeleo mengine;

- Mazoezi ya nyumbani ya moduli;
- Tathmini za moduli; na
- Muda wa moduli.
- Usaidizi katika moduli (wahadhiri waliosimamia moduli, usaidizi wa kiufundi, n.k.).

Ukitoa maoni mwafaka utatusaidia kuboresha moduli hii.

# Maelezo ya jumla kuhusu moduli

## Karibu katika moduli hii

Mpendwa mwanachuo, moduli hii inahusu Misingi ya Lugha na Isimu ya Kiswahili. Imeandaliwa kama mwongozo na rejea kwa wanachuo wa Shahada kwa Njia Huria na Masafa katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima. Moduli imegawanyika katika masomo saba ambayo ni: **kufafanua dhana ya lugha**, **kuchambua isimu ya lugha ya Kiswahili, kutumia fonolojia ya lugha ya Kiswahili, kuchambua mofolojia ya lugha ya Kiswahili, kutumia sintaksia ya lugha ya Kiswahili, kutumia semantiki na pragmatiki (ya lugha ya Kiswahili), na kutumia lugha ya Kiswahili katika miktadha mbalimbali.** Kila somo lina kazi na mazoezi ya kutosha yatakayokufanya uelewe vizuri yaliyomo kwenye moduli nzima. Ni matumaini yangu utafurahia kujifunza moduli hii.

## Umahiri wa Jumla

Baada ya kumaliza kujifunza moduli hii utaweza kuchambua na kutumia kanuni mbalimbali za lugha na isimu ya Kiswahili katika miktadha ya watumiaji wa lugha ya Kiswahili.

## Mbinu za usomaji

Kwa kuwa wewe ni mwanafunzi wa Elimu ya Sekondari kwa Njia Mbadala, utaratibu wako wa kusoma utakuwa tofauti na ule ulioutumia ulipokuwa ukisoma katika mfumo rasmi. Utachagua unachotaka kusoma, utakuwa na motisha ya kitaalamu na/au ya kibinafsi inayokusukuma, na bila shaka utakuwa ukiratibu shughuli zako za kiusomaji huku ukizingatia majukumu yako mengine ya kitaalamu au kijamii.

Kimsingi, utakuwa unayadhibiti mazingira yako ya masomo. Kwa hivyo, utahitajika kufikiria juu ya masuala ya utendaji yanayohusiana na udhibiti wa wakati, kuweka malengo, udhibiti wa shinikizo na kadhalika. Pengine utahitaji kujizoesha tena katika maeneo kama upangaji wa muda, namna ya kuimudu mitihani, na kutumia mtandao kama marejeleo ya ujifunzaji.
Mambo utakayozingatia sana ni *muda* na *nafasi*, yaani muda unaotenga kwa masomo yako na mazingira unamosomea.
Tunapendekeza kwamba uitumie nafasi hii – kabla ya kuanza kujisomea kibinafsi – kujifahamisha mambo haya. Kuna marejeleo

mengi mazuri kwenye mtandao. Viungo vichache vinavyopendekezwa ni:

- http://www.how-to-study.com/

Tovuti ya "How to study" yaani "Jinsi ya kusoma" imetengwa mahsusi kwa ajili ya marejeleo ya mbinu za usomaji. Utapata viungo kuhusu kujitayarisha kusoma (orodha ya mambo tisa muhimu kuhusu mahali pazuri pa kusomea), kuandika kumbukumbu, mikakati ya kusoma vitabu vya kiada, kutumia vyanzo vya kumbukumbu, dukuduku la mitihani.

- http://www.ucc.vt.edu/stdysk/stdyhlp.html

Hii ni tovuti ya Kitengo cha Masuala ya Wanafunzi, Virginia Tech. Utapata viungo vya namna ya kupanga muda wako (ikiwa ni pamoja na kiungo cha "wakati huenda wapi?"), orodha-kaguzi ya mbinu za usomaji, mbinu za kimsingi za kumakinikia jambo, udhibiti wa mazingira ya kusomea, kuandika kumbukumbu, namna ya kusoma insha kwa kusudi la kuchanganua, mbinu za kukumbuka.

- http://www.howtostudy.org/resources.php

Hii ni tovuti nyingine ya "jinsi ya kusoma" iliyo na viungo muhimu kuhusu udhibiti wa wakati, kusoma kwa ufanisi, mbinu za kusaili/kusikiliza/kuchunguza, kufaidi kutokana na kutenda (ujifunzaji wa kiutendaji), kukuza kukumbuka, vidokezo vya namna ya kudumisha motisha, kukuza mpango wa ujifunzaji.

Viungo vilivyo hapo juu ni mapendekezo yetu ya kukuwezesha kuanza. Wakati tulipokuwa tukiandika, viungo vya tovuti hizi vilikuwa vinatumika. Ikiwa unataka kupata tovuti zaidi, tembelea www.google.com kisha upige taipu na kutafuata "self-study basics" (misingi ya usomi wa kibinafsi), "self-study tips" (vidokezo vya usomi wa kibinafsi), "self-study skills" (mbinu za usomi wa kibinafsi) au tovuti nyingine zenye mada kama hizo.

## Je, unahitaji msaada?

Mpendwa mwanafunzi, katika mchakato wako wa kujifunza, unaweza kuhitaji msaada kuhusu mambo mbalimbali. Kwa mfano, mahali unapoweza kupata msaada na namna ya kupata msaada huo. Pamoja na hayo, unaweza kuhitaji ufafanuzi kuhusu moduli unazosoma. Hivyo basi, unashauriwa kuomba ufafanuzi wa yote hayo kwa mratibu wa kituo chako au mwezeshaji wako. Pia, unaweza kufungua tovuti ya Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima yenye anwani hii: www.iae.ac.tz au piga simu hii +255 22 2150836.

# Mazoezi

Baada ya kila somo, unahitajika kujibu maswali ya zoezi la somo. Majibu ya zoezi hili la kila somo hautayawasilisha kwa mwezeshaji wako, ni kwa ajili ya kufanya tafakuri ya ulichojifunza. Pia, utapewa majaribio na mazoezi ambayo utayafanya na kuyawasilisha kama utakavyoongozwa na mwezeshaji wako. Pamoja na hayo, utatakiwa kufanya mitihani ya majaribio kwa ajili ya upimaji wa maendeleo yako ya kitaaluma.

# Namna ya kutumia moduli hii

## Ishara za pambizo

Wakati unajifunza moduli hii utagundua kwamba kuna matumizi mengi ya ishara za pambizo. Ishara hizi zina jukumu la kuashiria aina fulani ya matini, kazi mpya au kubadilika kwa zoezi. Zimetumiwa ili kukuongoza kujua namna ya kuitumia moduli hii.

Seti nzima ya ishara imetolewa hapa chini. Tunapendekeza kuwa ujizoeze ishara hizi na maana zake kabla ya kuanza masomo yako.

| | | | |
|---|---|---|---|
| Zoezi | Tathmini | Zoezi la Nyumbani | Kisa Mafunzo |
| Mjadala | Zoezi la Kikundi | Usaidizi | Kumbuka! |
| Matokeo | Kusoma | Tafakari | Mbinu za Usomaji |
| Muhtasari | Istilahi | Muda | Kidokezi |

# Somo la Kwanza

## Kufafanua Dhana ya Lugha

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo hili utajifunza dhana ya lugha. Katika kufafanua dhana ya lugha utapitia mitazamo mbalimbali ya wataalamu wa lugha wanaoelezea maana ya lugha, kuchambua sifa za lugha, na kufafanua dhima za lugha. Aidha, utafafanua nadharia za lugha, na kujifunza kuhusu jamii za lugha. Tunaamini kuwa baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Mpendwa mwanafunzi, karibu katika somo hili.

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana nzima ya lugha: maana, sifa na dhima zake;
- Kufafanua nadharia za lugha; na
- Kuchambua jamii za lugha.

### Maana ya Lugha

Neno "lugha" limefasiliwa na wataalamu mbalimbali wa lugha kwa mitazamo tofauti lakini yenye kuelekeana. Baadhi ya wataalamu hao ni Weber (1985) anasema kuwa lugha ni mfumo wa mawasiliano ya mwanadamu ambao hutumia mpangilio maalumu wa sauti kuunda vipashio vikubwa zaidi, kwa mfano, mofimu, maneno, na sentensi.

Aidha, Kamusi ya TUKI (1990: 34) inafasili dhana ya lugha kuwa ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Massamba na wenzake (1999: 1) wanaiona lugha kama mfumo wa sauti nasibu ambazo hutumiwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao.

Kwa upande mwingine, Massamba (2004: 64) anasema, lugha ni mfumo wa sauti nasibu ambazo zimebuniwa na jamii kwa madhumuni ya mawasiliano kati yao. Naye Matinde (2012: 2)

anaiona lugha kama utaratibu maalum wa sauti za nasibu ambazo huhodhi maana katika jamii fulani.

Mpendwa mwanafunzi, baada ya kupitia fasili za wataalamu hao, tunaweza kusema kuwa, *lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zenye mpangilio maalum ili kuunda vipashio vikubwa zaidi kuanzia neno hadi sentensi zenye maana ili viweze kutumika katika mawasiliano ya mwanadamu.*

## Sifa za Lugha

**a) Lugha ni Mfumo wa Sauti**

Wazo hili la mfumo katika lugha liliasisiwa na mwanaisimu-muundo wa Kiswisi aitwaye Ferdinand de Saussure. Anasema, lugha ni mfumo, kwa sababu hujengwa na vipashio mbalimbali vinavyohusiana. Mfumo huu hutumiwa na jamii fulani katika mawasiliano. Kwa tafsiri rahisi tunaweza kusema mfumo ni mchakato wa kuviweka vipashio mbalimbali kwa utaratibu maalum katika lugha fulani. Mathalani, katika lugha ya Kiswahili; sauti za lugha hupangwa ili kupata silabi; silabi nazo hupangwa kwa utaratibu ili kupata neno; maneno hupangwa ili kupata sentensi.

**b) Sauti za Lugha ni Nasibu**

Mpendwa mwanafunzi, wazo la unasibu katika lugha lilianzishwa pia na mwanaisimu Ferdinand de Saussure wakati alipozungumzia dhana za “kiashiria” kwa maana ya umbo la kusemwa na kuandikwa, na “kiashiriwa” kwa maana ya dhana au umbo halisi la kitu. Massamba na wenzake (1999: 1) wanafafanua dhana ya unasibu kwa vigezo vitatu: *Kwanza, binadamu hazaliwi na lugha bali huikuta kwa nasibu tu. Pili, walioanzisha lugha huzipanga sauti katika utaratibu wa kinasibu. Tatu, hakuna uhusiano wa moja kwa moja kati ya maneno na maumbo halisi yanazowakilishwa na maneno hayo.* Kwa mfano, neno yai, halina uhusiano na yai lenyewe.

**c) Lugha ina Maana**

Lugha lazima iwe na maana. Maana katika lugha hutokana na jinsi sauti zinavyopangwa kwa utaratibu unaokubalika katika jamii fulani, hivyo kuwezesha maana ya neno au sentensi kueleweka na watumiaji wake.

**d) Lugha ni Mali Binadamu**

Lugha inamhusu binadamu na imekubalika kuwa chombo maalum kinachotumiwa na binadamu kwa madhumuni ya mawasiliano.

**e) Lugha ni Njia ya Mawasiliano**

Lengo mahususi la lugha yoyote huwa ni kusaidia watu kuwasiliana. Binadamu huwasiliana kwa malengo mbalimbali. Mathalani, mtu anapokuwa na sherehe au msiba, huwajulisha ndugu na marafiki kwa njia ya lugha (iwe ya maandishi au mdomo) ili washirikiane naye katika shughuli hiyo. Ni muhimu kujua kuwa zipo njia nyingine ambazo binadamu huzitumia katika mawasiliano. Lakini, si kila mawasiliano ni lugha.

**f) Lugha Huzaliwa, Hukua na Hufa**

Kuzaliwa kwa lugha ni pale inapoanza kutumiwa na binadamu katika mawasiliano baina yao. Aidha, lugha hukua kwa kuongeza msamiati. Vilevile, lugha huweza kufa endapo itakosa watumiaji. Kwa mujibu wa Wanjala na Kvoi (2013: 144), mojawapo ya lugha iliyokaribia kufa ni **Kami** inayozungumzwa na jamii moja mkoani Morogoro.

**g) Lugha Hurithiwa**

Lugha hurithiwa pale mtoto anapozaliwa na kuikuta lugha inayozungumzwa na jamii inayomzunguka, mfano, nyumbani, shuleni, n.k. Mfano mzuri ni jinsi mtoto anavyoweza kuitumia lugha asili ya wazazi au walezi wake.

**i) Lugha Huathiri na Huathiriwa**

Lugha huathiri kwa maneno yake kuingizwa katika lugha nyingine. Pia, huathiriwa pale inapokopa maneno kutoka lugha nyingine.

**j) Lugha ina Utoshelevu**

Utoshelevu wa lugha hutokana na lugha kuweza kutumika katika nyanja mbalimbali kulingana na mahitaji ya watumiaji wa lugha hiyo. Mfano, lugha ya Kiswahili inajitosheleza kwa sababu inatumika kutolea elimu na maarifa mengine, n.k. Hivyo, hakuna lugha bora au dhaifu kuliko lugha nyingine.

## Kidokezo

Mpendwa mwanafunzi, tumeona sifa mbalimbali za lugha ya mwanadamu. Hata hivyo, sifa hizo zinahusu lugha asilia ya mwanadamu; si lugha-unde wala lugha ya ishara. Massamba na wenzake (2004: 1) wanasema, lugha asilia ni lugha inayotumiwa na binadamu katika mawasiliano yao kwa njia ya sauti zinazounda maneno, wakati "lugha-unde" ni lugha iliyoundwa kwa makusudi maalum ya kutumika katika mashine kama vile kompyuta, na lugha ya ishara ambayo japokuwa nayo hutumiwa na binadamu lakini yenyewe haitumii sauti.

### 3. Dhima za Lugha

Mpendwa mwanafunzi, tunapozungumzia dhima za lugha tunarejelea hasa katika umuhimu wa lugha kwa mtu na jamii kwa ujumla. Baadhi ya dhima hizo ni kama zifuatazo:

**a) Lugha ni Kitambulisho**

Lugha ni kitambulisho cha jamii, mtu binafsi, au kundi la watu. Lugha hutumika kama kielelezo cha kuelezea hulka ya mtu, watu au jamii nzima. Binadamu ana uhuru wa kuchagua namna na kile anachotaka kusema. Hivyo basi, lugha inatumika kama chombo cha kujieleza kwa kutumia njia mbalimbali. Vilevile, lugha hutumiwa kuwatambulisha watu wa jamii fulani kutokana na lafudhi yao.

**b) Lugha ni Chombo cha Kuendeleza Mahusiano Mema katika Jamii**

Watu wanapoongea lugha moja huweza kuwasiliana. Hali hii hubainisha maelewano na kujenga mshikamano na mahusiano mema baina yao na jamii kwa ujumla.

**c) Hifadhi ya Utamaduni na Jamii**

Lugha ni chombo mwafaka cha kueneza na kuhifadhi amali na utamaduni wa jamii. Utamaduni wa jamii huhifadhiwa kupitia nyimbo, hadithi, vitendawili, nahau, n.k.

**d) Chombo cha Fikra**

Utafiti umebainisha kuwa, kwa kiasi fulani, lugha ndiyo humwezesha mtu kufikiri. Pale ambapo mtu huwa amezama katika tafakuri, bila kufahamu huanza kuyatamka yanayopita akilini. Katika hali kama hii, lugha husaidia kufanya tafakuri hiyo. Zipo nadharia kadhaa zinazodhihirisha hili. Mfano, nadhariatete ya Sapir-Whorf (Edward Sapir (1884-1939) na Benjamin Lee Whorf (1897-1941) ambayo hueleza kuwa binadamu hutumia lugha kuutafakari na kuujengea maana ulimwengu unaomzunguka kwa kuongozwa na taratibu za lugha yake. (Massamba, 2016: 92).

**e) Lugha ni Chombo cha Kujipatia Maarifa**

Kwa kupitia lugha binadamu huweza kujifunza mambo mbalimbali ulimwenguni. Kwa mfano, kujifunza mbinu mbalimbali za kupambana na magonjwa ya mlipuko kama vile *ugonjwa wa korona 19 (uviko 19)*, jinsi ya kukabili mabadiliko ya hali ya hewa, n.k.

## 4. Nadharia za Asili ya Lugha ya Binadamu

Mpendwa mwanafunzi, kuna nadharia au mitazamo mbalimbali inayofafanua asili ya lugha ya binadamu. Baadhi yanadharia hizo ni kama zifuatazo:

**a) Nadharia ya Lugha kama Sauti Asilia**

Matinde (2012: 7) anasema kuwa kuwa lugha ya binadamu inatokana na miigo ya sauti asilia kutokana na milio ya wanyama, ndege, wadudu ambao wanapatikana katika mazingira wanayoishi binadamu. Mfano, mlio wa **"bow-bow"** uliowezesha kupata neno la Kiswahili **"mbwa"**, au mlio wa kuku wa **kuu–kuu** uliwezesha kupata neno la Kiswahili – **kuku**.

Nadharia hii ina mapungufu. Tunajua wazi kuwa wanyama au ndege hutoa milio au sauti. Lakini, si lazima sauti za wanyama na ndege hao zifanane kati ya lugha moja na nyingine kutokana na kila lugha kuwa na utaratibu wake wa kuwakilisha sauti zinazotolewa na wanyama au ndege hao.

Pia, yapo maneno katika lugha yanayotokana na umbo la kitu, wala sio sauti. Kwa mfano neno la Kiswahili "kifaru" lenye maana ya kifaa cha kijeshi kimetokana na umbo la mnyama *"kifaru"*.

Vilevile, baadhi ya maneno katika lugha hayahusishi na sauti asilia, bali huwa ni dhahania, kama vile *"njaa"*, *"uongo"*, n.k.

**b) Nadharia ya Mfumo wa Sauti za Nasibu**

Nadharia hii inaeleza kuwa lugha ya binadamu ilianza kwa bahati tu. Hakukuwa kikao rasmi kilichokaliwa ili kukubaliana kuyapa majina vitu vinavyomzunguka mwanadamu. Hata hivyo, mapungufu yanayojitokeza katika nadharia hii ni kuwa kila jamii inatumia kitaja tofauti na jamii nyingine lakini kitajwa ni kilekile. Ili nadharia hii iwe na mantiki tulitegemea kila kitajwa kiwe na kitaja kile kile. Kwa mfano, kifaa chenye miguu minne ambacho watu hukikalia, kwa Kiswahili hujulikana kama *"kiti"* lakini kwa Kiingereza *"chair"*. **Je, katika lugha yako ya asili kinaitwaje?**

**c) Nadharia ya Asili ya Lugha Kimaumbile**

Nadharia hii iliasisiwa na Noam Chomsky mwaka 1960. Chomsky anaamini kuwa mtoto huzaliwa na uwezo wa kupata lugha yoyote ya jamii inayomlea au inayomzunguka. (Mtazamo huu unahusisha kuwepo kwa kifaa maalumu cha upataji lugha "KIULU" ambayo ni sehemu ya ubongo ambayo humwezesha mtoto kuwa na uwezo wa kupata lugha). Uwezo wa mtoto kupata lugha hutofautiana kulingana na anavyokua. Mapungufu ya mtazamo huu ni kuwa ili kupata lugha ni muhimu kwa mtoto kuwa miongoni mwa jamii ya watu. Je, kama mtoto akiwa peke yake bila watu wengine hupata wapi uwezo wa kujua lugha?

**d) Mtazamo wa Dini**

Mtazamo huu unaelezwa kuwa lugha zote zilitokana na lugha moja iliyoumbwa na Mungu. Kwamba binadamu walikuwa wanazungumza lugha moja mpaka wakati Mfalme wa Babeli alipoamuru kujenga mnara mrefu ulioitwa **"Mnara wa Babeli"** ili kumfikia Mungu. Mungu alikasirika sana. Akaamua kuingiza tofauti za lugha kwa wajenzi wa mnara huo kiasi cha kushindwa kuelewana. Kuona hivyo, wajenzi hao hawakuendelea na ujenzi wa Mnara wa Babeli na hatimaye wakatawanyika. Hivyo, inaaminika kuwa lugha nyingi zinazozungumzwa leo ni matokeo ya kuanguka kwa mnara wa Babeli. Na kwamba, watu hao walitengana na kwenda kuishi katika maeneo mengine.

Mtazamo mwingine wa kidini ni ule unaohusishwa na Adamu. Adamu anaaminika ndiye binadamu wa kwanza kuumbwa na Mungu na kuwekwa duniani. Na ndiye aliyewapa majina wanyama, ndege na vitu vingine kutokana na uwezo aliopewa na Mungu.

Hata hivyo, nadharia hii ina mapungufu kwani zipo lugha nyingi zilizozuka miaka mingi baada ya Adamu. Je, nazo zimetokana na Mungu?

**e) Lugha Hutokana na Shughuli za Uzalishaji Mali**

Nadharia hii inadai kuwa lugha ya binadamu ilitokana na miguno ya watu wengi walipokuwa wakifanya kazi pamoja. Kazi kama vile kubeba vitu vizito, n.k. ambazo zilihitaji binadamu hao watumie nguvu nyingi. Miguno iliyotolewa wakati wa kufanya kazi hizo ilijitokeza kama nyimbo na baadaye ikawa lugha mbalimbali kulingana na shughuli iliyokuwa ikifanyika. Mtazamo huu nao unaonesha kukosa ushahidi kwani tunaona hata wanyama na ndege hutoa miguno na milio mbalimbali. Je, nayo ichukuliwe kuwa ni lugha?

## 5. Jamii za Lugha

Mpendwa mwanafunzi, **jamii za lugha** ni dhana inayotumika kuelezea makundi ya lugha. Wanaisimu hususani katika tawi la **isimu linganishi** wanazigawa lugha zinazozungumzwa na binadamu katika makundi kulingana na vigezo vifuatavyo:

a) Kigezo cha kinasaba,

b) Kigezo cha kijiografia,

c) Kigezo cha kimuundo, na

d) Kigezo cha kiuamilifu.

**a) Jamii za Lugha kwa Kigezo cha Kinasaba**

Uainishaji lugha kinasaba huweza kuelezwa kama uwekaji lugha katika makundi kutokana na kuwa lugha hizo zimetokana na **lughamame** au **asili moja**. Kundi hili huwa jamii ya lugha zifuatazo:

**i) Kihindi-Kizungu** ni Kihindi, Kashmiri, Kijerumani, Kiingereza, Kiswedishi, Kiitaliano, Kifaransa, Kiispaniola, Kireno, n.k.,

**ii) Kihamiti-Semiti -** hujumuisha Kiebrania, Kimisri, Kisomali, Kigala, Kichadi, Kiarabu na Kiabeshi),

**iii) Lugha za Kiafrika** ambazo Massamba (2002:72-77) anazigawa jamii za lugha za Kiafrika katika makundi matatu:

*(i) Kundi la lugha za Kibantu* - Mfano Kikongo, Kisukuma, n.k.

*(ii) Kundi la lugha za Kihamiti-Kinailoti* - Mfano Kiarabu, Kimasai.

*(iii)Kundi la lugha za Kikhoisani* - Mfano Kisandawe, n.k.

**iv) Jamii ya Lugha za Kiamerika-Kihindi -** hujumuisha lugha zinazozungumzwa katika Amerika ya Kaskazini, Amerika ya Kati na Amerika ya Kusini.

**b) Jamii za Lugha kwa Kigezo cha Kijiografia**

Uanishaji huu huzingatia mahali lugha moja inapozungumzwa. Kwa mfano, lugha za Kibantu zimegawanywa katika makundi yafuatayo kutegemeana na mahali wazungumzaji wake wanapopatikana.

i. Afrika Mashariki: Tanzania, Kenya, Uganda

ii. Afrika ya Kati: Kongo, Zambia, Malawi, n.k.

iii. Afrika Kusini: Afrika Kusini, Zimbambwe, Botswana, n.k.

**c) Jamii za Lugha kwa Kigezo cha Kimuundo**

Hiki ni kigezo ambacho kimetumika kwa kiasi kikubwa sana. Inaaminika kuwa ndicho kigezo cha uhakika katika uanishaji wa lugha. Kigezo hiki huzingatia lugha zenye miundo inayofanana. Wanaisimu linganishi wamegawa lugha hizo katika makundi mawili: *lugha-tenganishi* na *lugha-ambishi*.

**i) Lugha-Tenganishi** ambazo hazina viambishi, pia maneno yake hayawezi kunyambuliwa. Hii ina maana kuwa huwezi kutenganisha neno katika vipandevipande. Mfano wa lugha katika kundi hili ni Kichina ambapo alama moja hutumika kwa neno.

**ii) Lugha-Ambishi** ambao hupachika vipande vya maneno katika mizizi ya maneno. Lugha za kundi hili zimegawanyika katika makundi madogo matatu kama ifuatavyo:

***Lugha-Ambishi Mchanganyo*** ambazo huunganisha viambishi katika maneno kiasi kwamba si rahisi kuvitenganisha viambishi katika maneno hayo. Baadhi ya lugha hizo ni Kiingereza, Kiarabu, Kilatini, Kigiriki, n.k. Kwa mfano katika Kiingereza: neno **"did'** ni kitenzi cha wakati uliopita. Hata hivyo, mofu ya wakati uliopita haionekani kwa uwazi.

***Lugha-Ambishi Bainishi*** ambazo maneno yake huundwa kwa mizizi ya maneno pamoja na viambishi mbalimbali. Baadhi ya lugha zenye muundo huu ni lugha za Kibantu, Kijapani, Kituruki, n.k. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili: maneno kitanda, vitanda, kijitanda; ambayo ni nomino, yameundwa na viambishi awali (**ki-, vi-, ki-, ji-** pamoja na mzizi **-tanda**).

***Lugha Muundo Gubi*** ambazo maneno yake huundwa kwa maumbo mbalimbali yaliyowekwa pamoja. Hii ndio kusema maneno haya huwa na muundo changamano. Kwa mfano, lugha ya Kieskimo kama katika maneno: **'iglu'** (nyumba), **'iglua'** (nyumba yake - mmiliki ni mwanaume), **'igluga'** (nyumba yangu).

**d) Jamii za Lugha kwa Kigezo cha Kiuamilifu**

Hiki ni kigezo cha kugawanya lugha kulingana na matumizi yake. Hapa tunaweza kupata makundi yafuatayo ya lugha.

**i) Lugha Kienzo -** Hizi huzingatia istilahi zinazotumika katika taaluma fulani. Kwa mfano, katika taaluma ya isimu kuna istilahi kama vile nomino, kiambishi, mofu, mofimu, sentensi, n.k ambazo huwezi kuzikuta katika taaluma zingine.

**ii) Lugha Rasimi -** ambazo hutumiwa na watu mashuhuri, na huaminika kuwa ndio lugha bora zaidi kuliko nyingine. Lugha hii huwa na istilahi nyingi ambazo taaluma zingine huzitumia ili kukidhi mahitaji yake. Kwa mfano, lugha za Kilatini na Kigiriki.

**iii) Lugha Rasmi -** Ni lugha ambayo huteuliwa katika nchi fulani ili itumike katika mawasiliano yote rasmi ya kitaifa na kimataifa katika nchi. Baadhi ya nchi huamua kutumia lugha rasmi za mataifa yaliyowatawala kabla ya kupata uhuru. Kwa mfano, lugha rasmi nchini Tanzania ni Kiswahili na Kiingereza.

**iv) Lugha ya Taifa -** ambayo hutumiwa na nchi ili kuwatambulisha na kuwaunganisha wananchi wa nchi fulani. Lugha hii pia huweza kutumika kama lugha rasmi ya nchi. Kwa mfano, nchini Tanzania, lugha ya Kiswahili ni lugha rasmi lakini pia ni lugha ya taifa.

**v) Lugha Sanifu -** Ni miongoni mwa lahaja za lugha fulani ambayo hufanyiwa marekebisho mbalimbali ili itumike kama msingi wa kutolea maarifa. Lugha hii huwa imetolewa makosa yanayohusu sauti za lugha, maumbo ya maneno, miundo ya sentensi, maana za maneno, istilahi n.k. Kwa mfano Kiswahili kinachotumika kufundishia kimetokana na kusanifishwa kwa lahaja ya Kiunguja.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Ukiwa mwaisimu chipukizi unaweza kuifafanua vipi dhana ya lugha?
2. Chambua nadharia za lugha ya mwanadamu.

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Eleza sifa za lugha ya mwanadamu.
2. Kwa kutumia uzoefu wako, eleza mambo yanayotofautisha mawasiliano ya mwanadamu na wanyama wengine.
3. Tumia lugha yako ya asili na nyinginezo unazozifahamu kuelezea nadharia ya asili ya lugha ya mwanadamu.

# Somo la Pili

## Kuchunguza Historia ya Lugha ya Kiswahili

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita ulijifunza dhana ya lugha ambapo ulifafanua maana ya lugha, kuchambua sifa za lugha na kufafanua dhima za lugha. Vilevile, ulifafanua nadharia za lugha, na kuchambua jamii za lugha. Katika somo hili utajifunza historia ya lugha ya Kiswahili. Kwa kuanza, utafafanua historia ya lugha ya Kiswahili kwa kupitia mitazamo mbalimbali ya wanaisimu wanaoelezea historia ya lugha hiyo. Vile vile, utachambua sera ya lugha nchini Tanzania. Tunaamini kuwa baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Mpendwa mwanafunzi, karibu katika somo hili.

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua historia ya lugha ya Kiswahili; na
- Kuchambua sera ya lugha nchini Tanzania.

**1. Historia ya Lugha ya Kiswahili**

Mpendwa mwanafunzi, tutaangazia historia ya lugha ya Kiswahili katika pande tatu; *asili, chimbuko*, na *kuenea* kwake.

**a) Asili ya Lugha ya Kiswahili**

Dhana "asili ya lugha" ina maana *jinsi lugha ilivyoanza*. Hivyo, kwa dhana ya asili ya lugha ya Kiswahili ina maana ya jinsi lugha ya Kiswahili ilivyoanza kutumiwa kama chombo cha mawasiliano. Ipo mitazamo maarufu minne inayoelezea asili ya Kiswahili. Mtazamo kuwa: a) Kiswahili ni Kiarabu, b) Kiswahili ni lugha chotara, c) Kiswahili ni pijini na krioli, na d) Kiswahili ni Kibantu.

**(i) Kiswahili ni Kiarabu**

Inaaminika kuwa asili ya lugha ya Kiswahili ni lugha ya Kiarabu kwa vigezo vifuatavyo:

*i)* Neno lenyewe "Kiswahili" lilitokana na neno la Kiarabu **"sahl"** wingi wake **"sawahil"** likiwa na maana "pwani". Hivyo kuamini kuwa Kiswahili ni Kiarabu.

***ii) Kuwepo kwa Maneno Mengi ya Kiarabu katika Kiswahili***

Lugha ya Kiswahili ilionekana kuwa na maneno mengi ya Kiarabu. Maneno yanayohusu *salamu* kama vile "shikamoo", n.k. Yanayotaja muda kama vile "adhuhuri", "alasiri", n.k., yanayotaja *namba* kama vile "moja", "mbili", n.k.

Kigezo hiki kina mapungufu. Kwanza, haikuelezwa *idadi halisi* ya maneno ya Kiarabu yanayosemekana kuwa mengi katika lugha ya Kiswahili. Pili, lugha moja *kukopa maneno* kutoka katika lugha nyingine si jambo geni. Kwani Kiswahili pia kimekopa maneno mengi kutoka lugha ya Kiingereza, Kijerumani, Kihindi, Kireno, hata lugha za asili za Tanzania. Kigezo hiki kingekuwa sahihi endapo lugha za Kiarabu na Kiswahili zingetokana na **lugha-mama** moja.

***ii) Dini ya Kiislamu***

Inaelezwa kwamba kwa kuwa wenyeji wengi wa pwani ya Afrika Mashariki ni Waislamu, na Uislamu ulileta na Waarabu, basi lugha ya Kiswahili nayo ni Kiarabu. Hata hivyo, kigezo hiki nacho hakina uthibitisho wa kutosha kwa kuwa katika pwani ya Afrika ya Mashariki kulikuwa na watu kutoka mataifa mengine, na sio Waarabu pekee.

**(ii) Kiswahili ni Lugha Chotara**

Wanaisimu kama vile Massamba (2002: 19) akimnukuu Hamo Sassoon (1980) wanasema kuwa, Kiswahili ni lugha chotara iliyotokana na Kiarabu na lugha za Kibantu. Lugha hiyo ilizaliwa baada ya wanaume wa Kiarabu waliochelewa pepo za kusi za kuwarudisha makwao, kuamua kuweka makazi pwani ya Afrika Mashariki kusubiri msimu mwingine wa pepo za kusi. Wakati wanasubiri pepo hizo waliamua kuwaoa wanawake kutoka lugha za Kibantu; hivyo Kiswahili kikazaliwa kwa njia hiyo.

Hata hivyo, mtazamo huu una mapungufu. Kwani mtu anaweza kujiuliza, hao wanaume walipoenda kuposa walitumia lugha gani kuwasiliana na wakwe zao?

**(iii) Kiswahili ni Pijini na Krioli**

Kwa maelezo ya Sassoon yaliyotafsiriwa na Massamba (2002), Kiswahili kilianza kama pijini ya Kiarabu na lugha ya wenyeji yaani Kibantu. **Pijini** hiyo ikakomaa na kuwa **krioli**. Mtazamo huu wa Sassoon una mapungufu. Kutokana na maelezo

yake, Kiswahili kilikuwa asilimia 80 *"lugha ya mama na watoto"*, na Kiarabu asilimia 20 *"lugha ya baba (Mwarabu) na biashara"*. Na kwamba, Kiarabu *kilijaza mapengo* pale ambapo maneno ya lugha ya Kibantu yalikuwa hayatoshi au hayakuwepo. Hii inaonesha kuwa Kiswahili kilikuwepo kwa asilimia kubwa kuliko Kiarabu.

**(iv) Kiswahili ni Kibantu**

Huu ni mtazamo wa kisayansi unaoelezea asili ya lugha ya Kiswahili. Ni mtazamo unaozingatia vigezo vya kiisimu. Mwanaisimu mashuhuri anayeegemea mtazamo huu aliitwa **Malcolm Guthrie**. Mwanaisimu huyu alichunguza lugha zaidi ya 200 za Kibantu kwa kuzingatia kigezo cha kijiografia, na kubaini mfanano mkubwa kati ya lugha hizo. Aliweka bayana utafiti wake mwaka 1948 katika toleo la kwanza la kitabu chake kilichoitwa "**The Classification of the Bantu languages bound with Bantu Word Division**". Katika moduli hii tutaelezea vigezo vya kiisimu kutoka vyanzo tofauti tofauti. Vigezo hivyo ni: *kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia,* na *kisemantiki*.

**i. Kigezo cha Kifonolojia**

Kigezo hiki kinazingatia vitamkwa vya lugha. Hapa tutaangalia kipengele cha **muundo wa silabi**. Muundo wa silabi za Kiswahili hufanana sana na ule wa lugha za Kibantu. Kwa mfano, kwa muundo wa Konsonanti, Konsonanti na Irabu (KKI): Kiswahili: $ **sha** $ **mba** $ Kizaramo: $ **ng'a** $ **nda** $.

**ii. Kigezo cha Kimofolojia**

Kigezo hiki kinazingatia maumbo ya maneno. Kigezo hiki kinazingatia hasa

***a) Mpangilio wa Viambishi*** (yaani vipande vya maneno vinavyopachikwa katika mizizi ya maneno) katika lugha ya Kiswahili unafanana sana na ule wa lugha za kibantu. Kwa mfano,

| Kiswahili | Kipogoro | Kirangi |
|---|---|---|
| **Tu - na - som - a** | **Twa- n'ku- som- a** | **Tw- o- som- a** |
| **Nfs1$_W$ - Nj$_{Uliopo}$ -Mz I$_i$** | **Nfs1$_W$ Nj$_{Uliopo}$ Mz I$_i$** | **Nfs1$_W$ Nj$_{Uliopo}$ Mz I$_i$** |

**N.B.** *Nfs1$_W$ = Nafsi 1$_{Wingi}$; Nj$_{Uliopo}$ = Njeo ya wakati uliopo; Mz = Mzizi wa neno; I$_i$ = Irabu ishilizi*

***b) Uambishaji na Unyambulishaji* -** Maneno ya lugha ya Kiswahili huweza kuambishwa kwa kuongeza vipande vya maneno kabla au baada ya mzizi wa neno ili kuunda neno jipya katika kategoria

nyingine, na pia huweza kunyambulishwa kwa kuongeza viambishi baada ya mzizi wa neno ili kupata neno lingine katika kategoria hiyo hiyo.

**Jedwali 1: Uambishaji na Unyambulishaji wa Maneno**

| Kiswahili | Kizaramo | Kirangi |
|---|---|---|
| **Uambishaji:**<br>**Mzizi:** -lim-<br>ki-**lim**-o | **Uambishaji:**<br>**Mzizi:** -lim-<br>ki-**lim**-o | **Uambishaji:**<br>**Mzizi:** -rem-<br>i-**rem**-aa, |
| **Unyambulishaji:**<br>**Mzizi:** -lim-<br>Lim-i-a,<br>lim-iw-a,<br>lim-ik-a | **Unyambulishaji:**<br>**Mzizi:** -lim-<br>Lim-i-la,<br>lim-igw-a,<br>lim-ik-a | **Unyambulishaji:**<br>**Mzizi:** -rim-<br>rem-e- ra,<br>rem-irw-a,<br>rim-ik-a |

**Chanzo:** Mwandishi (2021)

***c) Ngeli za Nomino*** - Ngeli za nomino ni makundi ya nomino zinazofanana kimaumbo. Makundi ya nomino za lugha ya Kiswahili yanafanana sana na makundi ya nomino za lugha za kibantu kwa kuzingatia maumbo ya umoja na uwingi.

**Jedwali 2: Ngeli za Nomino**

| Kiswahili | Kirangi |
|---|---|
| **1. M-** mfano: M-toto,<br>**2. Wa-** mfano:Wa-toto | **1. M-** mfano: Mu-singa,<br>**2. Va-** mfano: Va-singa |
| **3. M-** mfano: M-ti<br>**4. Mi-** mfano: Mi-ti | **3. Mu-** mfano: Mu-ti<br>**4. Mi-** mfano: Mi-ti |
| **5. Ki -** mfano: Ki-ti<br>**6. Vi-** mfano: Vi-ti | **5. I -** mfano: i-chuumbi<br>**6. Ma-** mfano: Ma-chuumbi |

**Chanzo:** Mwandishi (2021)

**iii. Kigezo cha Kisintaksia**

Kigezo hiki kinazingatia miundo au mpangilio wa maneno katika tungo. Miundo kama vile virai, vishazi, na sentensi inayohusu lugha ya Kiswahili na ile ya lugha zingine za kibantu ina mfanano mkubwa sana. Kwa mfano,

**Jedwali 3: Miundo ya Lugha ya Kiswahili na Kibantu**

| MUUNDO | LUGHA | MFANO |
|---|---|---|
| **Kirai (KN)** | **Kiswahili:** → | (i) Mtoto mdogo<br>**KN** + **V** |
| | **Kirangi:** → | (ii) Musinga muduudi |

| | | KN + V |
|---|---|---|
| **Sentensi (Sahili):** | **Kiswahili:** → | (i) Mgeni ameondoka<br>**N + T** |
| | **Kirangi:** → | (ii) Muyeeni arokire<br>**N + T** |

**Chanzo:** Mwandishi (2021)

**iv. Kigezo cha Kisemantiki**

Kigezo hiki kinazingatia msamiati wa lugha. Msamiati ni jumla ya maneno yanayopewa maana katika lugha. Uchunguzi umeonesha kuwa msamiati wa lugha ya Kiswahili unafanana sana na ule wa lugha za Kibantu. Msamiati huo ni ule wa msingi ambao unahusu viungo vya mwili kama vile *macho, mikono, kichwa, miguu, tumbo,* n.k., na maumbile ya dunia kama vile *miti, mito, bahari,* n.k. (Taz. Massamba na wenzake (1999: 10). Kwa mfano,

**Jedwali 4: Mfanano wa Msamiati wa Lugha za Kibantu**

| Kiswahili | Kigogo | Kiruri |
|---|---|---|
| Mguu | mugulu | okuguru |
| Macho | meso | ameeso |
| Kichwa | mutwe | omutwe |

**Chanzo:** Imerekebishwa kutoka Massamba na wenzake (1999: 10)

Licha ya kuwepo tofauti ndogondogo za matamshi, na mabadiliko ya viambishi, lakini tofauti hizo hazihusu mzizi wa neno ambao ndio msingi wa msamiati husika.

## Kidokezo

Mpendwa mwanafunzi, tumeeleza mitazamo minne kuhusu historia ya lugha ya Kiswahili. Pamoja na tofauti ndogondogo zilizojitokeza katika baadhi ya vipengele, bado mtazamo wa kuwa lugha ya Kiswahili ina asili ya Kibantu unaweza kuwa na mashiko zaidi kuliko mitazamo mingine. Inaaminika tofauti hizo zilichangiwa kwa kiasi kikubwa na mwachano wa muda mrefu wa wazungumzaji wa lugha hizo ambazo zinasemekana zilikuwa na asili moja (Rejea Massamba 2002). Hivyo, tuhitimishe kwa kusema kuwa Kiswahili ni Kibantu.

**b) Chimbuko la Lugha ya Kiswahili**

Mpendwa mwanafunzi, neno “chimbuko” lina maana ya eneo au mahali lugha ilikoanzia. Kumekuwa na mitazamo tofauti kuhusu mahali hasa Kiswahili kilipoanzia.

***i) Kiswahili Kilianzia Afrika ya Magharibi***

Wataalamu wengine wanaosema kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Afrika ya Magharibi, hususani katika nchi ya Kameruni. Kwamba, Wabantu wa mwanzo waliishi Afrika ya Magharibi. Hivyo, inaaminika kuwa Kiswahili ndiko kilipoanzia.

***ii) Kiswahili Kilianzia Kongo***

Baadhi ya wataalamu huamini kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili lilikuwa katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo. Wanasema kwamba baada ya wale Wabantu wa mwanzo kutoka Afrika ya Magharibi kukaa kwa muda mrefu katika misitu minene ya Kongo walianza kutawanyika na kuelekea maeneo mengine kwa sababu mbalimbali, ikiwemo kutafuta maeneo yenye uoto wa asili. Hivyo walijikuta wakitokea kingo za Uganda na Kigoma hadi kufikia Ziwa Viktoria. Walikaa hapo kwa muda mrefu hadi walipoamua kuondoka maeneo hayo na kuelekea katika mabonde yenye rutuba ya mto Tana katika visiwa vya Shupate na Shungwaya katika nchi ya Kenya.

***iii) Kiswahili Kilianzia Pwani ya Afrika ya Mashariki***

Baadhi ya wanaisimu kama vile Massamba na wenziwe (1999: 13) wanaamini kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni pwani ya Afrika Mashariki hadi katika baadhi ya maeneo ya nchi ya Somalia. Inasemekana kwamba wenyeji wa maeneo hayo huzungumza lugha zinazoshabihiana sana Kiswahili cha sasa. Baadhi ya lugha hizo ni Kipate kinachozungumzwa katika visiwa vya Pate; Kiamu (Lamu), Kimtang'ata (Tanga na Pangani), Kimvita (maeneo ya pwani ya Mombasa), Kingozi (maeneo ya Pate), Kingazija (maeneo ya kisiwa cha Ngazija), Kipemba (maeneo ya Pemba), Kiunguja kinachozungumzwa maeneo ya Unguja, n.k. Lugha hizo kwa pamoja hujulikana kama *lahaja za lugha ya Kiswahili*, yaani *vilugha* vyenye kufanana na Kiswahili. Mfanano huo ulitokana na mwingiliano wa muda mrefu kati ya Wabantu waliokuwa wakizungumza lugha zao za asili yaani lugha za Kibantu. Hivyo, kwa kuwa ushahidi wa kufanana kwa lahaja, nasi tunaamini kuwa chimbuko la lugha ya Kiswahili ni Pwani ya Afrika Mashariki.

**c) Kuenea kwa Lugha ya Kiswahili**

Kuenea kwa lugha kuna maana ya kusambaa sehemu nyingine zaidi ya pale ilipoanzia. Wanaisimu wanabainisha mambo yafuatayo yaliyochangia kuenea kwa Kiswahili:

**i) Misafara ya Biashara**

Lugha ya Kiswahili ilienea kutoka pwani ya Afrika Mashariki hadi maeneo ya bara ya Tanzania (zamani Tanganyika) kupitia kwa wafanyabiashara wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki waliofanya biashara na jamii za bara ya Tanganyika kabla ya kuja kwa wakoloni. Pia, wafanyabiashara wa Kiarabu walipokuja Afrika Mashariki kwa ajili ya kutafuta *pembe za ndovu* na *watumwa* katika maeneo ya bara ya Tanganyika, Kenya, Mashariki ya Kongo, walihitaji pia watumwa wa kuwabebea mizigo. Hivyo, watumwa wa pwani na bara wakasaidia kuenea kwa Kiswahili.

**ii) Utangazaji Dini za Kigeni**

Mafundisho ya dini ya Kiislamu chini ya Waarabu yalianza kutolewa kwa Kiarabu. Hata hivyo, wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki walikuwa hawaifahamu lugha hiyo. Hivyo Waarabu wakalazimika kujifunza Kiswahili ili waweze kufasili Kuruan, na hivyo dini ya Kiislamu iliwafikia watu wenyeji wa pwani kupitia kwa Waarabu waliojifunza Kiswahili.

Wamisionari walipokuja pwani ya Afrika Mashariki walianza kutumia lugha za kienyeji kuandika vitabu vya dini ya Kikristu. Baadaye, waliona taabu kujifunza lugha za kienyeji pamoja na gharama za uchapishaji vitabu kuwa kubwa. Nao wakalazimika kujifunza Kiswahili ili kueneza mafundisho ya dini zao. Wamisionari wa madhehebu tofauti walianzisha magazeti kwa lugha ya Kiswahili ili waweze kujifunza zaidi lugha hiyo. Kwa mfano, Walutheri walitoa gazeti la ***Habari za Mwezi*** lililoanza kuchapishwa mwaka 1888. Wakatoliki nao walitoa gazeti lililojulikana kama ***Barazani*** katika mwaka 1910. Hivyo, Kiswahili kikazidi kuenea.

**iii) Elimu**

Wakoloni wa Kiarabu walianzisha Madrasa ili kuwafundishwa wenyeji wa pwani ya Afrika Mashariki elimu kuhusu lugha ya Kiarabu. Wajerumani nao walipofika Tanganyika na Zanzibar mwaka 1884, walianzisha shule ndogo ndogo kwa ajili ya wafanyakazi wa ngazi za chini waliotumika katika shughuli za utawala na biashara. Shule hizo pia zilifundisha kwa Kiswahili. Waingereza walipoanza kuitawala Tanganyika na Zanzibar baada ya Ujerumani, nao waliendeleza matumizi ya Kiswahili katika elimu hususani elimu ya Msingi. Mwaka 1925 wakasanifisha lahaja ya Kiunguja ili iwe lugha rasmi ya kufundishia katika nchi zote nne za iliyokuwa Afrika Mashariki (yaani, Tanganyika, Zanzibar, Kenya na Uganda). Hadi leo Kiswahili bado kinaendelea kutumika

kutolea elimu na somo katika ngazi mbali mbali za elimu katika nchi za Afrika Mashariki, na duniani kwa ujumla.

**iv) Vyombo vya Ukuzaji Kiswahili**

Nchi za Afrika Mashariki zilipoanza kupata uhuru mwanzoni mwa miaka ya 1960, zilitaka pia Kiswahili kiendelee kutumika zaidi. Ndipo mwaka 1963, Serikali ya Tanganyika ikaanzisha Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima ambayo ilitoa machapisho kuhusu kisomo kwa lengo la kuwawezesha watu wazima ambao hawakupata fursa ya elimu wakiwa wadogo kupata elimu. Machapisho hayo yaliandikwa kwa lugha ya Kiswahili. Pia, Serikali ilianzisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) mwaka 1967 ili kuratibu shughuli zote za ukuzaji nna utekelezaji wa lugha ya Kiswahili.

**v) Vyombo vya Habari**

Nchini Tanzania, matangazo ya redio Tanganyika na Televisheni Zanzibar yalianza kurushwa kwa lugha ya Kiswahili. Hivyo kukifanya Kiswahili kisambae sehemu mbalimbali za nchi tangu wakati wa ukoloni hadi sasa. Kwa upande wa magazeti, gazeti la "Uhuru" nalo limesaidia kuenea kwa lugha ya Kiswahili kwa jamii.

## Kidokezo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umefurahi kujua historia ya lugha ya Kiswahili ambayo umekuwa ukiitumia katika shughuli zako za kila siku kuanzia nyumbani hadi kwenye jamii. Sasa tufuatane kwa ukamilifu tuweze kujua kuhusu sera ya lugha nchini Tanzania.

**2. Sera ya Lugha Nchini Tanzania**

Dhana ya "sera ya lugha" inaweza kufafanuliwa kama sheria rasmi inayohusu matumizi ya lugha katika jamii, nchi au taifa fulani. Tunaweza kuzigawa sera za lugha nchini Tanzania katika vipindi vikuu vitatu:

**a) Sera ya Lugha Kabla ya Uhuru**

Kabla ya uhuru, hususani wakati wa ukoloni, Kiswahili kiliweza kutumiwa kwa malengo mbalimbali kupitia makundi makuu matatu ya wakoloni: ***i) Wapelelezi na Mawakala wa Ukoloni*** ambao walikiteua na kukitumia Kiswahili kama lugha ya shughuli zao za upelelezi na kueneza dini ya Kikristu. ***ii) Wakoloni wa Kijerumani*** walikiteua Kiswahili kitumike katika elimu na katika ngazi za chini na za juu za utawala wa Kijerumani. Katika ngazi ya chini waliamua kutumia mfumo wa utawala wa moja kwa moja uliowahusisha 'majumbe' na 'maakida' kutoka maeneo ya pwani, ambao walikuwa watumiaji wazuri wa lugha ya Kiswahili. **iii)**

**Wakoloni wa Kiingereza,** nao waliendeleza matumizi ya lugha hiyo katika ngazi za chini za utawala kwa kuwatumia Majumbe, na Maakida. Kiswahili pia kilitumika katika dini. Ili kukidhi vizuri majukumu yao, wakoloni hao wakaanzisha utaratibu wa kuisanifisha lugha ya Kiswahili katika mwaka 1930.

**b) Sera ya Lugha Wakati wa Kupigania Uhuru**

Licha ya Tanzania, hususani iliyokuwa Tanganyika kuwa na lugha nyingi za makabila, wapigania uhuru waliamua kutumia lugha ya Kiswahili ili kuwaunganisha watu wa makabila mbalimbali katika harakati za kudai uhuru. Katika harakati hizo, mikutano ya chama cha Tanganyika African Association (TAA) iliendeshwa kwa Kiswahili. Hata chama cha TAA kilipowezesha kuanzishwa kwa Tanganyika African National Union (TANU) mwaka 1954, bado Kiswahili kiliendelea kutumika. Kwa mfano, zipo kanda za sauti zilizorekodiwa kuhusu Mwalimu Julias Kambarage Nyerere, Bibi Titi Mohamed wakiwahutubia wananchi wa Tanganyika katika harakati hizo.

Aidha, nyimbo zilitungwa kuwahamasisha Watanganyika kuwa na imani na Chama cha TANU katika kuleta ukombozi. Kwa mfano wimbo wa **"*TANU Yajenga Nchi*".**

**c) Sera ya Lugha baada Uhuru**

Baada uhuru ambapo tunaangalia tangu kupata uhuru hadi sasa, Tanzania imekuwa na sera zifuatazo kuhusu lugha:

a) Kiswahili ambayo ni lugha yenye asili ya Kibantu iliteuliwa rasmi kuwa:

- Lugha ya taifa yenye kuunganisha jamii nyingi zenye kutumia lugha tofauti za kiasili.
- Lugha rasmi ambayo hutumika kwenye shughuli rasmi katika nchi; mfano katika Bunge, mahakama,
- Lugha ya kufundishia katika ngazi ya elimu ya awali na shule za msingi ambazo zinamilikiwa na serikali, na pia kama somo katika shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu nchini Tanzania.
- Lugha inayotumika katika vyombo vya habari vilivyo nchini licha ya kwamba vipo vinavyotumia lugha za Kigeni, hususani Kiingereza.

b) Kiingereza ambayo ilikuwa lugha ya kigeni iliyoanza kutumika wakati wa ukoloni iliteuliwa kuwa:

- Lugha rasmi ambayo hutumika katika mawasiliano rasmi ya kimataifa.
- Lugha inayotumika kufundishia katika elimu ya juu, sekondari, na katika shule za awali na msingi za binafsi na baadhi ya shule za msingi za umma, na pia somo katika shule za awali na msingi nchini Tanzania.
- Lugha rasmi ya mawasiliano katika mahakama za ngazi za juu, n.k.

c) Lugha za kiasili ziliamuliwa ziendelee kutumika katika mawasiliano ya kila siku vijijini katika ngazi za familia na shughuli za kiutamaduni za jamii mbalimbali.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Unaielewaje historia ya lugha ya Kiswahili?
2. Onesha nafasi na matumizi ya lugha ya Kiswahili katika jamii za lugha za ulimwengu.

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Tumia hoja na mifano kufafanua historia ya lugha ya Kiswahili.
2. Chambua sera ya lugha nchini Tanzania.

# Somo la Tatu

## Kuchambua Isimu ya Lugha ya Kiswahili

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita, tulijifunza kuhusu historia ya lugha ya Kiswahili ambapo tuliona mahali Kiswahili kilipoanzia. Mwisho, tukachambua sera ya lugha nchini Tanzania. Katika somo hili tutachambua isimu ya lugha ya Kiswahili. Kwa kuanza **tutaeleza maana ya isimu, kufafanua matawi ya isimu, kufafanua matawi ya isimu fafanuzi, na kueleza isimu ya lugha ya lugha ya Kiswahili**. Tunaamini kuwa baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Mpendwa mwanachuo, karibu katika somo hili.

### Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua maana ya isimu;
- Kuchunguza matawi ya isimu;
- Kuchambua matawi ya isimu fafanuzi; na
- Kufafanua isimu ya lugha ya Kiswahili.

### Maana ya Isimu

Mpendwa mwanafunzi, wanaisimu mbalimbali wametoa fasili za dhana ya "isimu" kwa namna tofauti lakini zenye kuelekeana. Kwa mfano, Besha (1994:11) anasema isimu ni taaluma ambayo inachunguza na kuweka wazi kanuni ambazo ndizo msingi wa kila lugha. Anabainisha kanuni hizo kama **maarifa ya mjua-lugha** ambayo ni: (i) Kutambua sauti zinazotumika katika kuunda maneno ya lugha, (ii) Kutambua mfuatano sahihi na usio sahihi wa vipashio vya lugha, (iii) Kutambua tungo zinazovunja kanuni ya sarufi ya lugha na zisizovunja kanuni hizo, (iv) Kutambua sentensi zenye utata, na (v) Kutambua kusudio la sentensi.

Naye Matinde (2012:18), anafasili isimu kuwa ni taaluma inayochunguza na kuchambua lugha (ya wanadamu) kwa kutumia misingi ya kisayansi. Isimu ni sayansi kwa kuwa hufuata mbinu za kimsingi za utafiti wa kisayansi ambazo ni:

**a) Utaratibu Maalum**

Wanaisimu hufanya utafiti na kisha kuwasilisha matokeo ya utafiti wao kwa kutumia vigezo vya kisayansi hatua kwa hatua kuanzia kutambua tatizo la utafiti, kuunda nadharia-tete au makisio ya masuluhisho, kuteua nadharia ya utafiti, kukusanya data, kuchanganua data, na kukubali au kukataa nadharia-tete baada ya kutoa matokeo ya utafiti.

**b) Iktisadi**

Iktisadi au uwekevu ni kitendo cha kutumia kanuni chache kuelezea mambo mengi kwa mara moja. Taaluma ya isimu hutumia kanuni fupi (fomula) katika kuelezea dhana fulani bila kutumia maneno mengi. Sifa hii huifanya isimu iwe taaluma ya kisayansi kama ilivyo kwa fizikia, baiolijia, au kemia. Kwa mfano:

**Isimu: S= KN + KT + KE**

(Hii ina maana kuwa **Sentensi** inaundwa kwa **Kikundi Nomino** pamoja na **Kikundi Kitenzi**, na **Kikundi Kielezi**.

**c) Utonafsi (Urazini/Uhoromo)**

Mtafiti hatakiwi kuhusisha hisia zake na kuzitumia kueleza jambo fulani. Hii ina maanisha kuwa mtafiti hatakiwi kuruhusu hisia zake kuathiri utafiti wake wa kisayansi hata kama ataguswa na suala linalotafitiwa.

**d) Uwazi**

Maswala katika isimu huelezwa kwa udhahiri usio na utata wowote. Yaani hoja huelezwa kwa kina bila kuleta vuguvugu lolote la kimaana.

## Matawi ya Isimu

Isimu ni taaluma yenye matawi mengi sana. Matawi hayo ambayo husaidia katika uchambuzi wa lugha. Baadhi ya matawi hayo ni kama:

### a) Isimu Historia

Kwa mujibu wa Matinde (2012: 39), isimu historia tawi la isimu ambalo huchunguza mabadiliko yanayotokea katika lugha fulani katika kipindi fulani katika historia ya lugha husika. Mabadiliko haya yanaweza kuwa ya kifonolojia, yaani yanayohusu sauti za lugha mahususi, kimofolojia yanayohusu maumbo ya maneno, sintaksia yanayohusu miundo ya sentensi, na hata semantiki yanayohusu maana za maneno. Uchunguzi wa mabadiliko ya lugha kihistoria yanaweza kuwa ya: **(i) kidaikronia**, yaani maendeleo na mabadiliko ya lugha katika vipindi au nyakati mbalimbali, kuanzia chimbuko lake, kukua kwake hadi ilivyo sasa **(ii) kisinkroni** - jinsi lugha ilivyo sasa bila kuangalia ilivyokuwa hapo awali. Pia, huchunguza lugha kwa wakati maalumu kama vile lugha ya Kiswahili ilivyokuwa katika miaka ya 1950, 1960, au 1970, n.k.

### b) Isimu Nafsia/ Saikolojia

Tawi hili la isimu huchunguza jinsi mwanadamu anavyopata ujuzi wa lugha yake, hasa lugha anayojifunza Kinachochunguzwa hapa ni jinsi mtumiaji wa lugha anavyopata ujuzi wa lugha yake katika hatua mbalimbali za makuzi ndani ya jamii anamozaliwa na kukulia.

### c) Isimu Anthoropolojia

Kwa mujibu wa Matinde (2012: 33), tawi hili liliasisiwa na Hymes miaka ya 1960 alipounda dhana ya “Ethnografia ya mawasiliano”. Dhana hiyo ilikuwa ikihusishwa na uchunguzi wa mahusiano baina ya lugha na utamaduni. Kwa mfano, kujua maneno ambayo ni mwiko kuyatamka, lugha gani inatumiwa na rika lipi? n.k.

### d) Isimu Linganishi

Tawi hili la isimu huchunguza lugha zinazozungumziwa ulimwenguni kwa viwango vyote vya isimu kama vile kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, na kisemantiki. Wanaisimu huzichunguza lugha hizi na kuzifafanua kwa undani kisha huzigawa katika makundi mbalimbali kinasaba, kijiografia, n.k.

**e) Isimu Jamii**

Hili ni tawi la isimu ambalo huchunguza uhusiano uliopo kati ya lugha na jamii. Kwa mfano, huchunguza rejesta mbalimbali ambapo hueleza jinsi wazungumzaji wanavyotumia lugha kulingana na uhusiano wao, mada inayohusika, wakati, n.k. Pia, huchunguza jinsi wazungumzaji wanavyomudu *lugha zaidi ya moja* ambayo hujulikana kama *ulumbi* au *wingilugha*, na jinsi lugha hizo zinavyotumika katika jamii; jinsi *lugha tofauti zinavyoathiriana* wakati wazungumzaji wa lugha hizo wanapokutana kwa kuangalia lugha ipi inapewa hadhi ya juu kuliko nyingine, sera za lugha, n.k.

**f) Isimu Fafanuzi**

Hili ni tawi la isimu ambalo huchunguza muundo mzima wa lugha fulani. Kwamba, ndilo tawi linalobeba taaluma nzima ya isimu. Kwani, mwanaisimu hawezi kuunda nadharia zozote kuhusu lugha bila kujua muundo wa lugha hiyo. Ndani ya taaluma hiyo kuna matawi mengine madogo yanayojenga mfumo wa lugha. Matawi hayo ni fonolojia, mofolojia, sintaksia, semantiki na pragmatiki.

**g) Isimu Kokotozi**

Tawi la isimu linaloshughulikia uchanganuzi wa vipengele vya kiisimu kwa kutumia kompyuta au mashine nyinginezo. Kwa mfano, matumizi ya *spektografu* kuweza kubaini jinsi mawimbi ya sauti yanavyosafiri, au ukokotozi wa kompyuta ili kubaini sauti za lugha zinavyotamkwa.

**h) Isimu Matumizi**

Matinde (2012: 40) anaeleza kuwa tawi hili inajishughulisha na kutumia nadharia, mbinu na maarifa ya kiisimu katika kuelezea matumizi ya lugha husika. Kwa mfano, lugha ipi inafaa katika kufundishia lugha hasa ya kigeni, utengenezaji wa kamusi, ufasiri na ukalimani, lugha za matangazo, mahakama, n.k.

## Matawi ya Isimu Fafanuzi

**a) Fonolojia (Isimu Umbo-Sauti).** Ni tawi la isimu linalochunguza mifumo ya sauti za kutamkwa zinazotumika katika

lugha mahususi. Tawi hili hujishughulisha na vipengele kama mfuatano wa sauti/ fonimu irabu, konsonanti na viyeyusho katika kuunda silabi hadi mofu. Tawi hili huhusishwa kwa karibu na tawi la fonetiki kwa kuwa huwezi kujifunza fonolojia ya lugha yoyote ile bila kujua fonetiki ya lugha hiyo.

**b) Mofolojia (Isimu Maumbo).** Ni tawi la isimu linalochunguza na kuchambua kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofu mbalimbali ili kuunda maneno ya lugha fulani.

**c) Sintaksia (Isimu Miundo).** Ni tawi la isimu linalichunguza mpangilio wa vipashio katika tungo za kiwango cha neno, kirai, kishazi, au sentensi.

**d) Semantiki (Isimu Maana).** Ni tawi la isimu linalochunguza maana katika ngazi ya neno, sentensi hadi matini. Semantiki huhusishwa kwa karibu na tawi la pragmatiki kwa kuwa yote huchunguza maana ingawa ni kwa viwango tofauti.

**e) Pragmatiki** ni tawi la isimu linalohusishwa zaidi na semantiki. Huchunguza maana za maneno kwa kuzingatia muktadha yanamotumika.

## Isimu ya Lugha ya Kiswahili

Mpendwa mwanafunzi, tutaelezea isimu ya lugha hii kwa kuzingatia historia yake kama inavyoelezwa na Massamba na wenzake (1999: 46) ambao wao wametumia neno "sarufi".

### a) Isimu ya Lugha ya Kiswahili Iliyoandikwa na Wageni

Wakitumia neno "sarufi" kwa maana ya isimu, Massamba na wenzake (1999: 46) wanasema, watu wa kwanza katika Afrika Mashariki kuelezea isimu ya lugha ya Kiswahili walikuwa wageni, hususani Wamisionari, Wazungu, na baadaye wakoloni. Kwa maelezo ya Massamba na wenzake, Wamisionari waliandika isimu ya Kiswahili kwa ajili ya *kueneza dini za kigeni*. Baadaye wakoloni walitumia Kiswahili kwa ajili ya shughuli zao za *utawala*. Miongoni mwa wanaisimu wa kigeni wa mwanzo

kuandika isimu/sarufi ya Kiswahili alikuwa Askofu Edward Steere aliyeandika kitabu ***Handbook of Swahili Language: As Spoken at Zanzibar*** katika mwaka 1870. Kitabu hiki kiliendelezwa na Madan, A. mwaka 1894. Akinukuu kazi za Steere, Madan (1894: 16), anajaribu kuelezea ngeli (makundi) za nomino za Kiswahili ambayo hupokea maumbo tofauti ya umoja na wingi. Na kwamba, maumbo hayo pia huathiri maumbo ya vitenzi, vivumishi na viwakilishi. Kwa mfano, amebainisha maumbo **M-, Mu-** na **Mw-** katika umoja, na **Wa-** katika wingi kuwa katika ngeli inayohusu viumbe hai/ wanyama; na ngeli ya **M-** *(Mti)* katika umoja na **Mi-** *(Miti)* katika wingi ambayo inahusu viumbe visivyo na uhai. Anaendelea kueleza kuwa kundi la 3 linahusu nomino ambazo maumbo yake ya umoja na wingi hufanana, mfano neno *"**ny**-umba"*.

Aidha, Madan (1894: 226), anabainisha kanuni ya uundaji maneno. Katika hilo, anazungumzia suala la maneno ya mkopo yaliyoingizwa katika lugha ya Kiswahili kuchukua muundo wa lugha hiyo. Kanuni inayoelezwa hapa ni uwekeaji wa irabu mahali ambapo haikuwepo ili kurahisisha utamkaji wa maneno. Mfano, neno **"wákti"** lenye asili ya Kiarabu kufanyiwa marekebisho kwa kupachikwa irabu /**a**/ kati ya konsonanti /**k**/ na /**t**/ hivyo likatamkwa **"wákati"**. Pia, katika ukurasa wa 227 anaelezea kuhusu uundaji wa vitenzi vya mnyumbuliko hususani vitenzi vya usababishi vinavyotokana na vivumishi, na kuchukua maumbo **"isha"** au **"esha"**. Kwa mfano, kivumishi **"laini"** kuwa **"kulainisha"**.

Massamba na wenzake (1999: 47) wanaendelea kuelezea wageni (Wazungu) wengine baada ya Steere ambao nao waliandika kuhusu sarufi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya wageni hao ni Reichat, A na Kuesters, M. walioandika kitabu kilichoitwa ***Elementary Swahili Grammar*** katika mwaka 1926, na Ashton, E. O. aliyeandika kitabu cha ***Swahili Grammar (including Intonantion)*** katika mwaka 1940. Mwandishi mwingine ni Loogman, A. aliyeandika kitabu cha ***Swahili Grammar and Syntax***, mwaka 1965.

Pamoja na Wazungu kuandika mambo mengi kuhusu Kiswahili ambayo bado yanatumika hadi leo, bado kuna mapungufu yanayojitokeza katika baadhi ya dhana. Kwa mfano, fonimu /**th**/ *(**th**ihaka, **th**ahabu, fe**th**eha, ma**th**ehebu, fa**th**ili, Rama**th**ani, na**th**iri, ma**th**ara, bi**th**aa, n.k.)* (Taz. Madan, 1894: 37-55) kutumika badala ya /**dh**/ *(**dh**ihaka, **dh**ahabu, fe**dh**eha, ma**dh**ehebu, fa**dh**ili, Rama**dh**ani, ma**dh**ara, bi**dh**aa, n.k.)* kwa mfuatano. Pia katika

ukurasa wa 87, Madan anaweka na neno **kipofu** na **vipofu** katika kundi la vivumishi badala ya nonimo zinazohusu watu.

**b) Isimu ya Kiswahili Iliyoandikwa na Wazawa wa Lugha ya Kiswahili**

Massamba na wenzake (1999:49) kuwa, waandishi wazawa walianza kuandika vitabu vya sarufi ya Kiswahili katika miaka 1970. Miongoni mwa waandishi wazawa ni Nkwera, F. M.V. aliyeandika kitabu cha ***Sarufi na Fasihi katika Sekondari na Vyuo*** mwaka 1978, Kapinga M.C. aliyeandika kitabu cha ***Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu*** mwaka 1983, Mohamed, Mohamed A. aliyeandika kitabu cha ***Sarufi Mpya*** mwaka 1988), n.k.

Licha ya vitabu hivyo kuandikwa na wazawa wa lugha ya Kiswahili, bado navyo vilikuwa na mapungufu kadhaa. Kwa mfano, baadhi ya vitabu kuwa vigumu kwa walimu wa shule za sekondari. Pia, vitabu vingine vilichanganya baadhi ya mambo. Mfano, **K** (Kiima), **A** (Kiarifu) ***shamirisho*** na ***chagizo*** ambazo ni dhana za *sarufi mapokeo*, kuwekwa pamoja na **KN/ KJ** *(Kikundi Nomino/ Kikundi Jina)* na **FT/ KT** *(Fungu Kitenzi/ Kikundi Kitenzi)* na **KE** *(Kikundi Kielezi)* ambazo ni dhana za *sarufi miundo virai* (Taz. Massamba na wenzake, 1999: 48 na 50).

Mpendwa mwanafunzi, japokuwa vitabu vya awali vilivyoandikwa kuhusu isimu/ sarufi ya Kiswahili kuonekana kuwa na mapungufu, bado vitabu hivyo vimesaidia wanaisimu wengi kufanya utafiti zaidi kuhusu lugha ya Kiswahili na kuandika vitabu vinavyoeleza kwa kina kuhusu isimu ya lugha hiyo. Kwa mfano, Msokile, M. aliyeandika kitabu ***Kunga za Fasihi na Lugha*** (1992), Besha, R. M. aliyeandika kitabu cha ***Utangulizi wa Lugha na Isimu*** (1994), na Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. walioandika kitabu cha ***Sarufi Miundo ya Lugha ya Kiswahili (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo*** (1999). Wengine ni Mgullu, R. S. aliyeandika kitabu ***Mtaala wa Isimu: Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili*** (1999), Habwe, J. na Karanja, P. walioandika ***Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*** (2004), na Philipo, Z. T. T. aliyeandika kitabu ***Sintaksia ya Kiswahili: Misingi na Nadharia za Uchanganuzi wa Kiswahili*** (2013).

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Matawi ya isimu yanaweza kutofautishwaje?
2. Unaelewa nini kuhusu isimu na isimu ya lugha ya Kiswahili?

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Eleza maana ya isimu.
2. Eleza sababu zinazoifanya isimu iwe taaluma ya kisayansi.
3. Fafanua matawi ya isimu.
4. Eleza jinsi waandishi wazawa na waandishi wa kigeni walivyoelezea isimu ya lugha ya Kiswahili.

# Somo la Nne

## Kutumia Fonolojia ya Lugha ya Kiswahili

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita, tulichambua isimu ya lugha ya Kiswahili ambapo tuliona kuwa isimu taaluma inayochambua lugha kisayansi. Aidha, tulifafanua matawi ya isimu pamoja kufafanua matawi ya isimu fafanuzi. Mwisho, tulichambua isimu ya lugha ya Kiswahili kwa kuhusuisha matawi makuu matano yanayojenga isimu fafanuzi. Katika somo hili **tunaeleza jinsi ya kutumia fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Ili kukamilisha somo hili tutafafanua dhana za msingi katika fonolojia, kufafanua dhana ya fonetiki na fonolojia, kuchambua fonimu za lugha ya Kiswahili na kuainisha fonimu za lugha ya Kiswahili.** Mpendwa mwanafunzi, karibu katika somo hii ili uweze kujifunza mambo mbalimbali yanahusiana na fonolojia kwa kuhusisha lugha ya Kiswahili sanifu.

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana za msingi katika fonolojia (foni, fonimu, alofoni, silabi);
- Kutofautisha dhana ya fonetiki na fonolojia ya Kiswahili;
- Kuchambua fonimu za lugha ya Kiswahili; na
- Kuainisha fonimu za lugha ya Kiswahili.

### Dhana za Msingi katika Fonolojia

**a) Foni**

Ni kipashio cha msingi katika taaluma ya fonetiki ambacho huweza kufasiliwa kama kipande kidogo cha sauti ambacho hutamkwa na binadamu. Kipande sauti hiki hakiwezi kuhusishwa na lugha yotote mahususi (Hakuna lugha yoyote duniani inayoweza kudai kuwa foni fulani ni yake). Foni huwakilishwa kwa ishara za kifonetiki zilizo katika mabano mraba [ ]. Kwa mfano, [X] hutamkwa /kh/. Sifa muhimu za foni:

i) Hudhihirika kimatamshi,

ii) Hudhihirika kimaandishi,

iii) Haina maana (kwani kila foni huangaliwa kiupekee bila kuhusisha foni nyingine).

iv) Huwakilishwa kimaandishi kwa kutumia alfabeti za kifonetiki zilizo katika mabano mraba **[ ].**

**b) Fonimu**

Fonimu ni kipashio cha msingi katika taaluma ya fonolojia. Kipashio hiki hufasiliwa kuwa ni kipande kidogo kabisa cha sauti ambacho hutumika kuunda maneno yenye maana tofauti. Fonimu ndizo sauti za msingi katika lugha. Kwa mfano ;

/u/ /n/ /a/ /**s**/ /**o**/ /m/ /a/ /u/ /n/ /a/ /**s**/ /**e**/ /m/ /a/

**Unasoma** na **unasema** ni maneno ya lugha ya Kiswahili. Maana ya neno ‘*unasoma’* imebadilika au kupotea kutokana na fonimu **/e/** katika neno ‘unasema’ kuchukua nafasi ya fonimu **/o/.** Hapa, fonimu **/o/** na **/e/** ndizo zilizotumika kubadili maana katika maneno hayo kutoka lugha ya Kiswahili. Sifa za fonimu :

i) Hudhihirika kimatamshi

ii) Hudhihirika kimaandishi

iii) Huwa na maana

iv) Huwakilishwa kimaandishi kwa kutumia alfabeti za kifonetiki zilizo katika mabano mshazali / /

**c) Alofoni**

Alofoni ni *matamshi tofauti yanayowakilisha fonimu moja*. Tofauti hizo za matamshi zinaweza kubadili maana au zisibadili maana kulingana na mfumo wa lugha. Kwa mfano, mtu akisema *ku/**l**/a* kwa maana ya *ku/**r**/a*; basi hapa [**r**] na [**l**] hutambulika kama alofoni za fonimu [**r**] kwa kuwa hazijabadili maana. Pia, sauti /t/ isiyo na mpumuo na /$t^h$/ yenye mpumuo katika lugha ya Kiingereza ni alofoni za fonimu /t/ kwa kuwa mpumuo ni sifa inayotambulisha alofoni katika lugha hiyo. Alofoni hizo zina mazingira tofauti ya utokeaji. Wakati /$t^h$/ kama katika neno */till/* hutokea mwanzoni mwa neno, na /t/ kama katika neno */still/* huwa hazijitokezi mwanzoni mwa neno.

Mpendwa mwanafunzi, ukumbuke kwamba, sauti mbili zinaweza kuwa alofoni katika lugha moja lakini zikawa fonimu tofauti katika lugha nyingine.

**d) Silabi**

Silabi ni kipashio cha kifonolojia ambacho hubainisha jinsi sauti za lugha zinavyotamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti linalojitegemea. Fungu hili huweza kuwa na sauti moja peke yake, mbili au zaidi kutegemeana na muundo wa lugha. Kuna aina mbili za silabi:

i) ***Silabi Huru***

Hii ni aina ya silabi ambayo huishia na irabu. Silabi za aina hii zinapoishia na irabu hujulikana kama silabi zenye kilele. Kwa mfano $ n**a** $

ii) ***Silabi Funge***

Hii ni silabi ambayo huishia konsonanti. Silabi hizi zenye kuishia na konsonanti hujulikana kama silabi zenye ukingo. Kwa mfano;

$la**b**$ $ da $

$ **Al** $ ha $ mi $ si $, n.k.

## Dhana ya Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili

**a) Dhana ya Fonetiki**

Matinde (2012: 43) anaeleza kuwa fonetiki (phonetics) ni neno lenye asili ya Kigiriki linaloundwa na maneno mawili; "phone" likiwa na maana ya *sauti*, "tica" likiwa na maana ya uchunguzi. Hivyo, fonetiki ni taaluma ya uchunguzi wa sauti. Kwa fasili rasmi tunaweza kusema, fonetiki ni tawi la isimu linalochunguza sauti za lugha za wanadamu. Sauti zinazochunguzwa katika taaluma hii ni zile zinazotamkwa na binadamu wala sio sauti kama za kucheka, kulia, kukohoa, kupiga chafya, n.k. Kipashio cha msingi katika taaluma hii hujulikana kama **foni**. Kipashio hiki hakina maana katika taaluma ya lugha. Wanaisimu wanadai kuwa fonetiki ni moja tu tofauti na fonolojia zipo nyingi kama lugha zenyewe zilivyo nyingi. Kwa mfano, hatuna fonetiki ya Kiingereza au fonetiki ya Kiswahili.

Kwa mujibu wa Besha (1994: 18), taaluma ya fonetiki ilianza kujulikana sana katika karne ya 18 (B.B). Katika kipindi hicho, walimu wa lugha wa Ufaransa waliunda shirika la kifonetiki la kimataifa mfumo wa matamshi baada ya kugundua umuhimu wa taaluma ya fonetiki katika kazi yao. Matinde (2012: 54) anasema kuwa, wazo la kuanzisha mfumo wa alfabeti za kifonetiki lilitolewa na *Otto Jespersen* katika mwaka 1886. Ndipo mwaka 1888 kikaundwa *Chama cha Kimataifa cha Fonetiki*, na orodha ya kwanza ya alfabeti za kifonetiki ilichapishwa katika mwaka huo. Matinde anaendelea kueleza kuwa, wanafonetiki walianza kuunda alfabeti maalumu itakayowakilisha sauti za lugha katika unukuzi/maandishi ili kurahisha mawasiliano. Herufi hizo ziliwekwa pamoja katika "Alfabeti za Kifonetiki Kimataifa" (AKIKI) ambazo katika lugha ya Kiingereza zilijulikana kama *The International Phonetic Alphabet* (IPA). Lengo la chama hicho ilikuwa kuunda alfabeti moja kwa kila sauti.

### b) Matawi ya Fonetiki

Taaluma ya fonetiki ina matawi mbali mbali. Massamba na wenzake (2004: 5) wanaainisha matawi makuu manne:

#### *i) Fonetiki Matamshi*

Tawi hili huchunguza jinsi sauti mbalimbali za lugha zinavyotamkwa kupitia ala mbalimbali za matamshi kama vile mdomo, meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini, glota (koromeo), n.k.

Kibaiolojia mwanadamu ana viungo mbalimbali vinavyofanya kazi maalumu kama vile mguu, mikono, kichwa, midomo, masikio, pua n.k. Kila moja ya kiungo hiki kina kazi zake maalumu katika utaratibu mzima wa hutoaji na upokeaji wa sauti za mwanadamu. Kwa mfano, mdomo wa binadamu una viungo vyake vidogo kama vile meno, ulimi, fizi, koromeo, n.k vyenye majukumu mbalimbali. Hata hivyo, viungo vya midomo wa mwanadamu vina jukumu lingine la ziada katika lugha la kufanya sauti mbalimbali ziweze kutamkwa inavyopaswa. Vilevile, pua ya mwanadamu ni kwa ajili ya kunusa lakini hutumika kutoa sauti. Sehemu zote hizi zinazohusika katika kutolea sauti huitwa ***ala za sauti.*** Ala sauti hizi huwa katika mkondo wa bomba lililo wazi upande wa

kinywani na lililofungika upande wa mapafuni. Kimsingi alasauti hizi zipo za namna mbili; *alatuli* na *alasogezi*:


**(a) Ala tuli**

Hizi ni alasauti ambazo wakati wa utamkaji wa sauti za lugha huwa hazijisogezi. Mfano wa ala hizi ni mdomo wa juu, meno ya juu, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini na koromeo.

**(b) Ala sogezi**

Hizi ni alasauti ambazo zinajimudu. Wakati wa kutamka sauti za lugha alasauti hizi huwa zinajisogeza kuelekea alatuli. Alasauti hizi ni kama mdomo wa chini, ulimi, kidakatonge, nyuzisauti (zilizo kwenye koromeo) na mapafu.

**Alasauti za Lugha**




*1. Midomo 2. Meno juu 3. Ufizi 4. Kaakaa gumu 5. Kaakaa laini 6. Kidaka tonge 7. Meno chini 8. Ncha ulimi 9. Kiwiliwili (Bapa ulimi) 10. Shina ulimi (Nyuma ulimi) 11. Koromeo*

**Chanzo: Massamba na wenzake (2004:4)**

Mpendwa mwanafunzi, hebu tuone jinsi ala za matamshi pamoja na namna ya utamkaji zinavyobainishwa na wanafonetiki.

**Ala za Matamshi/ Mahali pa Matamshi**

**(a) Midomo**

Mdomo wa juu na mdomo wa chini ambayo ni ala sogezi hutumika kuzuia na kuiachia ghafla hewa ya kinywani. Mfano wa sauti zinazotamkiwa hapa ni **[p], [b], [m],** n.k.

**(b) Mdomo-Meno**

Mdomo wa chini hugusanishwa na meno ya mbele yaliyo juu, na kuzuia kwa kiasi fulani mkondo hewa kutoka kinywani. Mfano wa sauti zinazotamkiwa hapa ni **[f], [v], [ɱ].**

**(c) Meno**

Meno ni miongoni mwa ala za utamkaji ambazo ni tuli. Wakati wa kutamka foni ulimi hugusishwa kwenye meno ya mbele na kubana kidogo hewa inayosukumwa taratibu. Mfano wa zinazotamkiwa hapo ni **[ð] = *dh*, [θ] = *th*.**

**(d) Ufizi**

Ni ala ya matamshi ambayo ndiyo inayoshikilia meno. Wakati wa kutamka sauti hizi ncha ya ulimi hugusa ufizi kama tunapotamka sauti **[d], [t**], na **[n]**; kupigapiga kwenye ufizi kama tunapotamka sauti [r] **na [l]** au huukaribia ufizi kama tunapotamka sauti **[z]** na **[s]**.

**(e) Kaakaa Gumu**

Kaakaa gumu ni sehemu ya juu katika chemba ya kinywa iliyo nyuma ya ufizi. Sehemu hii huwa na matuta (jaribu kupitisha ulimi wako ili kuibaini). Wakati wa kutamka sauti za lugha **ulimi** huweza kugusa kwenye kaakaa gumu kama tunapotamka sauti **[č] au [ʧ] = *ch*, [ɲ]= ny,** na **[ Ɉ ]** = j; au kukaribia kwenye kaakaa gumu wakati tunapotamka sauti **[š] au** [ʃ] **= *sh*** na **[j] = y.**

**(f) Kaakaa Laini**

Ni ala tuli ambayo hujitokeza baada ya kaakaa gumuUlimi huinuliwa na kugusa kaakaa laini. Hapa tunapata sauti kama **[k], [g], [ŋ] = *ng'*** na **[ɣ] = *gh***.

**(g) Koromeo (Glota)**

Sauti za koromeo hutokea wakati nyuzi sauti zinapokutanishwa kwa muda mfupi. Nyuzi sauti ni kamba laini za nyama kwenye kisanduku cha sauti. Mfano wa sauti zinazotamkiwa kwenye glota

ambazo ni chache ni **[h] na [ɦ]** kama tunapotamka neno **“*Hamis*” au ɦ**.

**(h) Pua**


Pua ni ala tuli ambayo hutumika kupitisha hewa wakati wa kutamka foni za nazali. Kwa mfano, **[m], [n],** n.k.

**(i) Mapafu**

Mapafu ni ala sogezi ambayo hupatikana ndani ya bomba la sauti. Ndiyo yanayosaidia kutoa hewa nje wakati tunapozungumza. Hewa inayosukumwa nje ya bomba la sauti huitwa **mkondohewa-nje**, na ule unaorudisha hewa ndani huitwa **mkondohewa-ndani**. Sauti nyingi za lugha hutamkwa kwa mkondohewa-nje (Habwe na Karanja, 2004: 24).

**(j) Ulimi**

Ulimi ni miongoni mwa ala sogezi. Hii ni ala muhimu sana katika utamkaji wa sauti za lugha. Ala hii imegawanyika katika sehemu kuu tatu: *ncha ya ulimi (sehemu ya mbele ya ulimi), bapa la ulimi (sehemu ya kati ya ulimi),* na *shina la ulimi (sehemu ya nyuma ya ulimi).* Ulimi husaidia sana katika utamkaji wa irabu. Tunapotamka foni irabu ulimi huinuliwa kwa viwango mbalimbali kama vile *juu, nusu-juu* sambamba na paa la kinywa, *nusu-chini* au kuwa chini sambamba na uvungu wa kinywa. Chunguza kielelezo kifuatacho cha irabu-msingi (cardinal vowel):




Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004: 38) hali za alasauti za midomo na ulimi husababisha kuwe na idadi tofautitofauti za irabu katika lugha za ulimwengu. Mfano lugha ya Kiswahili ina irabu

tano (5), wakati lugha ya Kisukuma ina irabu saba (7). Fanya uchunguzi wa idadi ya irabu za lugha mbalimbali duniani.

### (ii) Namna ya Utamkaji

Namna ya utamkaji hurejelea jinsi ambavyo hewa inayopita katika bomba la sauti huzuiwa kwa namna mbalimbali wakati wa kutamka sauti za konsonanti.

#### (a) Kipasuo

Kipasuo (Plosive/ Stop), ni namna ya utamkaji wa sauti za lugha ambapo hewa itokayo mapafuni huzuiwa kabisa na kisha huachiwa ghafla. Hewa inapoachiwa hutokea sauti ya mlipuko (mf. unapojaza upepo katika tairi la baiskeli kwa kutumia pampu). Vipasuo huweza kupangwa kutegemeana na mahali pa kutamkiwa:

i) *Vipasuo vya midomo*: Hizi ni sauti [p] na [b] ambazo hutamkwa kwa midomo yote miwili.

ii) *Vipasuo vya ufizi*: sauti hizi ni [t] na [d] ambazo hutamkwa na ncha ya ulimi inapogusana na ufizi wa juu

iii) *Vipasuo vya kabla ya kaakaagumu*: hutamkwa kabla ya kaakaa gumu [ ʈ ] na [ ɖ ]

iv) *Vipasuo vya kaakaa gumu*: Hizi ni sauti [č] na [Ɉ] zinazotamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na kaakaa gumu

v) *Vipasuo vya kaakaa laini*: Hizi ni sauti [k] na [g] zinazotamkwa wakati bapa la ulimi linapogusana na kaakaa laini.

vi) *Vipasuo vya kwenye kidakatonge*: Hizi ni sauti [ q ] na [ɢ]

vii) *Vipasuo vya kwenye glota (koromeo)*: Hizi ni sauti [ʔ]

#### (b) Nazali/ King'ong'o

Nazali (Nazal), ni sauti ambazo hutamkwa wakati hewa itokayo mapafuni inapozuiwa isipite kupitia mdomoni wakati kidaka tonge kinapokuwa kimeteremka, badala yake hupitia puani. Sauti hizi ni kama

i) [m]: hutamkwa kwenye *midomo* yote miwili kama katika neno

ii) [ɱ]: hutamkwa kwenye *midomo-meno*. Katika Kiswahili sauti hii haipo bali hujitokeza katika utamkaji tu "mv" kama katika neno "*m*vi".

iii) [n] Hutamkwa wakati ncha ya ulimi inagusana na *ufizi* wa juu.

iv) [ɳ] hutamkwa wakati bapa la ulimi inakaribia kugusa kaakaa gumu

v) [ɲ] Hutamkwa wakati bapa la ulimi linapogusana na *kaakaa gumu*.

vi) [ŋ] Hutamkwa wakati bapa la ulimi linagusana na *kaakaa laini*.

vii) [N] Hutamkwa wakati shina la ulimi linagusana na *kidakatonge*.

**(c) Kimadende**

Kimadende (Trill), ni namna ya utamkaji ambapo ala ya sauti hulegezwa inapogusana na ala sauti nyingine na kufanya mkondohewa upite katika hali ya mtetemo. Sauti zinazotamkwa kwa namna hiyo ni;

i) [B] *kimadende cha midomo* hutamkwa kwa kupigapiga kwa haraka mdomo wa chini na wa juu baada ya kugusana

ii) [r] *Kimadende cha ufizi* hutamkwa ncha ya ulimi inapogusa *ufizi* wa juu kwa kupigapiga upesi. Mfano wa sauti hizi ni (rejea muungurumo wa gari rrrrrrrrr).

iii) [ʀ] *Kimadende cha kidakatonge*

**(d) Kipigo**

Kipigo (Tap/ Flap), ni namna ya utamkaji wa sauti kama ilivyo kimadende lakini yenyewe hutamkwa kwa haraka baada ya ala sogezi kugusa ala tuli mara moja kwa haraka. Sauti hizo hutegemeana na mahali pa matamshi

i) *Kipigo cha midomo-meno* [ⱱ]

ii) *Kipigo cha ufizi* [ ɾ ] kama neno *la*t*er* linavyotamkwa kwa Kiingereza cha Marekani (haitamkwi kama t ya kawaida)

iii) Kipigo *kabla ya kaakaa gumu* [ ɽ ]

**(e) Kikwamizi**

Kikwamizi (Fricative), hutokea hewa inapozuiwa na kisha kuruhusiwa kutoka taratibu. Wakati wa kutamka sauti za

vikwamizi hewa itokayo mapafuni huwa haizuiwi moja kwa moja, bali kunakuwepo na mwanya kidogo wa kupitishia hewa (kama mpira wenye pancha). Sauti za vikwamizi zimegawanyika katika makundi yafuatayo kutegemeana na mahali pa matamshi:

i) *Vikwamizi vya midomo*: sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapogusana na mdomo wa juu. Kwa mfano sauti [ɸ] = Brrrrrrr na [β] = $B^h$.

ii) *Vikwamizi vya midomo-meno*: sauti hizi hutamkwa wakati mdomo wa chini unapogusana na meno ya juu. Kwa mfano sauti [f] na [v].

iii) *Vikwamizi vya meno*: Hizi hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapokuwa katikati ya meno. Kwa mfano sauti [θ] na [ð].

iv) *Vikwamizi vya ufizi*: sauti hizi ni [s] na [z] ambazo hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapogusana na ufizi wa juu

v) *Vikwamizi vya nyuma ya ufizi (baada ya ufizi)*: sauti hizi hutamkwa wakati ambapo bapa la ulimi kwa mbele linapokaribia kugusana na kaakaa gumu. kwa mfano sauti

vi) *Vikwamizi vya kabla ya kaakaa gumu*: [ʂ] kama katika neno ***Sh**anghai* ambalo kwa Kichina cha Mandalin hutamkwa [ʂɑŋhai] na [ʐ]

vii) *Vikwamizi vya kaakaa gumu*: [ç] na [ʝ]

viii) *Vikwamizi vya kaakaa laini*: hizi ni sauti ambazo hutamkwa wakati bapa la ulimi kwa nyuma limapogusana na kaakaa laini. Mfano sauti [Ɣ]

ix) *Vikwamizi vya kidakatonge* [χ] na [ʁ]

x) *Vikwamizi vya koo* [ħ] na [ʕ]

xi) *Vikwamizi vya glota*: hizi ni sauti zinazotamkiwa kwenye koromeo mfano sauti [h] na [ɦ].

**(f) Kitambaza-Kwamizi**

Kitambaza-kwamizi (Lateral-fricative), ni namna ya utamkaji ambapo sauti inapotamkwa hewa hupita katika njia nyembamba kiasi cha kusababisha msukumo mdogo wa hewa na kasi ya utamkaji wa sauti kupungua. Sauti zinazohusika hapa ni vilainisho tambaza vya ufizi, sauti moja ikiwa ghuna na nyingine si ghuna. Sauti zenye sifa hii ni [ɬ] (tamka tla) na [ɮ].

### (g) Kitambaza

Kitambaza (Lateral), hutolewa wakati ambapo hewa kutoka mapafuni huzuiwa na ncha ya ulimi inapogusana na ala fulani ya matamshi na kuacha hewa ijisambaze pembeni mwa ulimi. Sauti hizi ni [ l ] kitambaza cha ufizi wa juu, [ ɭ ] kitambaza cha kabla ya kaakaa gumu, [ʎ ] kitambaza cha kaakaa gumu, na [ ʟ ] kitambaza cha kaakaa laini.

### (h) Kiyeyusho

Viyeyusho (Approximant), ni sauti ambazo ziko katikati ya irabu na konsonanti. Mara nyingi huitwa nusu-irabu. Wakati zinapotolewa huwa kuna mzuio mdogo sana wa mkondohewa. Wakati wa kuzitamka sauti hizi ulimi husogea harakaharaka kutoka au kuelekea kwenye irabu iliyo karibu. Tofauti kubwa kati ya sauti za viyeyusho na irabu ni kuwa wakati irabu ni silabi zenyewe hazina sifa hiyo. Mfano wa sauti hizo ni [ ʋ ] kiyeyusho cha midomo-meno (mf. veve), [ ɹ ] kiyeyusho cha ufizi**,** [ ɻ ] kiyeyusho cha kabla ya kaakaa gumu**,** [ j ] kiyeyusho cha kaakaa gumu na [ ɰ ] kiyeyusho cha kaakaa laini.

**Jedwali 5: Alfabeti za Kifonetiki za Kimataifa**

| | **Midomo**<br>- + | **Midomo-meno**<br>- + | **Meno**<br>- + | **Ufizi**<br>- + | **Nyuma ya Ufizi**<br>- + | **Kabla ya Kaakaa gumu**<br>- + | **Kaakaa gumu**<br>- + | **Kaakaa laini**<br>- + | **Kidakatonge**<br>- + | **Koo**<br>- + | **Koromeo**<br>- + |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Vipasuo** | p b | | | t d | | ʈ ɖ | č ɟ | k g | q ɢ | | ʔ |
| **Nazali** | m | ɱ | | n | | ɳ | ɲ | ŋ | N | | |
| **Vimadende** | B | | | r | | | | | ʀ | | |
| **Vipigo** | | ⱱ | | ɾ | | ɽ | | | | | |
| **Vikwamizi** | ɸ β | f v | θ ð | s z | ʃ ʒ | ʂ ʐ | ç ʝ | x ɣ | χ ʁ | ħ ʕ | h ɦ |
| **Vikwamizi-tambaza** | | | | ɬ ɮ | | | | | | | |
| **Viyeyusho** | | ʋ | | ɹ | | ɻ | j | ɰ | | | |
| **Vitambaza** | | | | l | | ɭ | ʎ | ʟ | | | |

**Chanzo:** Imerekebishwa kutoka IPA (2018) http://upload.wikimedia.org.com

Jedwali 5 linaonesha mahali pa kutamkia sauti za lugha, namna ya utamkaji na hali ya glota, yaani kuwa ghuna au si ghuna.

### *ii) Fonetiki Akustiki*

Hili ni tawi la fonetiki ambalo huchunguza jinsi sauti zinazotamkwa na mwanadamu zinavyoweza kusafiri kutoka kwa mzungumzaji hadi kwa msikilizaji. Kinachochunguzwa hapa ni mawimbi ya sauti yanavyosafiri kama ni kwa haraka sana, polepole, n.k.

*iii) Fonetiki Masikizi*

Tawi hili huhusika na uchunguzi wa namna mwanadamu anavyoweza kupokea sauti kupitia sikio lake, kuisafirisha hadi katika ubongo wake, kuitafsiri na kisha kupata maana fulani. Kutokana na tawi hili ndipo msikilizaji anaweza kubaini usahihi au makosa ya utamkaji yaliyofanywa na mzungumzaji. Kwa mfano, mzungumzaji wa lugha ya Kiswahili anayesema **thatha**; msikilizaji anaweza kubaini wazi mzungumzaji alikusudia kusema neno **sasa** ambalo ndilo sahihi.

*iv) Fonetiki Tiba-Matamshi*

Tawi hili huhusika na matatizo yanayoambatana na usemaji au utamkaji wa sauti na jinsi ya kuyatatua. Kwa mfano, kuna tatizo la mtu kuzaliwa na paa la kinywa au kaakaa lililogawanyika ambalo huathiri matamshi katika usemaji. Katika tawi hili lengo ni kujaribu kuchunguza na kutafuta ni kwa jinsi gani sauti zinazotamkwa na watu wenye matatizo kama hayo zinavyoweza kubainishwa. Kwa mfano, kwa kawaida irabu sio nazali. Lakini wapo baadhi ya watu wenye matatizo ya utamkaji huzungumza irabu [a] kwa kupitishia hewa puani kama zilivyo kwa nazali [m], [n], [ɲ] (tamka ny). Hivyo, wanafonetiki huipa **alama bandikizi** ya wimbi (~) juu ya sauti hiyo.

## 2. Dhana ya Fonolojia

### a) Maana ya Fonolojia

Fonolojia pia hujulikana kama umbosauti. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004: 42), fonolojia ni utanzu wa isimu unaochunguza jinsi sauti za lugha zinavyofanya kazi katika lugha mbalimbali (za wanadamu). Massamba (2004: 12) anafasili fonolojia kuwa ni tawi la isimu ambalo hushughulika na uchunguzi na uchanganuzi wa mfumo wa sauti za lugha (za wanadamu).

Kwa ufupi tunaweza kusema kuwa *fonolojia ni taaluma ya isimu inayochunguza mfumo wa sauti katika lugha mahususi.* Kwa mfumo tuna maana ya **utaratibu** wa kuunda maneno ya kila lugha ya mwanadamu. Kwa mfano jinsi fonimu zinavyoungana kuunda silabi hadi yanapopatikana maneno ya lugha husika. Kila lugha ina mfumo au utaratibu wake wa kuunda maneno. Ndio maana tuna fonolojia za kila lugha mahususi kama vile fonolojia ya lugha ya Kiswahili, fonolojia ya lugha ya Kiingereza, fonolojia ya lugha ya Kisukuma n.k. Kipashio cha msingi cha taaluma hii hujulikana kama **fonimu**.

**b) Matawi ya Fonolojia**

Taaluma ya fonolojia ina matawi mawili;

**(i) Fonolojia Vipande**

Hili ni tawi la fonolojia ambalo huchunguza vitamkwa au sauti za lugha mahususi. Kitamkwa ni sauti dhahiri inayosikika wakati wa utamkaji maneno na ambayo huweza kubainishwa kama kitu kimoja ambacho huweza kuwakilishwa kimaandishi kwa kutumia alama zijulikanazo kama herufi za alfabeti. Vitamkwa hivyo huweza kuwa katika ngazi ya silabi au neno

**(ii) Fonolojia Arudhi**

Hili ni tawi la fonolojia ambalo huchunguza mpangilio vipandesauti (fonimu na alofoni), pamoja na sifa zinazoambatana na utamkaji wa vipandesauti hivyo. Sifa hizi pia hujulikana kama **vipambasauti** ambavyo ni:

**a) Mkazo/ Shadda**

Ni hali ya neno au silabi katika neno kusikika kwa nguvu zaidi kuliko maneno au silabi nyingine. Katika lugha za Kibantu (Kiswahili kikiwemo), mkazo kuwekwa katika silabi ya pili kutoka mwisho. Lakini maneno ya kigeni yanafuata utaratibu mwingine. Kwa mfano:

**Kiswahili:** /Ba′**ra**: bara/ = sawasawa (kielezi) (asili ya Kiarabu)

/Bara′**ba**ra/ = njia (nomino)

Mpendwa mwanafunzi, dhima kuu ya mkazo ni kutofautisha kategoria na maana za maneno ambayo kiotografia (kimaandishi) huwa sawa lakini homografu (kimatamshi) huwa tofauti. kwa kawaida mkazo huweza kujitokeza katika ngazi ya neno au katika ngazi ya sentensi. Kwa mfano,

*a) M'**to**to* *b) Mtoto anakula '**e**mbe.*

Mfano a) unaonesha mkazo katika neno ambapo umewekwa katika silabi **$ to $** ya neno **mtoto,** na mfano b) unaonesha mkazo katika sentensi ambapo mkazo umewekwa katika silabi **$ e $** ya neno **embe).** Ili kubainisha mkazo, wanafonetiki hutumia alama [ ′ ] ambayo huwekwa juu ya irabu ya silabi yenye mkazo.

**b) Kiimbo**

Ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati mtu anapozungumza. Kupitia kiimbo, ndipo tunaweza kubaini kusudio la msemaji kama anauliza swali, anatoa taarifa, anatoa amri, au anashangaa. Kutokana na namna mzungumzuji anavyoweza kupandisha au kushusha sauti wakati wa kuzungumza tunaweza kupata aina mbalimbali za kiimbo:

- Kiimbo cha maelezo au taarifa: Kaka amenipiga.
- Kiimbo cha kuuliza: Nani amekupiga?
- Kiimbo cha amri: Nimesema, "usirudie tena kumpiga!"
- Kiimbo cha mshangao: Amekupiga!

**c) Kidatu**

Kidatu ni kiwango cha msikiko wa sauti katika usemaji. Kidatu kinaweza kuwa cha chini sana, kati au juu. Hivyo, tunaweza kuwa na sauti ya kidatu cha juu, kidatu cha kati au kidatu cha chini. Kidatu kwa kawaida hufungamana na kiimbo kwa vile ndicho kinachoweza kutuonesha kiwango cha sauti kuwa kimepanda au kimeshuka kwa kiasi gani. Kidatu humwezesha mzungumzaji kubadili kiwango chake cha sauti katika usemaji kutoka juu na kwenda chini, na kinyume chake.

**d) Toni**

Toni inaweza kufasiliwa kama kidatu katika silabi zinazojenga neno. Yaani, ni kiwango cha msikiko wa sauti inayojitokeza katika silabi mbalimbali zinazojenga neno. Kwa mujibu wa Chama za Alfabeti za Kimataifa (2015), kuna aina mbalimbali za toni. Baadhi ya toni hizo ni:

Toni juu ( ′ ), toni chini ( ˋ ), toni kati ( ˉ ), toni ya kupanda ( ˇ ) yaani sauti inaanzia chini na kisha kupanda, toni ya kushuka ( ˆ ) yaani sauti inaanzia juu na kisha kuteremka.

Mpendwa mwanafunzi, kuwepo kwa toni kumesaidia kubainisha maana ya neno na njeo au hali za vitenzi. Endapo toni itabadilisha maana, basi toni hiyo itajulikana kama **toni ya kileksika** (Pia toni ya kikamusi/ kimsamiati). Lakini, kama itabadilisha njeo au hali ya kitenzi basi toni hiyo itajulikana kama **toni ya kisarufi**.

Kimaandishi, alama ya toni huwekwa kwenye irabu ya silabi yenye toni. Lugha ya Kiswahili haina toni ingawa baadhi ya lugha za Kibantu zina toni. Tuangalie baadhi ya mifano kutoka Massamba,

(2011: 169): [ákwá] likiwa na maana ya "kulia", [àkwà] likiwa na maana ya "yai"

**e) Wakaa**

Wakaa ni muda ambao hutumika kutamka sauti katika lugha. Katika Kiswahili kuna wakaa wa kawaida na wakaa mrefu ambao hujibainisha tunapotamka irabu za kufanana ambazo zimeambatana. Katika maandishi, wakaa mrefu hubainishwa kwa kurudiwarudiwa kwa irabu. Lakini, tunaponukuu sauti kifonetiki, alama ya nukta mbili/ nukta-pacha **(:)** hutumika kuonesha kuwa fonimu fulani imerudiwa. Mfano,

| **Wakaa Mrefu (Kimaandishi)** | **Wakaa Mrefu Kifonetiki** |
|---|---|
| Kakamaa | [kakama:] |
| Juu | [ɟu:] |

**f) Lafudhi**

Lafudhi ni matamshi ya mzungumzaji wa lugha ambayo hutokana na athari za kimazingira yanayoweza kutambulisha eneo lake la kijiografia au kijamii analotoka. Kwa kusikiliza lafudhi ya mtu ndipo tunapoweza kubaini kwa urahisi kuwa anatoka eneo au katika jamii fulani. Mfano, kuna baadhi ya watu huzungumza Kiswahili kwa lafudhi ya Kisukuma, Kichaga, Kimakonde, Kikongo n.k, kama katika mfano ufuatao :

> *Baba kaleta chamaki nchanga* (lafudhi ya Kimakonde), mzungumzaji huyo anatokea Mtwara.

**g) Silabi**

Ni kipashio cha kifonolojia ambacho sauti hutamkwa kwa pamoja kama fungu moja la sauti linalojitegemea. Fungu hili huweza kuwa na sauti moja peke yake, mbili au zaidi kutegemeana na muundo wa lugha. Katika lugha nyingi silabi zimegawanyika katika aina kuu mbili; (i) **Silabi huru;** ni silabi ambayo huishia na *kilele* ikiwa na maana ya silabi inayoishia na irabu. Mfano, **a-na-pi-ka.** Silabi huru zinapotamkwa huwa na msikiko wa juu na (ii) **Silabi funge;** ni aina ya silabi inayoishia na *ukingo*, ikiwa na maana ya silabi inayoishia na konsonanti. Mfano, **al**-fa-ji-ri. Silabi funge inapotamkwa huwa na msikiko hafifu.

**h) Otografia**

Massamba na wenzake (2004:12), wanafasili otografia kuwa ni neno lenye asili ya Kigiriki lenye maana ya utaratibu wa kutumia alama au michoro ya maandishi kuwakilisha sauti zisisikazo katika usemaji wa lugha. Utaratibu huu wa uundaji wa silabi na mofimu

huweza kufanana au kutofautiana kati ya lugha moja na nyingine. Wataalamu wa lugha inayohusika hubuni utaratibu wa maandishi ambao utatumika kama mfumo wa maandishi katika lugha hiyo. Mfumo huo wa maandishi unaweza kuwa wa alama (mfano alama za alfabeti zinazotumika katika lugha ya Kiswahili), au michoro (kama inavyotumika katika lugha ya Kichina, Kihindi, n.k.). Kutokana na hali hiyo, ni wazi pia kwamba kila lugha itakuwa na utaratibu wake wa uwakilishaji wa maneno yake, iwe kimaandishi au kiusemaji.

## Fonimu za Lugha ya Kiswahili

Lugha ya Kiswahili kama ilivyo kwa lugha nyingi duniani ina fonimu tatu.

**a) Irabu**

Irabu ni fonimu ambayo hutamkwa bila mzuio wa hewa itokayo kwenye mapafu. Wakati wa kutamka irabu ala za matamshi huwa zimeachana kiasi cha kwamba hakuna mgusano wa ala inayohusika. Lugha ya Kiswahili ina jumla ya fonimu za irabu tano ambazo kifonetiki huandikwa /a, **ɛ**, i, **ɔ**, u/. Katika herufi za kawaida irabu /**a**/ huandikwa **ɑ**, /**ɛ**/ huandikwa **e**, na /**ɔ**/ huandikwa **o.**

**b) Konsonanti**

Konsonanti ni aina ya sauti ambazo wakati wa kuzitamka huwa kuna mzuio wa mkondohewa unaotoka mapafuni. Mkondohewa huo huzuiwa ama kwenye chemba ya kinywa au chemba ya pua. Uzuiaji wa mkondo huo unaweza kuwa wa namna tofauti. Kwa mfano, kuzuiwa kisha huachiwa ghafla, kama tunavyotamka sauti za vipasuo kama **/p/, /t/,** n.k. Lugha ya Kiswahili ina konsonanti 23. Tutaziona katika jedwali la alfabeti za kifonetiki.

**c) Viyeyusho**

Fonimu hizi pia huitwa nusu irabu. Ni fonimu ambazo namna ya utamkaji wake hukaribiana na ule wa irabu, ingawa katika jedwali la alfabeti za kifonetiki za kimataifa huoneshwa kama konsonanti. Viyeyusho ni sauti ambazo wakati wa utamkaji wake huwa kuna mzuio mdogo wa mkondohewa. Tofauti na irabu ni kwamba katika uundaji wa maneno viyeyusho hukosa sifa ya usilabi ambayo irabu huwa na sifa hizo. Katika lugha ya Kiswahili fonimu za viyeyusho 2, ambazo ni:

(i) **/w/**
(ii) **/j/** tamka **/y/**

## Uainishaji wa Fonimu za Lugha ya Kiswahili


Uainishaji wa fonimu huweza kufasiliwa kama kuziweka sauti za lugha mahususi katika aina au makundi mbali mbali.

**a) Uainishaji wa Fonimu Irabu za Kiswahili**

Habwe na Karanja (2004) wanazigawa fonimu irabu za lugha ya Kiswahili kwa kutumia vigezo vitatu: *Sehemu ya ulimi, mwinuko wa ulimi, na umbo la midomo*.


**(i) Kigezo cha Sehemu ya Ulimi**

Kwa kigezo cha sehemu ya ulimi tunazo irabu ambazo hutamkiwa ulimi ukiwa umeelekea sehemu ya mbele kama kwa irabu /**a**/**,** /**ɛ**/**,** na /**i**/, na irabu zinazotamkiwa ulimi ukiwa umeelekea nyuma ambazo ni /**ɔ**/ na /**u**/





**(ii) Kigezo cha Mwinuko wa Ulimi**

Kwa kigezo cha mwinuko wa ulimi tunazo irabu ambazo hutamkiwa ulimi ukiwa umeinuliwa juu sambamba na paa la kinywa kama kwa irabu /**i**/ na /**u**/, irabu zinazotamkiwa ulimi ukiwa kati kama kwa irabu /**ɛ**/ na /**ɔ**/**,** na irabu inayotamkwa ulimi ukiwa umelala chini sambamba na sakafu ya kinywa kama kwa irabu /**a**/.




**(iii) Kigezo cha Umbo la Midomo**

Wakati wa kutamka irabu za Kiswahili, ulimi huwa katika umbo la namna mbili; mviringo au tandazo. Ulimi huwa umeviringwa tunapotamka irabu /**ɔ**/ na /**u**/**,** na unakuwa umetandazwa tunapotamka irabu /**a**/, /**ɛ**/ na /**i**/**.** Katika kielelezo cha ulimi, irabu zote za nyuma hujulikana kama irabu viringo au viringe, na irabu za mbele hujulikana kama irabu tandazo au si viringo.




**b) Uainishaji wa Fonimu Konsonanti za Kiswahili**
Wanaisimu kama Matinde (2012), wanaanisha konsonanti kwa kutumia vigezo vifuatavyo: *Mahali pa matamshi, namna ya utamkaji, mkondohewa, na hali ya glota.*

**i) Kigezo cha Mahali pa Matamshi**
Kwa kigezo cha mahali pa matamshi, konsonanti za Kiswahili huweza kuainishwa kama ifuatavyo:

- **Fonimu za midomo:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa kwa kukutanisha mdomo wa juu na wa chini. Kwa mfano, konsonanti **/b/, /p/, /m/, /w/.**
- Fonimu za midomo-meno: Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa kwa kukutanisha mdomo wa chini na meno ya juu. Kwa mfano, konsonanti **/v/, /f/.**
- **Fonimu za meno:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa wakati ulimi unapokuwa katikati ya meno ya juu na ya chini. Kwa mfano, konsonanti **/ θ / = th, /ð/ = dh**.
- **Fonimu za ufizi:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa wakati ncha ya ulimi inapigusa ufizi kama fonimu /t/, /d/; ncha ya ulimi inapoukaribia ufizi kama tunapotamka konsonanti **/s/, /z/** au ulimi unapopigapiga kwenye ufizi kama tunapotamka fonimu /**r**/.
- **Fonimu za kaakaa-gumu:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa wakati ulimi unapogusa kaakaa gumu kama tunapotamka fonimu **/ʧ/ = ch na /ɟ/ = j**; au ulimi unapokaribia kwenye kaakaa gumu kama katika fonimu / ʃ/= **sh**, **/ɲ/ = ny**
- **Fonimu za kaakaa-laini:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa wakati bapa au sehemu ya kati ya ulimi inapokaribia kwenye kaakaa gumu kama katika fonimu **/ŋ/ = ng'.**

- **Fonimu za glota:** Hizi ni konsonanti ambazo hutamkwa kwa kuhusisha koromeo wakati huo shina la ulimi linapokuwa limerudishwa nyuma. Katika Kiswahili tuna fonimu moja tu ya glota ambayo ni /**h**/.

**ii) Kigezo cha Namna ya Utamkaji**

Kigezo cha namna ya utamkaji huzingatia namna mkondohewa utokayo mapafuni kwenda nje ya mapafu inavyozuiwa kwa namna mbali mbali wakati wa kutamka konsonanti. Mkondohewa huo huzuiwa ama kwenye chemba ya kinywa au chemba ya pua kwenda. Uzuiaji wa mkondohewa huo unaweza kuwa wa namna tofauti: Kwa mfano;

- Kuzuiwa kisha huachiwa ghafla, kama tunavyotamka sauti za vipasuo kama /**p/, /t**/.
- Kuzuiwa na kisha kuachiwa taratibu kama tunavyotamka sauti za vuzuiwa-kwamizi **/ʧ/ = /ch/ na /ɟ/ = j.**
- Kuzuiwa wakati ulimi unapokuwa kwenye meno **/θ/ = th na /ð/ = /dh/**.
- Kubana kiasi kisha kuruhusiwa upite katika nafasi nyembamba kama tunavyotamka sauti **[f]** na **[v]**.
- Kubanwa lakini ukiwa unaruhusiwa upite pembeni mwa ulimi kama tunavyotamka sauti **[l]**.
- Kuzuiwa ncha ya ulimi inapopigapiga ufizi na kusababisha mkondohewa huo upite chini ya ulimi kwa mbele kama tunavyotamka sauti **[r].**
- Kuzuiwa usipite kinywani na kuiruhusiwa upitie puani kama tunavyotamka sauti za nazali (ving'ong'o) **[m]**, **[n]**, **[ɲ] = /ny/** na **[ŋ] = ng'**.

**iii) Kigezo cha mkondohewa**

Wakati wa kutamka konsonanti za Kiswahili hewa itokayo mapafuni huweza kupita katika njia mbili; ama kwenye *chemba ya kinywa* au *chemba ya pua*. Mkondohewa unapita kwenye chemba ya pua huwa tunatamka konsonanti ambazo ni nazali au ving'ong'o tu; ambazo ni **/m/,** /**n**/, /**ɲ**/ na /**ŋ**/. Mkondohewa unapita kwenye chemba ya kinywa huwa tunatamka konsonanti nyinginezo.

**iv) Kigezo cha hali ya glota**

Wakati wa kutamka konsonanti za Kiswahili huwa kuna ya na namna mbili: **(i) Hali ya mtetemo/ mrindimo** au **(ii) kutokuwepo kwa mtetemo**. Kama wakati wa kutamka konsonanti kutakuwa na hali ya mtetemo basi tutatambua konsonanti hiyo ni **ghuna**. La, kama wakati wa kuzitamka hakutakuwa na hali ya mrindimo, basi

konsonanti hizo zitajulikana kama **si ghuna**. Katika jedwali 1, konsonanti ghuna zimejitokeza upande wa kulia (zimewekewa alama ya kujumlisha (+)) na konsonanti ambazo si ghuna ziko upande wa kushoto (zimewekewa alama ya kutoa (-)).

**Jedwali 6**: Fonimu Konsonanti za Kifonetiki za Kiswahili

| **Namna ya matamshi** | **Mahali pa matamshi** | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Midomo (4)** - + | **Midomo -meno (2)** - + | **Meno (2)** - + | **Ufizi (7)** - + | **Kaakaa-gumu (5)** - + | **Kaakaa-laini (4)** - + | **Koromeo/ Glota (1)** - + |
| **Vipasuo (6)** | p b | | | t d | | k g | |
| **Vipasuo-kwamizi (2)** | | | | | č/ ʧ ɟ<br>= ch = j | | |
| **Vikwamizi (9)** | | f v | θ ð<br>= th =dh | s z | ʃ<br>= sh | x ɣ<br>= kh = gh | h |
| **Nazali (4)** | m | | | n | ɲ<br>= ny | ŋ<br>= ng' | |
| **Vitambaza (1)** | | | | l | | | |
| **Vimadende (1)** | | | | r | | | |
| **Viyeyusho (2)** | w | | | | j<br>= y | | |

**Chanzo:** Imehaririwa kutoka Massamba na wenzake (2004)

Mpendwa mwanafunzi, lugha ya Kiswahili sanifu ina jumla ya fonimu 30 zinazotumika katika maandishi na matamshi: fonimu irabu 5, fonimu konsonanti 23, na fonimu viyeyusho 2. Fonimu **/x/** = *kh*, si konsonanti ya Kiswahili sanifu, licha ya kwamba baadhi ya lahaja za Kiswahili (husussani Kipemba na Kiunguja) huitumia.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Unazitofautishaje dhana za fonetiki na fonolojia ya Kiswahili?
2. Unaweza kuziainisha vipi fonimu za lugha ya Kiswahili?

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Eleza maana ya fonetiki.
2. Tofautisha matawi manne ya fonetiki.
3. Kwa kutumia mifano, faida ya kuwa na shirika la Alfabeti za Kimataifa.
4. Eleza uainishaji wa fonimu unavyojitokeza katika lugha ya Kiswahili.
5. Eleza maana ya dhana zifuatazo:
    a. Kiimbo,
    b. Kidatu,
    c. Lafudhi,
    d. Mkazo, na
    e. Toni.
6. Eleza sifa za foni [ɔ], [k], [l], [m], [a], [ð], [ŋ], [ɦ], na [ɛ]
7. Onesha mkazo katika maneno yafuatayo ya Kiswahili:
    a. Anakimbia,
    b. Oa,
    c. Nyufa, na
    d. Tambaa.

# Somo la Tano

## Kuchambua Mofolojia ya Lugha ya Kiswahili

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita, tulieleza jinsi ya kutumia fonolojia ya lugha ya Kiswahili. Katika somo hilo tulijifunza kuwa fonolojia ni taaluma ya isimu inayochambua sauti za lugha mahususi. Vilevile, tuliona kuwa lugha ya Kiswahili inazo fonimu za aina kuu tatu: irabu, konsonanti, na viyeyusho. Aidha, tulieleza vigezo vinavyotumika kuainisha fonimu za lugha ya Kiswahili. Katika somo hili **tunachambua kwa kina kuhusu mofolojia ya lugha ya Kiswahili.** Ili kukamilisha somo hili **tutafafanua dhana ya mofolojia** ikifuatiwa na **kufafanua dhana za msingi katika mofolojia.** Pia, somo **litachambua aina za maneno katika lugha,** na **kufafanua mbinu za uunadaji maneno.** Mwisho, **tutafafanua dhana ya mofofonolojia.** Mpendwa mwanafunzi, karibu katika somo hii ili uweze kujifunza mambo mbalimbali yanahusiana na mofolojia ya lugha Kiswahili sanifu.

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana ya mofolojia ya Kiswahili;
- Kufafanua dhana za msingi katika mofolojia (mofu, mofimu, alomofu, n.k.);
- Kuchambua aina za maneno;
- Kufafanua mbinu za uundaji maneno, na
- Kufafanua dhana ya mofofonolojia.

## Dhana ya Mofolojia ya Kiswahili

**a) Maana ya Mofolojia**

Mofolojia ni neno la Kigiriki lililitokana na maneno mawili ***"mofo"*** ikiwa na maana ya ***"umbo"*** na ***"ology"*** ikiwa na maana ya ***"sayansi ya"***. Kwa maana hiyo mofolojia ni ***sayansi ya uundaji maneno***.

Kwa mujibu wa Massamba (2004), mofolojia kuwa ni taaluma ya isimu inayoshughulikia uchambuzi na uchanganuzi wa kanuni na mifumo inayohusu upangaji wa mofimu mbalimbali ili kuunda maneno ya lugha. Habwe na Karanja (2004) wanasema, mofolojia hujihusisha na uchambuzi wa muundo wa ndani wa neno. Aidha, Rubanza (1996) anasema, mofolojia ni taaluma inayoshughulikia vipashio vya lugha na mpangilio wake katika uundaji wa maneno.

Kwa ujumla, mofolojia ni tawi la isimu linalochunguza na kuchambua maumbo ya maneno pamoja na kanuni za uundaji maneno ya aina mbalimbali kama vile vitenzi, nomino, vielezi, vivumishi n.k.

**b) Matawi ya Mofolojia**

Wanaisimu wanaigawa taaluma ya mofolojia katika matawi makuu mawili:

i) Mofolojia ya mnyambuliko wa maneno

ii) Mofolojia ya uundaji wa maneno.

**i) Mofolojia ya Mnyambuliko wa Maneno**

Mofolojia ya minyambuliko wa maneno (Inflectional Morphology) hushughulikia minyambuliko ambayo huwekwa kwenye mizizi ya maneno kuwakilisha maana mbalimbali lakini minyambuliko hiyo isibadili aina wala maana ya neno hilo. Aidha, kila lugha ina utaratibu wake wa kunyambua maneno katika lugha hiyo. Katika lugha ya Kiswahili, mizizi ya nomino inaweza kuwekwa viambishi awali kuonyesha dhana mbalimbali. Mfano, mzizi {-to}

| | |
|---|---|
| i) Umoja wa nomino: | m-to |
| ii) Wingi wa nomino: | mi-to |
| iii) Ukubwa wa nomino: | ji-to |
| iv) Udogo wa nomino: | ki-ji-to |

Mpendwa mwanafunzi, jaribu kunyambulisha mzizi wa kitenzi "-chez-" ili kupata maneno mengine ambayo ni vitenzi? Bila shaka umepata vitenzi vingine kama vile: ***chezwa,-chezewa, -chezeana, -chezeka, -chezesha,*** n.k.

**ii) Mofolojia ya Uundaji wa Maneno**

Hartman (1972) anaeleza ya kuwa mofolojia ya uundaji wa maneno (Derivational Morphology) ni eneo ambalo hushughulikia mikondo

na matokeo ya kiisimu ya uundaji wa maneno kwa kuweka viambishi katika mizizi ya maneno. Kiambishi kinachowekwa kwenye neno linaloundwa kinaweza kubadili au kisibadili aina na asili ya neno hata kama neno hilo lilikopwa. Mfano, kutokana na mzizi **-lim-** wa kitenzi uliotokana na kitenzi **lima**, tunaweza kuunda maneno yafuatayo:

| | | |
|---|---|---|
| i) u + ku + lim+ a | = | ukulima (N) |
| ii) ki + lim + o | = | kilimo (N) |
| iii) m + ku + lim + a | = | mkulima (N) |
| iv) ku + lim + a | = | kulima (T/ N) |

## Dhana za Msingi katika Mofolojia

**i) Mofu**

Mofu ni kipashio cha kimofolojia kinachowakilisha mofimu. Kwa fasili rahisi tunaweza kusema kuwa mofu ni umbo la kimofolojia linalowakilisha mofimu.

Lugha ya Kiswahili kama ilivyo lugha mbalimbali duniani ina maneno ya aina tofauti. Maneno ya lugha ya Kiswahili yameundwa kwa mofu mbalimbali. Mofu hizo zinaweza kuwekwa katika makundi matatu: *mofu tangulizi*, *mofu mzizi* na *mofu fuatishi*. **Mofu tangulizi** ni umbo la neno ambalo hujitokeza kabla ya mzizi, na **mofu fuatishi** ni umbo la neno linalojitokeza baada ya mzizi wa neno. Kuna baadhi ya maneno huwa na mofu tangulizi, mzizi na mofu fuatishi, kama katika neno: a-na-**lim**-a. Lakini maneno mengine huwa na mofu mzizi na mofu fuatishi peke kama katika neno: **uz-a**. Vipo vigezo viwili vinavyotumika kuainisha mofu; kigezo cha kimaana na kigezo cha kimuundo.

**Aina za Mofu kwa Kigezo cha Maana**

**a) Mofu Huru**

Hizi ni aina za mofu ambayo haiweza kusimama peke yake kama umbo huru (linalojitegemea). Kwa mfano, Arusha, maji, safi n.k.

**b) Mofu Tegemezi**

Ni aina ya mofu ambayo haiwezi kuwa peke yake na ikaleta maana. Mofu hii pia hujulikana kama mofu funge. Mfano;

A- ta- lim- a

1 2 3 4

**c) Mofu Tata**

Ni aina ya mofu ambayo hudokeza maana zaidi ya moja na hivyo kusababisha utata. Mfano; *A- li- m- pig-* ***i****- a mpira*

Utata unasababishwa na mofu -i-

- Alimpiga kaka kwa sababu ya mpira. *(Sababu)*
- Alimpiga kaka kwa mpira. *(Kifaa)*
- Alimpasia kaka mpira. *(Uelekeo)*
- Alipiga mpira badala yake. *(Kwa niaba)*

**Aina za Mofu kwa Kigezo cha Muundo**

**a) Mofu Changamano**

Ni aina ya mofu ambayo huundwa kwa maneno mawili ambapo kila moja huwa na maana inayojitegemea. Kwa mfano;

Mwanaanga ⟷ Mw+ ana + anga

Mbwamwitu ⟷ Mbwa + mwitu

**b) Mofu Kapa**

Ni aina ya mofu ambayo haiwakilishwi na alama au kitu chochote kilicho dhahiri. Huwa hayana maumbo dhahiri ya umoja au wingi kama katika neno;

| **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|
| U-kuta | Ø-kuta |
| Ø-tunda | ma-tunda |

**ii) Mofimu**

Mofimu ni kipashio kidogo kabisa katika lugha chenye kuwakilisha maana ya kisarufi au kileksika. Kipashio hiki hakiwezi kuvunjwavunjwa zaidi bila kupoteza maana. Mofimu huweza kujitokeza kama mzizi wa neno au kiambishi kimoja au zaidi, na hutenganishwa kwa alama ya kistari (-). Kiambishi ni mofimu inayopachikwa kabla, baada, au katikati ya mzizi wa neno. *(Lugha*

*ya Kiswahili haina viambishi kati).* Mzizi ni mofimu ya msingi katika neno. Kwa mfano; kutokana na mzizi wa neno "-chez- tunaweza kupata maneno**:** *m-**chez**-a-ji, m-**chez**-o, ku-**chez**-a, **chez**-ew-a, a-na-m-**chez**-esh-a, n.k.*

**Aina za Mofimu**

Kuna aina mbili za mofimu; mofimu huru na mofimu tegemezi.

**a) Mofimu Huru**

Ni aina ya mofimu ambayo huweza kusimama pekee na kujitosheleza kimaana yaani huwa na sifa ya neno. Mara nyingi mofimu huru huhusisha aina za maneno kama nomino, vivumishi au vielezi ambayo hayawezi kugawanyika zaidi na kubeba maana kisarufi. Mfano;

- Nomino: baba, dada, mama, kaka, shangazi n.k.
- Vivumishi: safi, chafu
- Vielezi: polepole, haraka

**b) Mofimu Tegemezi**

Ni aina ya mofimu ambayo huweza kuvunjwavunjwa na kubeba maana kisarufi, mofimu tegemezi hutegemeana ili kuleta maana kamili ya neno. Mfano; neno **anacheka** limeundwa na mofimu zifuatazo:- [a-na-chek-a] ambapo kila moja huwa na dhima kisarufi

A- mofimu ya nafsi (ya tatu umoja) mtenda

-na- mofimu ya njeo ya wakati uliopo

-chek- mofimu mzizi

-a mofimu tamati

**iii) Alomofu**

Ni maumbo mawili au zaidi yanayowakilisha mofimu moja. Yaani, maumbo tofauti yenye kubeba dhana au maana moja. Katika lugha ya Kiswahili, alomofu huweza kujitokeza kama ifuatavyo:

**a) Alomofu za Mofimu ya Umoja**

*Mw-alimu, m-toto, mu-uguzi, ki-ti, Ø-ua, u-fa*

Maumbo **mw-, m-, mu-, ki-, Ø** na **u**, ni alomofu zinazowakilisha dhana ya umoja.

**b) Alomofu za Mofimu ya Wingi**

*Wa-limu, wa-toto, vi-ti, ma-ua, Ø-kuta, ny-ufa.*

Maumbo **wa, vi, ma, Ø** na **ny,** ni alomofu za mofimu ya wingi. Yanapotumika kwenye sentensi mtu hubaini vinaongelewa vitu zaidi ya kimoja.

**c) Alomofu za Mofimu ya Utendewa**

Haya ni maumbo tofauti yanayowakilisha mofimu za utendewa, yaani mofimu zinazonufaika na vitendo. Mfano,

| **Kitenzi** | **Mofimu tendewa** |
|---|---|
| Soma | som**-ew-**a |
| Lima | lim-**iw**-a |
| Liwa | li**-liw-**a |
| Lea | le**-lew-**a |

Katika vitenzi, pia tunaweza kupata alomofu za utendea -i-, -e-, utendeka -ik-, -ek-, utendesha (usababishi) -ish-, -esh-, -z-, -iz-, -ez-, fy-, -s-

**d) Alomofu za Mofimu Njeo**

Alomofu za njeo ni maumbo tofauti yanayobainisha nyakati tofauti katika vitenzi. Kwa mfano, *a-**li**-pik-a**,** a-**ta**-pik-a**,** na a-**na**-pik-a.*

Maumbo **-li-, -ta-,** na **-ta-** ni alomofu zinazowakilisha maana ingawa maumbo hayo yametofautiana kimuonekano.

**e) Alomofu za Ukanushi katika Njeo**

Mfano;

| **Uyakinishi** | **Ukanushi** |
|---|---|
| A-**li**-pik-a | ha-**ku**-pik-a |
| A-**ta**-pik-a | ha-**ta**-pik-a |
| A-**na**-pik-a | ha-pik-**i** |

**f) Alomofu za Nafsi**

Kuna maumbo tofauti yanayobainisha nafsi. Maumbo hayo ya nafsi huambatanishwa kwenye vitenzi. Maumbo hayo ni kama yanavyooneshwa katika mifano hapa chini:

| **Nafsi** | **Umoja** | **Wingi** |
|---|---|---|
| Kwanza | (mimi) **Ni**-na-pik-a | (sisi) **Tu**-na-pik-a |
| Pili | (wewe) **U**-na-pik-a | (ninyi) **M**-na-pik-a |
| Tatu | (yeye) **A**-na-pik-a | (wao) **Wa**-na-pik-a |

**g) Alomofu za Hali**

Dhana ya hali kimofolojia huhusishwa na vitenzi. Vitenzi huweza kubainisha hali zifuatazo

**Hali ya kuendelea** (kitendo kinaendelea): Mfano; ***Ana**soma, **ana**lima, n.k.*

**Hali timilifu** (kitendo kimekamilika): Mfano; ***ame**soma, **ame**lima*

**Hali ya mazoea (desturi):** Mfano; ***hu**soma, **hu**lima, n.k.*

**Hali ya masharti:** Mfano; ***ange**soma **ange**faulu mtihani, **angeli**lima **angeli**...*

***angali**kuja **angali**...*

Katika mifano hivyo, maumbo: **-na-, -me-, hu-, -nge-** na **-ngeli-,** na **-ngali-** kwa pamoja huwakilisha hali mbalimbali katika vitenzi. Hivyo, hujulikana kama alomofu za hali. Yaani, maumbo tofauti yanayowakilisha hali.

**iv) Shina**

Kwa mujibu wa Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI, 2013: 505), shina ni sehemu ya neno yenye mzizi na viambishi (awali au tamati). Mfano;

(a) m+ toto (b) jeng+ a

$Kba_{ngeli\ 1}$ + Mz Mz + Kbt

**v) Mzizi**

Hili ni umbo la msingi la neno ambalo hubaki baada ya kuondoa viambishi awali na tamati. Mara nyingi mzizi haubadilikibadiliki. Kama mabadiliko ya mzizi yatajitokeza, basi mabadiliko hayo husababishwa na maathiriano ya kifonolojia. Mfano, **jeng**-a kuwa m-**jenz**-i. Hivyo, ***mzizi ni kipashio cha msingi katika neno*.** Mzizi

wa neno huweza kujitokeza mwanzoni mwa neno au baada ya kiambishi au viambishi kutegemeana na mfumo wa lugha. Kwa mfano katika lugha ya Kiswahili;

**Mzizi baada ya kiambishi awali** **Mzizi mwanzoni mwa neno**

(a) m+ **toto** (b) **jeng**+ a

Kba$_{\text{ngeli 1}}$ + Mz Mz + Kbt

Kuna aina mbili za mizizi; ***mizizi huru*** na ***mizizi tegemezi***

**a) Mizizi huru**

Hii ni mizizi ambayo husimama peke yake kama neno huru. Mizizi huru huwa ni neno kamili linalojitegemea. Baadhi ya mizizi hiyo

**Vitenzi vya mkopo:** shukuru, fikiri

**Nomino:** mama, Juma, Tanzania, gari, gauni, tunda n.k

**Vivumishi:** safi, chafu,

**Vielezi:** polepole

**b) Mizizi tegemezi**

Hizi ni mofu ambazo haziwezi kusimama peke yake. Badala yake mofu hizi hutegemeana ili ziweze kuunda neno kamili. Mizizi tegemezi huwa na maumbo tofauti.

- Mizizi yenye umbo la **fonimu moja** au **herufi**: Kwa mfano katika vitenzi jina: *ku-**l**-a, ku-**f**-a, ku-**p**-a, ku-**j**-a*.
- Mizizi ya **silabi moja**: Mfano; *m-**tu**, wa-**tu**; m- **to**, mi- **to***
- Mizizi ya **fonimu zaidi ya mbili**: Mfano; ***kimbi**-a, n.k.*
- Mizizi ya **changamano**: Ni mizizi inayotokana na mwambatano wa maneno mawili. Mfano;

Batamaji ← bata + maji

Mwanahewa ← -ana + hewa

**Sifa za Mzizi**

Mzizi wa neno huwa na sifa mbalimbali:

*Kwanza, mzizi ni mofu muhimu zaidi kuliko mofu zingine zote katika neno.* Sifa hii inadhihirika kwa kuzingatia ya kuwa mzizi wa neno huwa kama mhimili wa neno.

*Pili, mzizi pia una uwezo wa kukaa peke yake kama neno kamili kwa mfano maneno huru.*

*Tatu, mizizi kadhaa inaweza kuwekwa pamoja kuunda mzizi changamano.* Katika lugha ya Kiswahili kwa mfano, yapo maneno ambayo yameundwa kwa kutumia mizizi miwili au zaidi. Kwa mfano: Mwanahewa lina mizizi miwili: -ana + hewa; Amiri jeshi nalo lina mizizi miwili. Amiri + jeshi.

*Nne, mzizi haubadilikibadiliki, kwa maana ya kuwa umbo la mzizi ni moja tu na haliongezeki wala kupungua.* Kwa mfano, *-imb- ana**imb**a, ata**imb**a, haku**imb**a, uli**imb**a; -chez- si**chez**i, ha**chez**i, ali**chez**a; kamat- nilim**kamat**a, usim**kamat**e, wali**kamat**ana, tu**kamat**ie, n.k.*

### vi) Viambishi

Hivi ni vipande vya maneno ambavyo hupachikwa kabla, kati na baada ya mzizi wa neno. Lugha ya Kiswahili inatumia viambishi vinavyojitokeza kabla na baada ya mzizi. Kwa mfano,

| **Kabla ya Mzizi** | | **Mzizi** | **Baada ya mzizi** |
|---|---|---|---|
| a- | na- | lim- | a |
| Nafsi 3Umoja | NjeoUliopo | T | Kiambishi Tamati |

### vii) Neno

Kwa mujibu wa Lyons (1968:194), ili kupata fasili ya neno lazima lifasiliwe kifonolojia, kimofolojia, kisintaksia, kisemantiki na kiotografia. Hata hivyo, kwa kuwa tunazungumzaia tungo, basi tutazingatia kigezo cha kimofolojia tu.

**Kimofolojia,** neno ni mpangilio wa mofu wenye maana kisarufi na kileksika. Ni umbo linaloundwa na mofu mbalimbali zinazotambulika kama viambishi na mizizi huru na tegemezi. Kutokana na mtazamo huu tunapata: *Neno sahili/ huru:* **dada, tunda, n.k.;** neno *changamano* ambalo huundwa na mofu zaidi ya moja. Mfano; **a-na-ku-l-a;** na neno *ambatano* ambalo huundwa na

mofu huru zaidi ya moja na ambazo huambatanishwa pamoja, Mfano; Bata+mzinga = batamzinga**.**

## Kuchambua Aina za Maneno

Wanaisimu hutofautiana katika kubainisha idadi ya aina za maneno katika lugha hiyo. Kwa mfano, Massamba na wenzake (1999) wanabainisha aina **saba**, Habwe na Karanja (2004) wanabainisha aina **nane** za maneno: ***nomino, vitenzi, vivumishi, viwakilishi, vielezi, vihusishi, viunganishi, na vihisishi*.** Hata hivyo, tutatumia *vigezo vitatu* kupanga aina hizo za maneno: *kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia*.

### a) Aina za Maneno Kisemantiki

Kisemantiki, maneno ya lugha ya Kiswahili huainishwa kwa kutumia kigezo cha **maana** inayobebwa na neno hilo katika sentensi.

#### *i) Nomino (N)*

Ni aina za maneno ambazo hurejelea majina ya watu, vitu, wanyama, mahali, vyeo, hali, dhana, au vitendo.

**Aina za Nomino**

***Nomino za pekee:*** Hutaja majina ya watu au vitu mahususi kama vile majina ya *miji, nchi, mito, maziwa, bahari, bara, vyeo, milima, siku, miezi, vijiji*. Nomino za pekee huanza na herufi kubwa mahali popote katika sentensi. Mfano,

***<u>Tanzania</u>*** *ni nchi nzuri.*

***N***

***Nomino za dhahania:*** Hurejelea majina ya vitu vya kufikirika ambavyo hatuwezi kuviona au kuvishika. Kwa mfano, *upepo, ubaya, uzuri, wema* n.k.

***<u>Upepo</u>*** *unavuma kwa kasi.*

***N***

***Nomino za kawaida:*** Hutaja majina ya kawaida. Majina haya yanapoandikwa kwenye sentensi huanza na herufi kubwa. Lakini, yanapotokea mahali kwingineko huanza na herufi ndogo.

***Nomino zinazohesabika:*** dada, kaka, wanyama, mawe, shangazi, mtoto.

***Nomino za wingi:*** hutaja majina ya vitu visivyohesabika kama mchanga, maji, nywele, n.k.

***Nomino za makundi:*** hutaja majina yaliyo katika makundi. Kama vile, *darasa, jeshi, jamii,bunge, kamati, n.k. Mfano,*

*__**Bunge**__ hutunga na kupitisha sheria.*

***N***

***Nomino za kitenzi-jina:*** Ni majina yanayotokana na vitenzi. Majina kama vile *kulima, kucheza, kuimba, kupika* n.k. Mfano,

*__**Kulima**__ kunachosha.*

***N***

***ii) Vitenzi (T/Ts/t)***

Ni aina za maneno ambazo hutoa taarifa juu ya jambo linalofanywa na viumbe mbalimbali kama vile mtu, mnyama n.k.

**Aina za Vitenzi**

***Vitenzi vikuu (T):*** Ni kitenzi kinachotoa taarifa kamili. Mfano,

*Mtoto __**anacheza**__*

***T***

***Vitenzi visaidizi (Ts):*** Ni kitenzi kinachosaidiana na kitenzi kikuu kukamilisha taarifa. Mfano,

*Mtoto __**alikuwa**__ anachezea maji.*

***Ts*** ***T***

***Vitenzi vishirikishi (t):*** Ni kitenzi kinachohusisha nomino na kivumishi au kiwakilishi na kivumishi. Mfano,

*Kiki __**ni**__ mtukutu*

***N*** ***t*** ***V***

***iii) Vivumishi (V)***

Ni maneno ambayo hutoa taarifa zaidi kuhusu nomino au kiwakilishi chake kwa kuzingatia sifa, idadi, umiliki.

**Aina za Vivumishi**

***Vivumishi vya sifa:*** Huelezea sifa za nomino jinsi ilivyo. Kuna aina mbalimbali za vivumishi. Vipo vivumishi vya sifa, idadi, kuonesha, kuuliza, kumiliki, -ote, -o-ote, -ingine. Mfano,

*Tatu ni mtoto* ***msafi***

***V***

*Aziza ni msichana* ***mrembo***

***V***

***Vivumishi vya kumiliki:*** hubainisha nomino inayomilikiwa. Mfano,

*Nguo* ***zangu*** *zimechanika*

***V***

***Vivumishi vya kuulizi:*** *Mgeni* ***gani*** *aliyefika?*

***V***

***Vivumishi vya -enye- -enyewe:*** Mfano,

*Mgeni* ***mwenyewe*** *amelala*

***V***

***Vivumishi vya pekee:*** Hurejelea sehemu ya, baadhi ya, kati ya, au zaidi ya vitu vingi vyenye sifa zinazolingana. Vivumishi hivi ni kama *-o-ote* (chochote, kokote, zozote, popote n.k.), -ote (zote, chote, vyote, n.k.), *-ingine* (nyingine, mwingine, zingine, jingine). Mfano,

*Mnunulie viatu* ***vyote.***

***V***

*Watu* ***wengine*** *wana busara*

***V***

*Viazi* **vyote** vimeoza

***V***

*iv) Viwakilishi (W)*

Ni aina za maneno ambalo husimama badala ya nomino. Kuna aina mbalimbali za viwakilishi. Aina hizo ni kama viwakilishi vya nafsi (huru na viambata), kumiliki, kuuliza,

**Aina za Viwakilishi**

***Viwakilishi vya nafsi:***

***Viwakilishi nafsi huru:*** Mimi, sisi, wewe, ninyi, yeye, wao. Mfano,

***Mimi*** *nitakuja*

***W***

***Viwakilishi nafsi viambata:*** Ni vipande vya maneno ambavyo hupachikwa mwanzoni mwa vitenzi, kisha maneno hayo hufanya kazi kama vitenzi. Viambishi hivyo ni kama *ni-, tu-, u-, m-, a-, wa-*. Mfano,

***Ni****takuja. (mimi),* ***Tu****takuja (sisi),*

***U****takuja (wewe),* ***M****takuja (ninyi),*

***A****takuja (yeye),* ***Wa****takuja (wao).*

***Viwakilishi vya kumiliki:*** **-angu** (changu, zangu, yangu n.k), **-etu** (chetu, zetu, yetu n.k), **-enu** (chenu, zenu, yenu, n.k.), -ao (chao, zao, yao, n.k.). Kwa mfano,

***Zangu*** *zimechanika (nguo).*

***W***

***Viwakilishi vya idadi:*** -ote (zote, chote, vyote, n.k.), ki-moja, vi-wili, mi-chache, mengi, tisa, n.k. Mfano,

***Nyingi*** *zimechanika (nguo zaidi ya mbili).*

***W***

***Viwakilishi vya sifa:*** wa-fupi, m-fupi, vi-fupi, m-refu, wa-refu, vi-dogo, wa-dogo n.k. Mfano,

***Mrefu*** *afute ubao (mtu).*

***W***

***Vivumishi vya kuonesha:*** -le (zile, kile, pale, vile, mule). Mfano,

*<u>**Vile**</u> zimechanika (viatu/ vitabu, vikapu, n.k.).*

**W**

***Viwakilishi vya kuulizi:*** -pi (ngapi, vipi, zipi, kipi, n.k.). Mfano,

*<u>**Kipi**</u> kimechanika (kiatu/kitabu/kikapu, n.k.?*

***W***

***Viwakilishi vya pekee:*** *-o-ote* (chochote, kokote, zozote, popote n.k.), -ote (zote, chote, vyote, n.k.), *-ingine* (nyingine, mwingine, zingine, jingine) Mfano,

*Kiliwe <u>**chochote**</u> (chakula).*

***W***

*<u>**Zote**</u> zimechanika (kanga/ nguo/ n.k.).*

***W***

*<u>**Mwingine**</u> aingie. (mgonjwa/ mwanafunzi).*

***W***

***v) Vielezi (E)***

Ni aina za maneno ambayo hueleza jinsi kitendo kilivyofanyika, mahali kilipofanyika, wakati na namna kilivyofanyika.

**Aina za Vielezi**

***Vielezi vya mahali:*** Hueleza mahali kitendo kilipofanyikia au kinapofanyikia. Mfano,

*Mama amekwenda <u>**sokoni.**</u>*

***E***

***Vielezi vya namna:*** Hueleza jinsi kitendo kinavyofanyika au kilivyofanyika. Mfano,

*Dada hufagia uwanja <u>**polepole.**</u>*

***E***

***Vielezi vya idadi*** Hivi hueleza kitendo kimefanyika au hufanyika mara ngapi. Mfano,

*Dada huenda sokoni <u>**mara tatu kwa juma.**</u>*

***E***

***Vielezi vya wakati*** hueleza muda kitendo hufanyika, kilipofanyika au kinapofanyika. Mfano,

*Dada hufagia uwanja **<u>kila asubuhi.</u>***

***E***

***vi) Vihisishi (I)***

Vihisishi ni aina ya maneno ambayo huonesha hisia alizonazo mtu. Mara nyingi maneno haya hutokea mwanzoni mwa sentensi na kufuatiwa na sentensi yenye kuonesha hisia. Mfano,

**Aina za Vihishi** (kwa mujibu wa Matinde (2012: 149-150).

**Vihisishi vya kuitikia:** ***<u>Enhe</u>!*** *Ikawaje?* ***<u>Abee!</u>*** *Umeniita?*

***I*** ***I***

**Vihisishi vya kushukuru:** ***<u>Asante</u>!*** *Umenisaidia sana.*

***I***

**Vihisishi vya furaha:** ***<u>Huree!</u>*** *Nimeshinda.*

***I***

**Vihisishi vya masikitiko:** ***<u>Yalaa!</u>*** *Nimejikata.*

***I***

**Vihisishi vya mshangao:** ***<u>Mtume!</u>*** *Nini kimekupata?*

***I***

**Vihisishi vya kufariji:** ***<u>Poleni!</u>*** *Mmeumia sana?*

***I***

**Vihisishi vya kuapa:** ***<u>Haki ya Mungu!</u>*** *Sijaiba.*

***I***

**Vihisishi vya kukanya au kuonya:**

***<u>Thubutu!</u>*** *Jaribu kunipiga halafu uone.*

***I***

**Vihisishi vya mwigo sauti:** *Alidumbukia* ***<u>chubwi!</u>***

***I***

**b) Aina za Maneno Kimofolojia**

Kimofolojia, maneno ya lugha ya Kiswahili huainishwa kwa kuzingatia **maumbo**. Yaani, jinsi maneno yalivvyoundwa. Uchunguzi uliofanywa na wanaisimu umebaini kuwepo kwa makundi makuu mawili kimofolojia:

(i) Maneno yanayoambishwa

(ii) Maneno yasiyoambishwa

**(i) Maneno Yanayoambishwa**

Maneno yanayoambishwa ni yale ambayo yanaweza kuwekewa viambishi. Mizizi ya maneno haya huweza kuwekewa viambishi mbalimbali mwanzoni (kabla) au mwishoni (baada) mwa mzizi wa neno. Lugha ya Kiswahili ina utajiri wa maneno yanayoweza kuambishwa kuliko yale yasioambishwa. Mfano wa maneno yanayoweza kuambishwa ni:

***Nomino tegemezi:*** Haya ni majina ambayo maumbo yake hayawezi kusimama peke yake kama maneno huru. Badala yake huundwa kwa kiambishi pamoja na mzizi wa neno husika. Mfano,

| Kiambishi | Mzizi | Nomino |
|---|---|---|
| *Ma-* | *ua* | *maua* |
| *Ki-* | *ti* | *kiti* |
| *Vi-* | *ti* | *viti* |
| *Ma-* | *rais* | *Marais* |
| *Ma-* | *waziri* | *Mawaziri* |

***Nomino za changamani:*** Ni nomino ambazo huwa na mchanganyiko wa neno tegemezi na neno huru. Mfano,

*Mwanahewa* ← *Mw-ana + hewa,* n.k.

***Vitenzi tegemezi:*** Ni vitenzi ambavyo havina maumbo yanayojitegemea. Hivyo, maumbo yake hutegemeana ili kuunda neno moja. Mfano,

| **Viambishi awali** | **Mzizi** | **Viambishi tamati** |
|---|---|---|
| A- na- | -kimbi- | -a |
| Wa- li- | -lim- | -a |

***Vivumishi tegemezi:*** Maumbo mengi ya vivumishi ni tegemezi. Hutegemea nomino inayoelezewa ili kujenga upatanisho wa kisarufi. Mfano, kivumishi -zuri huweza kuwa katika kundi la maneno yanayoambishwa au yasiyoambishwa.

*Mtoto m-zuri anasoma*

*Kiatu ki-zuri kimechanika*

Pia, ***Kivumishi****: -baya*. Kikiongezewa viambishi mwanzoni tunapata maneno: ***ki****-baya (V),* ***vi****-baya (V/ E),* ***m****-baya (N),* ***wa****-baya (N),* n.k.

***Viwakilishi tegemezi*** (vinavyopokea viambishi awali + mzizi). Mfano, kivumishi cha kumiliki - changu, chetu, zangu, n.k.

| **Kiambishi** | **Mzizi** | **Kiwakilishi** |
|---|---|---|
| ch-/z- | -angu | changu, zangu, zetu, n.k. |
| z-/vy-/ch- | -etu | zetu, vyetu |

***Vielezi tegemezi:*** Hivi hutokana maneno ya kategoria nyingine kupachika viambishi *kabla* au *baada* ya mzizi wa neno, na vielezi vingine kuambatanishwa maneno zaidi ya moja ambapo kila neno husimama peke yake. Hivyo, tuna vielezi tegemezi vinavyopachikwa *viambishi awali* + *mzizi*, vielezi tegemezi vinavyoanza na *mzizi* + *viambishi tamati* na vielezi tegemezi vya mwambatano wa maneno. Mfano,

**Vielezi tegemezi vinavyopokea viambishi awali**

| **Kiambishi awali** | | **Mzizi** | **Kielezi** |
|---|---|---|---|
| *Ki* | + | *vivu* → | ***ki****vivu* |
| | | ***V*** | |

**Vielezi tegemezi vinavyopokea viambishi tamati**

| **Mzizi** | | **Kiambishi Tamati** | **Kielezi** |
|---|---|---|---|
| *Soko* | + | *ni* | *sokoni* → |
| ***N*** | | | |

**Vielezi tegemezi vya mwambatano wa maneno**

Mwalimu huingia darasani <u>mara tatu kwa juma.</u>

**1 2 3 4**

***Vihusishi tegemezi:*** Vihusishi hutumia maneno yenye muundo wa -a uanganifu (ya, za, cha, na, kwa, chini ya, kando ya, mbele ya, ndani ya, baada ya, kabla ya, n.k. Mfano,

| **Kiambishi** | **Mzizi** | **Kihusishi** |
|---|---|---|
| kw-/ z-/ w-/ vy- | -a | kwa, za, wa, vya, |

**Mfano:** *Alikwenda <u>kwa</u> miguu*

**(ii) Maneno Yasiyoambishwa**

Maneno yasiyoambishwa huweza kuelezwa kama maneno yenye **maumbo huru**. Baadhi ya lugha huwa na maneno yasiyoambishwa ambayo ni mengi zaidi kuliko yale yanayoambishwa. Lakini, lugha nyingine zina maneno mengi yanayoambishwa kuliko yale yasiyoambishwa ***(Rejelea jamii za lugha kwa kigezo cha kimuundo).*** Maneno yasiyoweza kuambishwa ni kama:

***Nomino huru:*** Ni majina ambayo hayapokei viambishi. Mfano, *Tanzania, Rais, Waziri Mkuu, Juma, dada, mama, shangazi, Kilimanjaro, Kondoa, Rufiji, ua, Afrika, ufa, n.k.*

***Nomino mwambatano:*** Haya ni majina ambayo yametokana na kuunganishwa maneno huru mawili. Mfano,

*Askarikanzu* ← *Askari + kanzu,* n.k.

***Vitenzi huru:*** Ni kitenzi ambacho hakipokei viambishi. Mfano, kitenzi shirikishi *si, ni*.

***Vivumishi huru:*** Kama *baya, zuri, bora, safi*, n.k. Mfano,

*Ua zuri linanukia*.

***Viwakilishi huru:*** Hivi ni viwakilishi ambavyo havipokei viambishi. Mfano wa viambishi hivi ni *viwakilishi nafsi huru* kama vile *mimi, sisi, wewe, ninyi, yeye, wao*.

***Vielezi huru:*** Vielezi hivi huundwa kwa kurudiarudia neno huru moja. Mfano,

Pole + pole = polepole

Haraka + haraka = harakaharaka

***Viunganishi huru:*** *na, ila, pia, lakini, hivyo, ijapokuwa, ingawa, japo,* n.k.

***Viunganishi vya maneno mawili au zaidi:*** *Kwa sababu, kwa hiyo, kwa hivyo.*

***Vihusishi huru:*** *na.*

***Vihusishi vya neno zaidi ya moja:*** Vihusishi hivi hutokana na kategoria nyingine za maneno hususani vielezi: Mfano, *mbele ya*, *nyuma ya*, *kando ya*, *ndani ya*.

***Vihisishi***: Vihisishi vingi vya Kiswahili vina maumbo yaliyotokana na nomino. Kinachotofautisha maneno haya na nomino ni matumizi ya alama ya mashangao (!) baada ya kuliandika neno hilo. Mfano, Asante! Umenisaidia sana.

**I**

### c) Aina za Maneno Kisintaksia

Uainishaji wa maneno kisintaksia, huzingatia *dhima* au *kazi* inayofanywa na neno fulani katika sentensi. Tuangalie dhima hizo kwa kuhusisha na aina nane za maneno.

#### i) Nomino Kisintaksia

**Kiima cha sentensi.** Nomino hujitokeza mwanzoni mwa sentensi na hivyo kufanya kazi kama **kiima** cha sentensi, yaani kubeba dhima ya mtenda wa jambo. Mfano,

***Mti*** *umeanguka*/

**K**

**Yambwa.** Nomino hufanya kazi kama **yambwa**. Yambwa ni neno au kikundi cha maneno ambacho huelezea mtendwa wa jambo au kitu au mtu. Ni neno au kufungu cha maneno ambacho huelezea mtu, kitu au jambo linaloathiriwa moja kwa moja na na kitenzi. Mfano,

*Mwanafunzi anachota* ***maji***

**N**- Yambwa

**Yambiwa.** Nomino hufanya kazi kama **yambiwa**. Yambiwa ni neno ambalo hudokeza mtendewa wa jambo ambaye haathiriki moja kwa moja na kitenzi. Mfano,

*Mwanafunzi anamchotea* ***mwalimu*** *maji*

**N**-yambiwa

Kwa kawaida yambwa huweza kutokea peke yake lakini yambiwa ni lazima itokee pamoja na yambwa. Katika lugha ya Kiswahili, kimfuatano, *yambiwa* hutokea baada ya *kitenzi*; na *yambwa* hufuata baada ya *yambiwa*.

**Kijalizo.** Nomino huweza kuwa **kijalizo** kwa maana huwa ni neno linalokamilisha maana ya sentensi. Katika sentensi, nomino hii hutokea baada ya kitenzi. Kwa mfano,

*Juma ni* ***mwalimu***

**N**

Neno mwalimu limekamilisha taarifa kuhusu nomino Juma.

**Kikumushi.** Nomino pia huweza kufanya kazi kama kikumushi. Yaani, ni kipashio cha kisintaksia ambacho huongeza taarifa ya ziada kuhusu kipashio kingine. Mfano,

*Mtoto amelala **usingizi***.

Hapa, tungeweza kusema: *Mtoto amelala*, bado sentensi ingeeleweka.

**ii) Vitenzi Kisintaksia**

Vitenzi hutoa hufanya kazi kama kiarifu kwa maana hutoa taarifa kuhusu kinachofanywa au kinachomuhusu nomino ya mtenda/ kiima.

**iii) Vivumishi Kisintaksia**

Kivumishi hufanya kazi kama **kikumushi.** Hukumusha nomino au kiwakilishi cha nomino. Yaani hutoa taarifa ya ziada kuhusu nomino au kiwakilishi cha nomino. Mfano,

*Kunguru **mwoga** hukimbiza bawa lake.*

**N V**

Ni sawa na kusema, *kunguru hukimbiza bawa*.

Kivumishi hutumika kama **kijalizo**. Mfano, *Mage ni **mpole***. Kivumishi **mpole** kimekamilisha taarifa ya kitenzi shirikishi **ni**.

**iv) Viwakilishi Kisintaksia**

Kiwakilishi hujitokeza mwanzoni mwa sentensi na kuwa kama **kiima** (kinabainisha mtenda). Mfano,

***Ninyi*** *mnapenda kujisomea.*

Pia, kiwakilishi kina dhima ya kuwakilisha nomino. Mfano,

***Ninyi*** *mnapenda kujisome.*

Neno ninyi linaweza kuwakilisha wanafunzi/watu/vijana/, n.k.

**v) Vielezi Kisintaksia**

Vielezi vina dhima ya **kukumusha** *kitenzi, kivumishi* au *vielezi* vingine. Taarifa inayotolewa na kielezi huwa ni ya ziada kwa maana inaweza kuachwa katika sentensi bila kuathiri maana ya sentensi hiyo. Mfano,

*Uchafu **umezagaa** **<u>mno</u>**.*

**T E**

*Tatu ni **mweupe** **<u>sana</u>**.*

**V E**

*Mtoto anakula **kivivu** **<u>sana</u>**.*

**E E**

**vi) Vihusishi Kisintaksia**

Katika mpangilio wa sentensi kihusishi huwa na dhima ya kuonesha uhusiano wa maneno yanayojenga sentensi. Mara nyingi maneno haya huonekana kama kategoria nyingine ya maneno kama vile vielezi. Lakini, kisintaksia huwa na kazi nyingine. Mfano, vihusishi vya mahali, huhusisha mahali alipo mtu, kitu, au hali. Kama:

*Kuku yuko **<u>juu ya</u>** paa*

**H N**

*Alijificha <u>nyuma ya</u> nyumba*

**H N**

**vii) Viunganishi Kisintaksia**

Ni maneno yanayounganisha neno na neno lingine, au sentensi na sentensi. Maneno yanayotumika kama viunganishi ni kama na, au, lakini, hivyo, kwa sababu, n.k. Mfano,

*Baba **<u>na</u>** mama wamekaa chini ya mti.*

***U***

*Wanafunzi wamechoka **<u>lakini</u>** wanaendelea kucheza mpira*

***U***

*Mtoto anacheza, kaka anachota maji **<u>na</u>** dada anapika.*

***U***

Licha ya kwamba viunganishi hushabihiana na vihusishi, jambo la kuzingatia ni namna maneno hayo yanavyofanya kazi kwenye sentensi.

**viii) Vihisishi Kisintaksia**

Vihisishi vina dhima ya kuonesha hisia. Mara nyingi maneno haya hutokea mwanzoni mwa sentensi na kufuatiwa na sentensi yenye kuonesha hisia kama vile kushukuru, kuonya, furaha, masikitiko, hata mwigo wa sauti. Mfano,

*Vihisishi vya furaha*: Huree! Nimefaulu.

**I**

*Vihisishi vya mwigo sauti*: Alidondoka puu!

**I**

## Mbinu za Uundaji Maneno

Mpendwa mwanafunzi, katika somo la kwanza tuliona kuwa sifa mojawapo ya lugha ni kukua. Kukua kwa lugha hutokana na kuongeza msamiati ili kukidhi haja ya mawasiliano katika jamii. Zipo mbinu tofauti zinazosaidia kuongeza msamiati katika lugha. mbinu zifuatazo hutumika kuunda maneno katika lugha ya Kiswahili:

**i) Ukopaji**

Kukopa ni mojawapo ya mbinu ya kiisimu ambayo hutumiwa na lugha zote ulimwenguni kuunda istilahi na maneno mapya ili kukidhi mawasiliano katika miktadha anuwai. Hii ina maana ya kuchukua istilahi ya lugha fulani na kisha kuitumia kama istilahi katika lugha nyingine. Mbinu ya ukopaji inaweza kuwa:

***i) Ukopaji kwa tafsiri*** - maneno ya lugha chanzi (inayokopwa) hutafsiriwa katika lugha kopaji, mfano neno la Kiswahili *"soko huria"* limekopwa kutoka Kiingereza *"free market"*.

***ii) Utohozi*** - Neno lililokopwa hufanyiwa marekebisho kulingana na sheria za kifonolijia na kimofolojia za lugha kopaji. Mfano, *"Likizo ya ugonjwa"* katika Kiswahili yametoholewa kutoka Kiingereza *"Sick leave"*.

***iii) Ukopaji sisisi*** - Kukopa neno kutoka lugha kopwa bila kulifanyia marekebisho. Neno huchukuliwa kama lilivyo. Mfano neno la Kiingereza *"safari"* limekopwa sisisi kutoka lugha ya Kiswahili.

**ii) Ufupishaji**

Ufupishaji ni mbinu ambayo hutokana na kitenzi 'fupisha' chenye maana ya kufanya kitu kiwa kifupi au kupnguza urefu wa kitu. Kuna mbinu mbalimbali ambazo zinatumika katika ufupishaji wa maneno ambazo ni:

***i) Ufupishaji mkato:*** Baadhi ya silabi au vipashio huondoshwa kabisa na kuacha tu sehemu ya neno asilia, kwa mfano, Dar es Salaam=Dar, Morogoro=Moro.

***ii) Akronimu:*** Baadhi ya meneno hutokana na ufupisho wa maneno asilia. Ufupisho huu hutumia herufi au silabi za kwanza katika kirai au kikundi cha maneno kuunda neno jipya. Kwa mfano, UVIKO-19 = Ugonjwa wa Virusi vya Korona.

***iii) Uhulutishaji:*** Mbinu hii hukaribiana na mbinu ya akronimu, tofauti ni kwamba viambishi au sehemu ya mwanzo ya neno huunganishwa na sehemu ya kwanza ya neno, la pili kuunda neno la msamiati mpya. Kwa mfano:

| **Kifungu Asilia** | **Neno Jipya** |
|---|---|
| Chakula + jioni | chajio |

**iii) Uambishaji**

Ni mbinu ya uundaji maneno ambapo viambishi hupachikwa kabla au baada ya mzizi wa neno na kuunda neno la kategoria hiyo hiyo. Mara nyingi maneno yanayoambishwa huwa katika dhana ya umoja na wingi, ukubwa na udogo, n.k. Kwa mfano,

| | |
|---|---|
| M- tu | wa- tu |
| Ki- jiji | vi- jiji |

**iv) Uambatishaji**

Hii ni mbinu ambayo huhusisha kuunganishwa kwa maneno mawili kuunda neno moja jipya ambalo maana yake huwa tofauti na maneno ambayo yametumika kuunda neno hilo:

| **(a) Nomino** | **+** | **Nomino** | **Neno Jipya** |
|---|---|---|---|
| Bata | + | mzinga | Batamzinga |

| **(b) Nomino** | **+** | **Kivumishi** | **Neno Jipya** |
|---|---|---|---|
| Pembe | + | tatu | Pembetatu |

| **(c) Kitenzi** | **+** | **Nomino** | **Neno Jipya** |
|---|---|---|---|
| Chemsha | + | Bongo | Chemshabongo |

**v) Unyambulishaji**

Unyambulishaji au unyambuaji ni mbinu ya uundaji wa maneno mapya hivi kwamba viambishi mbalimbali huambikwa kwenye mzizi husika na kuunda neno jipya, kwa mfano; kutokana na mzizi {–imb-} tunapata maneno: *kulima, kilimo, limiana, mkulima,* n.k.

**vi) Uradidi**

Uradidi ni mbinu ya kuunda maneno ambayo sehemu ya neno lolote hurudiwarudiwa ili kuunda neno jipya au msisitizo fulani. Lengo kubwa la uradidi ni kusisitiza jambo au hali fulani. Kuna aina kuu mbili za uradidi yaani uradidi kamili na uradidi nusu.

*(a) Uradidi Kamili:* Huu ni uundaji wa maneno ambapo neno lolote hurudiwa. Mfano, *Pole + pole = polepole*; *Pili + pili = pilipili*

*(b) Uradidi nusu*, Huu ni uundaji wa maneno ambapo sehemu ya neno hurudiwarudiwa. Mfano ***baba**ika*, ***papa**rika*, n.k.

**vii) Uhamishaji**

Ni mbinu ya uundaji wa maneno ambao huhusisha upanuzi wa maana ya neno hupanuliwa na kurejelea dhana tofauti. Hata hivyo upanuzi huo huzingatia misingi iliyomo neno la kwanza na kujaribu kuzioanisha na maana, umbo, tabia na uamilifu wa neno la pili. Mfano, *"kupe"* ni mdudu anayenya damu. Lakini, neno *"kupe"* pia limetumika kama mtu mnyonyaji kwa kuwa anaishi kwa kuwategemea wenzake. Hivyo maana ya neno hilo imehamishwa kutoka kwa *mdudu* kwenda kwa *binadamu*.

**viii) Ubunifu**

Ubunifu ni mbinu ya kubuni msamiati na istilahi katika lugha husika na kurejelea dhana au vitu vipya ambavyo hapo awali

havikuwepo katika jamii husika. Kuna njia kuu mbili za kubuni misamiati na istilahi mpya katika lugha ambazo ni:

***(a) Kubuni pasi na vigezo au kinasibu***. Mfano, *"runinga"* limebuniwa kinasibu kutokana na neno la Kiingereza "television".

***(bi) Kubuni kwa kuongozwa na vigezo maalum*** kama vile kuzingatia mlio wa kifaa, mnyama, mdudu, n.k. Mfano, neno ***"mtutu"*** limebuniwa kutokana na mlio wa risasi zinapopigwa kutoka kwenye bunduki yaani, ***tu-tu-tu-tu***.

## Dhana ya Mofofonolojia

Mofofonolojia ni dhana inayohusisha dhana mbili tofauti; *mofo* ikiwa na maana ya 'umbo', na *fonolojia* ikiwa na maana ya 'sauti za lugha mahususi'. Kwa msingi huu, mofofonolojia pia mofofonimiki inaweza kufasiliwa kama *mabadiliko ya sauti za lugha ambayo katika mazingira maalum ya utokeaji wake huathiri baadhi ya mofimu zinazounda maneno*.

**a) Michakato ya Kimofofonolojia**

**i) Usimilisho**

Mchakato wa usilimisho ni aina ya maathiriano ambayo hutokea wakati ambapo fonimu moja katika neno hupoteza sifa ilizonazo na kupokea sifa za fonimu iliyo jirani yake. Kwa mfano, konsonanti inaweza kupata baadhi ya sifa za irabu au irabu ikapata baadhi ya sifa za konsonanti, na konsonanti moja huweza kuathiri konsonanti nyingine au irabu moja huweza kuathiri irabu nyingine. Kwa mfano, konsonanti huweza kuiathiri nazali inayofuatana nayo na kusababisha nazali kutamkiwa mahali pale ambapo konsonanti inatamkiwa. Lakini, kuna mazingira mengine nazali haiwezi kuathiriwa na sauti inayochangia mahali pa utamkaji. Kwa kawaida, nazali zote hutambulika kwa "N" kubwa. Kama katika mifano ifuatayo:

| **Mofimu za neno** | **matamshi yake** |
|---|---|
| i) N + goma | /ŋgɔmɑ/ |
| ii) N + bwa | /mbwɑ/ |
| iii) N + doo | /ndɔɔ/ |

Hapa, nazali /N/ ambayo hutamkiwa kwenye ufizi imejitokeza kama /**ŋ**/ inapofuatiwa na sauti **g** ya kaakaa laini; imejitokeza kama **/m/** inapofuatiwa na **b** ya midomo; lakini inabaki kuwa **/n/** inapofuatiwa na **d** ya ufizi (zinatamkiwa mahali pamoja)

**ii) Udondoshaji wa Fonimu**

Huu ni mchakato unaohusu kuachwa kwa sauti fulani katika matamshi wakati mofimu mbili zinapokaribiana. Yaani, sauti ambayo ilikuwepo katika umbo la ndani lakini katika umbo la nje hutoweka.

| **Kabla ya mabadiliko** | | **Baada ya mabadiliko** |
|---|---|---|
| A | Mu + tu | mtu |
| | Mu + sichana | msichana |
| B | Mu + ungwana | muungwana |
| | Mu + uguzi | muuguzi |

Kinachojitokeza katika data A ni kuwa irabu /u/ katika mofimu {mu-} ikifuatiwa na konsonanti halisi basi irabu hiyo hudondoshwa; lakini inapokaribiana na irabu inayofanana nayo katika data B hubaki kama ilivyo.

Pia udondoshaji hutokea pale ambapo irabu mbili zinapofuatana katika mpaka wa mofimu, kwa mfano

| **Umbo la ndani** | **Umbo la nje** |
|---|---|
| Hautaki | hutaki |
| Chaake | chake |

**iii) Ukaakaishaji**

Ukaakaishaji wa fonimu hutokea pale ambapo fonimu zisizo za kaakaa gumu zinapobadilika na kuwa za kaakaa gumu.

| **Umbo la ndani** | **umbo la nje** | **umbo la nje** |
|---|---|---|
| /ki+enu/ | [kjenu] = $k^y$enu | [ ʧenu] = chenu |
| /ki+ombo/ | [kjombo] = $k^y$ombo | [ ʧombo] = chombo |

Hapa tunaona kwamba kipasuo cha kaakaa laini /k/ kimebadili mahali pa matamshi na kuwa kizuiwa-kwamizi /ʧ/ (**ch**) cha kaakaa gumu katika mazingira ya kufuatiwa na sauti /j/ (**y**).

**iv) Tangamano la Irabu**

Huu ni mchakato ambao irabu mbili hukubali kuandamana katika mazingira maalumu. Kwa mfano irabu za utendea [i] na [e] katika lugha ya Kiswahili, utokeaji wake hutegemeana na irabu itakayojitokeza katika mzizi wa neno.

(i) Kama mzizi wa neno una irabu /i/, /u/ au /a/ basi irabu ya kiambishi cha utendea lazima kiwe ni [i], Mfano.

| **Kitenzi cha kawaida** | **Kitenzi cha utendea** |
|---|---|
| /imb+a/ | [imb-i-a] |
| /dak +a/ | [dak-i-a] |
| /andik+a/ | [andik-i-a] |
| /chun+a/ | [chun-i-a] |

(ii) Kama mzizi wa neno una irabu /e/ au /o/ katika hali ya utendea kiambishi chake kitakuwa ni [e]. Mfano,

| **Kitenzi cha kawaida** | **Kitenzi cha utendea** |
|---|---|
| /som+a/ | [som-e-a] |
| /og+a/ | [og-e-a] |
| /chez+a/ | [chez-e-a] |

Hapa mofu ya utendea ina alomofu mbili ambazo ni /i/ na /e/ ambapo alomofu /i/, inatokea pale ambapo mzizi unakuwa na irabu /i/,/u/ na /a/ kwa upande mwingine alomofu /e/ inatokea wakati mzizi wa kitenzi una irabu /e/ na /o/.

### v) Muungano wa Irabu

Mchakato huu hutokea pale ambapo irabu ya mofimu moja inapokaribiana na irabu ya mofimu nyingine katika mpaka wa mofimu, irabu hizo huungana na kuzaa irabu moja. Irabu hizo sharti moja iwe ya chini na nyingine ya juu. Mfano;

| **Kabla ya mabadiliko** | | | **Baada ya mabadiliko** |
|---|---|---|---|
| wa | + | enye | wenye |
| wa | + | izi | wezi |
| ma | + | ino | meno |

Lakini, katika mazingira mengine mabadiliko kama hayo hayawezi kutokea. Katika isimu tunaita "vighairi" kama katika mifano ifuatayo:

| | |
|---|---|
| wa+igiz+a+ji | waigizaji |
| wa+ingereza | waingereza |
| wa+oko+a+ji | waokoaji |

### vi) Uyeyushaji

Uyeyushaji pia hujulikana kama irabu kuwa nusu irabu. Huu ni mchakato ambapo irabu irabu za juu /u/ na /i/ hubadlika na kuwa /w/ au / j/ katika mazingira ya kufuatiwa na irabu zisizofana nazo. Kwa kifupi ni kwamba:

/u/ inapofuatiwa na irabu yoyote isiyofanana nayo hubadilika kuwa [w], na

/i/ ikifuatiwa na irabu yoyote isiyofanana nayo hubadilika na kuwa [j].

**Mfano wa /u/**

| **Kabla ya mabadiliko** | **Baada ya mabadiliko** |
|---|---|
| /mu+embe/ | [mweembe] |
| /mu+anafunzi/ | [mwaanafunzi] |

Hivyo tunaona wazi kuwa irabu ya juu nyuma /u/ imebadilika na kuwa kiyeyusho [w] katika mazingira ya kufuatiwa na irabu isiyofanana nayo ambayo ni /a/, /e/ na /o/.

**Mfano wa irabu /i/**

| **Kabla ya mabadiliko** | **Baada ya mabadiliko** |
|---|---|
| /mi+ezi/ | myeezi |
| /mi+eusi/ | myeeusi |
| /mi+oyo/ | myooyo |

Tunaona kuwa irabu ya juu mbele /i/ hubadilika na kuwa y inapofuatana na irabu nyingine isiyofanana nayo ambayo ni /e, a na o/.

Mpendwa mwanafunzi, licha ya taaluma za mofolojia na fonolojia kuwa na uhusiano mkubwa kupitia athari zilizobainishwa hapo juu, bado taaluma hizi zina utofauti mkubwa. Hii ni kwa sababu fonolojia inajishughulisha na uchambuzi na ufafanuzi wa sauti za lugha mahususi lakini mofolojia inahusika na uchambuzi wa maumbo ya maneno katika lugha.

## Tafakuri ya Somo




Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Unaweza kufafanua dhana zipi za msingi katika mofolojia?
2. Unaweza kuchambua aina za maneno kwa kigezo cha kisemantiki, kimofolojia na kisintaksia?

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Fafanua dhana zifuatazo kwa mifano:
   i) Mofu
   ii) Mofolojia
   iii) Mofimu
   iv) Mzizi wa neno
   v) Shina
   vi) Alomofu
2. Chambua aina za maneno ya Kiswahili kimofolojia.
3. Chunguza maneno kutoka katika lugha yako ya asili. Je, maneno hayo yameundwa kwa mbinu zipi?
4. Chambua viambishi vya maneno yafuatayo:
   i) Kilimo
   ii) Anajisomea
   iii) Kitakachokuja

# Somo la Sita

## Kutumia Sintaksia ya lugha ya Kiswahili

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita tulichambua mofolojia ya lugha ya Kiswahili. Tuliona kuwa mofolojia ni taaluma ya isimu inayochunguza maumbo ya maneno na kanuni zinazohusika na uundaji wa maneno katika lugha. Katika somo hili, tutajifunza kutumia sintaksia ya lugha ya Kiswahili. Kwa kuanza, tutafafanua dhana ya sintaksia, kisha tutafafanua dhana za msingi katika sintaksia kama vile kiima, kijalizo, n.k. Pia, tutachambua nadharia za sintaksia, kuchambua tungo za lugha ya Kiswahili, na kuchambua sulubu za miundo ya lugha ya Kiswahili. Mpendwa mwanafunzi, naamini baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili.

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana ya sintaksia;
- Kufafanua dhana za msingi katika sintaksia (Kiima, kiarifu, kirai, kishazi, kijalizo, kikumushi, n.k.);
- Kuchambua nadharia za sintaksia;
- Kuchambua tungo za lugha ya Kiswahili; na
- Kuchambua sulubu za miundo ya lugha ya Kiswahili.

### Kufafanua Dhana ya Sintaksia

**a) Maana ya Sintaksia**

Kwa mujibu wa Philipo (2013: 9), sintaksia ni neno lililotokana na lugha ya Kilatini likiwa na pande mbili "syn" na "taxis". Katika lugha ya kiingereza neno hili linaweza kutafsiriwa kama "put together" ambapo katika lugha ya Kiswahili tungeweza kutafsiri kama "weka pamoja". Yaani, kuweka pamoja vipashio vya lugha kwa kufuata utaratibu maalum. Vipashio hivyo vya lugha ni neno, kirai, kishazi na sentensi.

Hivyo, sintaksia inaweza kufasiliwa kuwa ni tawi la isimu linalochunguza miundo sahihi ya tungo na kanuni mbalimbali za lugha zinazotawala miundo hiyo. Katika uchunguzi huo, sintaksia huhusika na mpangilio wa tungo katika kiwango cha neno, kirai, kishazi na sentensi. Kipashio cha msingi katika sintaksia ni ***neno.***

**b) Historia ya Sintaksia**

Kwa mujibu wa Harper (2001-2010) *Online Etymology Dictionary*, neno sintaksia liliibuka takribani miaka ya 1600 (karne ya 5 Kabla ya Kuzaliwa Kristu (KK). Neno hilo lilitokana na neno la Kigiriki "*syntaxis"* ambalo maana yake ni kupanga au kuweka vitu pamoja katika mpango. Inaaminika kuwa Wagiriki ndio walioweka msingi wa taaluma ya lugha tuijuavyo hivi leo. Walianza kuchunguza lugha yao ya Kigiriki na kuweka nadharia za kifalsafa kuhusu asili ya lugha, Kazi hiyo ilianza kufanywa na mwanafalsafa mkuu wa kale aliyeitwa *Plato*, akifuatiwa na *Aristotle, Dionysius Thrax, Apollonius, Donatus* na *Priscian*. Hivyo Wagiriki wanaaminika kuwa ndio waanzilishi wa sintaksia (Khamis & Kiango, 2002: 1).

Baada ya kutoka Ugiriki, taaluma ya sintaksia iliendelea kukua na kuenea katika miji mingine ya Roma ambapo ilielezwa kwa kutumia lugha ya Kilatini; lugha inayoaminika kuwa na asili moja na Kigiriki. Mmoja wa wanaisimu mashuhuri wa Roma alikuwa *Marcus Terentius Varro* (Pia, Varro Reatinus) mwaka 116 hadi 27 Kabla ya Kristu. Kutoka katika Kilatini, sintaksia iliendelea kuchambuliwa katika lugha ya Kisanskriti ilimhusisha mwanaisimu wa India aliyeitwa *Panin*. Kisanskriti ni lugha iliyo katika kundi la India-Ulaya. Ni miongoni mwa lugha rasmi ya nchini India, na inaaminika kuwa mama wa lugha zote za nchini humo.

Baadae, sintaksia iliweza kuenea katika sehemu nyingine za Ulaya kupitia kwa wanaisimu mbali mbali akiwemo mwanaisimu maarufu wa Uswisi aliyeitwa *Ferdinand de Saussure* Mwanaisimu huyu anaaminika kuwa ndiye ***baba wa sarufi mamboleo***. Mwanaisimu huyu alifundisha isimu kwa miaka mingi. Kwa heshima, wanafunzi wake walikusanya nukuu alizotoa kwenye mihadhara, na kutoa kitabu kilichoitwa ***Course in General Linguistics*** mwaka 1916, ikiwa ni miaka mitatu baada ya yeye kufariki dunia.

Nchini Marekani kuliibuka wanaisimu mbalimbali kama vile, *Noam Chomsky, Leonard Bloomfield* na wengineo; ambao walikuwa na mchango mkubwa katika taaluma ya sintaksia. Kwa mfano, Noam Chomsky aliibua dhana ya *maumbo ndani na maumbo ya nje ya sarufi*.

## Dhana za Msingi Katika Sintaksia

**a) Kiima (K)**

Hiki ni kipashio kinachotambulishwa katika sarufi mapokeo. Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004: 160) kiima ni sehemu ya kwanza ya sentensi ambayo huelezwa na kiarifu, na kwamba huweza kukaliwa na nomino ya mtenda wa jambo au kiwakilishi cha nomino, au nomino ya kitendwa. Kwa mfano,

**K**

<u>Viumbehai wote</u> / hupumua

N V

**b) Kiarifu (A)**

Kiarifu ni dhana ambayo hufafanuliwa kama sehemu ya sentensi ambayo hutoa taarifa au jibu kuhusu kiima amefanya au hufanya nini. Mfano,

**A**

Viumbehai wote hupumua

T


**c) Kirai**

Kirai (au kikundi) ni neno au kifungu cha maneno ambacho hakina muundo wa kiima na kiarifu. Au ni kipashio cha kimuundo ambacho huweza kuwa neno moja au kifungu cha maneno kisicho na uhusiano wa kiima na kiarifu. Neno kuu ndio hutambulisha aina ya Kirai. Lugha ya Kiswahili ina miundo mikuu mitano ya virai. Miundo hiyo ni: kirai nomino (KN), Kirai kitenzi (KT), Kirai kivumishi (KV), Kirai Kielezi (KE), na Kirai kihusishi (KH). Mfano; **KN = N+ U + N = KN:** Baba na mama

**d) Neno kuu**

Ni dhana inayojitokeza kwenye muundo virai unaotokana na kategoria ya neno. Ndio kiini cha kirai kwa kuwa ndicho kinamiliki neno au maneno mengine katika kirai. Kwa mfano, katika kirai nomino, neno kuu ni kategoria ya nomino, katika kirai

kitenzi neno kuu linatokana na kategoria ya kitenzi, n.k. Chunguza mchoroti ufuatao hapo chini:




## Mjadala

Mpendwa mwanafunzi, jadiliana na mwanachuo mwenzako kuhusu sentensi hapo juu. Je, mmeweza kubaini neno kuu lipi katika mchoroti huo?

### e) Kishazi

Kishazi ni neno au kifungu cha maneno ambacho huwa na kitenzi kiwe kitenzi kikuu, kisaidizi au kishirikishi. Ni kipashio muhimu sana katika sentensi. Kwa kawaida kishazi huweza kusimama peke yake kama sentensi yenye maana kamili, au kishindwe kusimama peke yake mpaka kitegemee neno au kifungu kingine cha maneno ili kukamilisha maana.

### (i) Kishazi Kikuu (KK)

Ni tungo yenye kusimama peke yake na kutoa taarifa kamili bila kutegemea tungo nyingine. Tungo hii pia hujulikana kama kishazi huru (KHr). Mfano; ***Bibi anakata kuni***.

**(ii) Kishazi Tegemezi (KTeg)**

Ni tungo ambayo haiwezi kusimama peke yake. Hivyo hutegemea kishazi huru ili iweze kukamilika kimaana. Kwa kawaida kishazi tegemezi huwa na kitenzi kisicho kamili. Kitenzi kisicho kamili pia hujulikana kama *kitenzi kilichoshushwa hadhi*. Kushushwa hadhi kwa kitenzi hicho husababisha kiwe na muundo tegemezi. Kutokana na utegemezi huo, kishazi tegemezi huzua shauku ya kutaka kujua zaidi kuhusu mtu au jambo linaloelezwa. Mfano,

Nguo ili**yo**chanika ... (ifanywe nini? - ishonwe)

## f) Kijalizo

Ni dhana inayotokana na kitenzi 'jaliza' ambacho kina maana 'kamilisha'/ 'ongezea' habari ili kukamilisha au kutosheleza maana. Kwa ujumla tunaweza kusema: kijalizo ni neno au kifungu cha maneno ambacho hukamilisha taarifa. Hii ina maana kwamba kama kijalizo hakipo taarifa huwa haijakamilika. Kijalizo huanzia ngazi ya neno hadi sentensi. Kwa kawaida katika sentensi, kijalizo huweza kuwa nomino, kivumishi, kielezi, au kitenzi. Kwa mfano,

(a) Ndege wote... (wamefanya nini?)

Ndege wote wameruka

**T**

(b) Watanzania wengi huamini kuwa **umoja ni nguvu.**

**Kijalizo (S)**

## g) Kikumushi


Hili ni neno au kifungu cha maneno ambacho hutoa maelezo ya ziada katika sentensi. Neno au kifungu hicho cha maneno huweza kuwa katika kategoria ya nomino, kivumishi, kitenzi, kielezi, kihusishi, au sentensi. Hii ndio kusema, kikumushi **si** kipashio cha msingi katika tungo. Kinaweza kuachwa bila kuathiri maana ya sentensi. Kwa mfano;

Watanzania **wengi** ni wazalendo **kwa nchi yao**.

**Kikumushi (V)** **Kikumushi (H)**


**h) Shamirisho (SH)**

Ni kipashio cha sarufi/ mkabala wa kimapokeo ambacho hubainisha nomino inayojitokeza upande wa kiarifu (A). Ni neno linalojaza nafasi ya mtendwa katika sentensi. Mfano;




**i) Chagizo (CH)**

Hii ni sehemu ya sentensi inayokaliwa na neno katika sentensi lililo ndani ya kiarifu ambalo hufanya kazi ya kutoa taarifa jinsi au namna kitendo kinavyofanyika, mahali kinapofanyikia, wakati au idadi ya kitendo. Kwa kawaida maneno yaliyo kwenye chagizo ni vielezi. Mfano;




**j) Yambwa**

Katika mkabala wa kimapokeo yambwa hujulikana kama *shamirisho*. Ni kipashio kinachotaja nomino iliyopata athari au manufaa ya kitendo. Katika lugha ya Kiswahili sentensi huweza kuwa na yambwa moja au mbili.

**(i) Yambwa Tendwa**

Hii ni nomino ambayo hupata athari ya moja kwa moja ya kinachotendwa na kiima. Mfano,

Wakulima wanavuna **mahindi.**

**(ii) Yambwa Tendewa/Yambiwa**

Hii ni nomino ambayo hupata manufaa kutokana na jambo linalotendwa. Mfano,

Wakulima wanamvun**i**a **bibi** mahindi.

Lugha ya Kiswahili ni miongoni mwa lugha ambazo yambwa tendewa huwekwa kabla ya yambwa tendwa. Muundo wa yambwa tendewa hubainika kutokana na kuwepo kwa kiwakilishi cha utendea (-i-/ -e- au utendewa -iw-/ -ew-).

**k) Sentensi (S)**

Sentensi ni tungo yenye kutoa taarifa kamili. Ni tungo yenye kutoa taarifa kamili kwa kuwa ina kitenzi chenye maana kamili. Sentensi huainishwa kwa kuzingatia vigezo viwili; *kigezo cha maana* na *kigezo cha muundo*. (Tutafafanua zaidi katika vipengele vitakavyofuata).

**3) Nadharia za Sintaksia**

Nadharia inafasiliwa na Massamba (2004: 63) kuwa ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimawazo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kiolezo cha kuelezea jambo.

**a) Nadharia ya Sarufi Mapokeo**

Massamba na wenzake (1999: 42) wanasema, sarufi mapokeo (Traditional Grammar) ilianza karne ya 5 K.K na ilifikia kilele chake katika karne za 18 na 19 B.K. Philipo (2013: 87) akitumia dhana ya mkabala anasema, sarufi mapokeo iliibuka katika karne ya 3 Kabla ya Kristo (K.K.), na kwamba ilihusu lugha ya Kilatini na Kigiriki ambazo zilifanana sana kinasaba. Anaendelea kusema kuwa sifa kuu ya sarufi mapokeo ilikuwa elekezi zaidi, ikisisitiza matumizi sahihi ya lugha ya Kilatini.

Nadharia ya sarufi mapokeo iliasisiwa na wanasarufi wakongwe ambao walikuwa wanafalsafa wa Ugiriki. Habwe na Karanja (2004:129) wanataja wanafalsafa hao kuwa ni:

**Plato** aliigawa sentensi katika mafungu makuu mawili: (i) nomino: maneno yaliyoweza kufanya kazi ya kiima (ii) tendo: maneno yenye kueleza matendo, au sifa za kiima. Haya aliyaita kiarifu. Hivyo, kwa mujibu wa Plato, sentensi katika lugha, kama ilivyokuwa katika falsafa, ilitakiwa kuwa na kiima na kiarifu.

**Aristotle** aliobainisha njeo katika aina za maneno. Aidha, alianisha kitenzi elekezi na kitenzi kisicho elekezi. Pia aliendeleza kazi ya mwalimu wake kwa kuanisha aina tano za maneno: Nomino, Kitenzi, Kivumishi, Kiunganishi, na Kielezi.

**Protagoras,** kwa kutumia kigezo cha maana alianisha aina tatu za sentensi: swali, maelezo, amri.

**Dionysius Thrax** alianisha aina nane za maneno katika lugha ya Kigiriki: Nomino, kitenzi, faridipeke (particle), kibainishi (article), kihusishi, kibadala, kielezi, kiungo

**Appolonius**. Alikuwa Mgiriki. Alishughulikia uhusiano baina ya maneno. Mfano, **nomino na kitenzi:** Mfano, ***Mtoto (N) anakula (T)***, **kitenzi na kielezi**, **nomino na kivumishi**. Kuthibitisha hili, chunguza mifuatano mingine ya maneno yanayounda sentensi za lugha ya Kiswahili.

Warumi nao waliathiriwa na sarufi ya Kigiriki. Hawa walitumia mafanikio ya Wagiriki kama mfano wa kuelezea sarufi ya lugha yao ya Kilatini ambayo ilitokana na misingi ya Kigiriki. Miongoni mwa wanasarufi hao ni **Varro** ambaye alitenga viambishi na minyambuliko katika maumbo ya maneno.

**Ubora wa Nadharia ya Sarufi Mapokeo**

i) Ni nadharia ya kwanza kugawa sentensi katika pande mbili, *kiima na kiarifu*. Utaratibu huo unafuatwa hadi leo.
ii) Imesaidia kuanzisha dhana za kisarufi zinazotumika hadi sasa. Mfano, *kiima, kiarifu, nomino, kitenzi, kielezi, kivumishi, sentensi, mtenda, mtendwa.*
iii) Ni nadharia iliyofasili kategoria za kisarufi kama vile *njeo* (njeo ya wakati uliopo, uliopita, ujao), *nafsi* (katika umoja na wingi), *kauli* (kutenda, kutendwa, kutendea, n.k.), *uhusika* (kifaa/ ala, yambwa, yambiwa, n.k.), *dhamira* (kuuliza, kutoa taarifa, kutoa amri).
iv) Wanamapokeo katika nadharia hii walionesha namna ya kuchanganua sentensi ili kubainisha vipashio vinavyounda sentensi husika. Mfano, Sentensi inaundwa na Kiima na Kiarifu. Kisha, Kiima kinaundwa na **N/ W au N + V**, na Kiarifu kinaundwa na *Prediketa* (inahusisha vitenzi), *Shamirisho* (inahusisha nomino iliyo upande wa kiarifu), na *chagizo* (inahusisha vielezi).
v) Ilisaidia kueleza maana ya dhana mbalimbali. Mfano, nomino ni aina ya neno linalotaja jina la mtu, kitu, mahali.

vi) Ilisaidia kuibua watafiti waliochunguza lugha kisayansi kwa kuzingatia muundo wa lugha.
vii) Katika kipindi hiki Sarufi ilishughulikiwa sambamba na falsafa, dini, fasihi (hususani mashairi), n.k.

**Udhaifu wa Nadharia ya Sarufi Mapokeo**

i) Ilielekeza namna ya kutumia lugha kwa kufuata misingi ya Kilatini na Kigiriki. Walisema, lugha haipaswi kuanza na kiunganishi (kihusishi/kijalizo) wala kuishiwa na kihusishi. Mfano, sio sahihi kusema:

*Kwamba tusipokula mtatuchapa, mimi nakataa.*

ii) Iliamini lugha iliyo kwenye maandishi ndiyo bora. Hii ilisababisha wanamapokeo kutumia sarufi ya Kilatini na Kigiriki kuchambua lugha nyingine. Ilhali hakuna lugha bora kuliko nyingine.
iii) Haikuchambua lugha kwa kuzingatia muundo wa lugha husika. Kwa mfano, iliamini kuwa lugha huwa na muundo wa kiima na Kiarifu. Lakini, zipo lugha ambazo huwa na muundo wa Kiarifu kisha Kiima. Mfano,
iv) Haikuonesha uhusiano wa maneno yanayounda sentensi. Kwa mfao, walichanganya vipashio kama vile Kihusishi na nomino -

***Kiti <u>cha mtoto</u>*** badala ya ***Kiti <u>cha</u> <u>mtoto</u>***
**V** **H** **N**

**v)** Walidharau wazawa kwa misingi ya madaraja. Mfano, wasomi/ wanasiasa, watawala ndio walioonekana na sifa ya kuandika sarufi ya lugha Kilatini bila kuzingatia umilisi.

**b) Nadharia ya Sarufi Msonge**

Nadharia ya sarufi msonge (Scale-and-Category Grammar) ilianzishwa ili kuziba mapungufu yaliyojitokeza katika nadharia ya sarufi mapokeo. Mojawapo ya mapungufu hayo yalikuwa sarufi mapokeo kuelezea kuwa vipashio vya lugha ni neno na sentensi. Badala yake nadharia ya sarufi msonge inaiona lugha kama mfumo mkuu wenye mifumo mingine ndani mwake ambayo imepangiliwa kwa utaratibu wa kimsonge (Massamba na wenzake, 1999: 56). Ni nadharia iliyoasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani aliyejulikana kama Michael A. K. Halliday, mwaka 1960.

Katika nadharia hiyo, Halliday anabainisha kuwa lugha hujengwa na vipashio ambavyo hupangwa kingazi/ kimadaraja; kuanzia ngazi ya juu hadi ngazi ya chini. Kwamba, kipashio kikubwa ambacho ni

sentensi hujengwa na vipashio vya chini yake ambavyo ni vishazi. Vishazi navyo hujengwa na virai, ambavyo navyo hujengwa na maneno; maneno ambayo nayo hujengwa na mofimu mbalimbali. Mpangilio huo una maana kwamba kila kipashio cha lugha kina kipashio kimoja au zaidi cha kipashio cha chini yake. Mfano:

| | |
|---|---|
| **Sentensi moja:** | ***Anachezea kijiko***. Imejengwa na: |
| **Kishazi kimoja:** | *Anachezea kijiko.* = kishazi huru |
| **Virai viwili:** | *Anachezea* *kijiko*<br>KT KN |
| **Maneno matatu:** | *1) Anachezea* *2) Kijiko*<br>T N |
| **Mofimu saba:** | *A-na-chez-e-a* *ki-jiko*<br>1 2 3 4 5 6 7 |
| **Fonimu** | *A-n -ch-e-z- k-i-j-o*<br>1 2 3 4 5 6 7 8 9 |

**Ubora wa Nadharia ya Sarufi Msonge**

i) Nadharia ya sarufi msonge imesaidia kubainisha vipashio vingine vya lugha mbali ya sentensi na neno ambavyo vimetajwa katika sarufi mapokeo. Vipashio hivyo ni vishazi, virai, na mofimu.
ii) Nadharia hii imeweza kubainisha kuwepo kwa kishazi tegemezi ambacho katika sarufi mapokeo kilijulikana kama kivumishi.

**Udhaifu wa Nadharia Msonge**

i) Kuna uwezekano wa kuacha baadhi ya vipashio vya lugha. Kwa mfano, kiunganishi endapo kitatumika kuunganisha kishazi au kirai fulani ni wazi kuwa kiunganishi hicho hakiwezi kuwa katika daraja la kishazi wala kirai Watoto walikwenda kuwinda lakini hawakurudi na kitoweo.
ii) Kuna uwezekano wa kuchambua sentensi kwa kuzingatia maana na sio muundo.

**c) Nadharia ya Sarufi Miundo Virai**

Sarufi miundo virai (Phrase Structure Grammar) ni nadharia iliyojikita katika kuchambua tungo kwa kuzingatia miundo virai. Baadhi ya waanzilishi wa nadharia hii ni Ferdinand De Saussure anayeaminika kuwa ndiye *baba wa sarufi mamboleo*, Nikolaj Trubertzkoy, Leonard bloomfield, Edward Sapir.

**Misingi ya Sarufi Miundo Virai**

i) Sentensi hugawanywa katika miundo mikuu miwili, Kirai Nomino (KN) na Kirai Kitenzi (KT). KN nacho kiligawanywa katika N/ W au N + KV.

ii) Uchanganuzi wa wa sentensi huzingatia muundo kuliko maana. Yaani, kuangali vipashio vinavyounda sentensi.

iii) Lugha huchunguzwa kwa misingi ya lugha husika. Kwani kila lugha ina upekee wake.

**Ubora wa Nadharia ya Sarufi Miundo Virai**

i) Huonesha hadhi ya vipashio vinavyojenga tungo, kuanzia cha juu (aina ya sentensi) hadi cha chini (maneno yanaounda sentensi hujitikeza kwa chini.
ii) Huonesha jinsi vipashio vinavyotawala au kumiliki vipashio vingine. Mfano, S hutawala KN na KT; KN hutawala N, KV, KH na KE

**Udhaifu wa Nadharia ya Sarufi Miundo Virai**

i) Nadharia hii haioneshi muundo usio na ukomo (sentensi za uchamko).
ii) Haikuweza kuonesha uhusiano wa sentensi mbili zilizo na dhana ya aina moja. Mfano, *"Baba anakata mti"* (sentensi tenda) kuwa *"mti unakatwa na baba"* (sentensi tendwa); au sentensi zenye urejeshi (baba aliyekata mti...).
iii) Kanuni za miundo virai haikuwa na uwezo wa kuunganisha sentensi mbili zilizo na maana sawa. Mfano,
    Baba analima.
    Mama analima.
iv) Walichanganua miundo ya sentensi za lugha mbalimbali kwa kutumia muundo wa lugha ya Kiingereza. Wakati miundo ya lugha hutofautiana.

**d) Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi**

TUKI (1990) wanasema, Sarufi geuza maumbo zalishi (SGMZ) (Transformation Generative Grammar) ni nadharia ya sarufi iliyotilia umuhimu uwezo wa kanuni chache za kisarufi kuweza kuunda sentensi nyingi zenye urefu usio na kikomo. Kimsingi, ni nadharia inayoweza kufafanuliwa kama mfumo wa kanuni ambazo huweza kutumika kuzalisha sentensi nyingi kutokana na sentensi msingi moja. Nadharia hii iliasisiwa na mwanaisimu wa Kimarekani, Noam Chomsky mwaka 1957 katika kitabu chake

"Syntactic Structures" na kuiendeleza mwaka 1965 katika kitabu chake alichokiita "Aspects of the Theory of Syntax".

**Misingi ya Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi**

Nadharia ya sarufi geuza maumbo zalishi (SGMZ) ilikuwa na misingi ifuatayo:

i) Sentensi ina miundo mikuu miwili; muundo wa ndani (umbo la ndani) na muundo wa nje (umbo la nje). Kwamba, muundo wa ndani ni dhana dhahania ambayo hujenga maana ya sentensi. Muundo wa nje ni sehemu ya sentensi tunazozizungumza au kuziandika. Sentensi hizo zimetokana na umbo la ndani kabla ya kupokea mabadiliko.

ii) Mageuzi huanzia kwenye muundo wa ndani kabla ya kuufikia muundo wa nje.

iii) Ili kulipata umbo la nje lazima kanuni za mageuzi zitumike kutoka umbo la ndani kuelekea la nje. Hii ina maana kuwa kuna mageuzi yalifanyika ndipo tukapata umbo la nje la sentensi kwa mfano ya utendwa, urejeshi, swali, utendea, n.k. Kanuni hizo ni:

**Udondoshaji:** Kukiondoa kipashio fulani katika sentensi. Kwa mfano katika sentensi zenye ukanushi:

**Sentensi yakinishi:** Juma anasoma kitabu
**Sentensi kanushi:** Juma **h**~~**a-**~~a~~na~~som~~a~~**i** kitabu

**Uhamishaji:** Kukiondoa kipashio kimoja katika nafasi yake na kukihamishia mahali pengine. Kwa mfano katika sentensi ya utenda kuwa utendwa:

**Sentensi tenda: Babu** amekata mti
**Sentensi tendwa:** Mti umekatwa na **babu**

Katika sentensi ya kwanza, neno babu liko mwanzoni. Lakini katika sentensi ya utendwa, neno babu limehamishiwa mwishoni.

**Upachikwaji/ uchopekaji:** Kukiweka kipashio ambacho hapo awali hakikuwepo katika sentensi. Kwa mfano,

**Sentensi tenda: Babu** amekata mti
**Sentensi tendwa:** Mti umekatwa na **babu**

Kiambishi cha utendwa -w- kimepachikwa kati na mzizi **kat-** na irabu tamati **a**: kata - kat-**w**-a. Vilevile, kihusishi **"na"** kimepachikwa kati ya neno **umekatwa** na neno **baba**.

**Ubadilishaji:** Kukiweka kibadala cha kipashio fulani katika sentensi. Mfano,

**Umbo la nje:** Kaka ame**ji**pikia chakula


**Umbo la ndani:** $Kaka_1$ pika $kaka_2$ chakula

Kiambishi **-ji-** kimewekwa badala ya neno $kaka_2$.

iv) Mageuzi yafanyike kwa kuhusisha sentensi rahisi (ambazo hazijapokea mabadiliko). Mfano, Baba uza ng'ombe.

v) Mti wa matawi (mchoroti) hutumika kuonesha mchakato wa mageuzi ya miundo virai. Mfano,

**Umbo la ndani na nje la sentensi:** Kaka alijipikia chakula




vi) Sarufi ifafanuliwe kwa kuzingatia *umilisi* (yaani, sheria ambazo msemaji mzawa anazijua) na *utendaji* (utumiaji wa sheria) wa wazawa wa lugha.

**Ubora wa Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi**

i) Nadharia ya sarufi geuza maumbo zalishi imesaidia kuonesha uhusiano wa sentensi zilizoonekana kama mbili tofauti.

ii) Pia, nadharia hii imesaidia kuondoa utata; Kwa mfano, **Ali amempigia Tatu mpira**

Ali amepiga mpira kuelekea kwa Tatu

Ali amempiga Tatu kwa sababu ya mpira

Ali amempiga Tatu kwa mpira

iii) Vile vile, nadharia hii imesaidia kuonesha miundo ya sentensi iliyofichwa. Mfano, kutokana na nadharia hii ndipo tutaweza kuonesha jinsi sentensi za kujitendea, utendwa, ukanushi, swali, n.k zinavyopatikana.
iv) SGMZ imesaidia kuonyesha jinsi sentensi inavyoshushwa hadhi hivyo kusababisha iwe tegemezi kwa nyingine.

**Ubora wa Nadharia ya Sarufi Geuza Maumbo Zalishi**

v) Nadharia ya sarufi geuza maumbo zalishi imesaidia kuonesha uhusiano wa sentensi zilizoonekana kama mbili tofauti.
vi) Pia, nadharia hii imesaidia kuondoa utata; Kwa mfano, **Ali amempigia Tatu mpira**

Ali amepiga mpira kuelekea kwa Tatu
Ali amempiga Tatu kwa sababu ya mpira
Ali amempiga Tatu kwa mpira

vii) Vile vile, nadharia hii imesaidia kuonesha miundo ya sentensi iliyofichwa. Mfano, kutokana na nadharia hii ndipo tutaweza kuonesha jinsi sentensi za kujitendea, utendwa, ukanushi, swali, n.k zinavyopatikana.
viii) SGMZ imesaidia kuonyesha jinsi sentensi inavyoshushwa hadhi hivyo kusababisha iwe tegemezi kwa nyingine.

**4. Kuchambua Tungo za Lugha ya Kiswahili**

Kwa mujibu wa Massamba na wenzake (1999: 68), tungo ni nomino ambayo hutokana na kitenzi "tunga" yaani *kushikamanisha vitu pamoja kwa kupachika kitu kama uzi, n.k. ndani mwake ili kupata utungo*. Wakihusisha dhana ya tungo katika taaluma ya sarufi wanasema, tungo ni kuweka pamoja au kupanga pamoja vipashio sahili ili kujenga kipashio kikubwa zaidi. Wanagawanya tungo za lugha ya Kiswahili katika makundi makubwa manne.

**a) Tungo Neno**

Tungo-neno ni kipashio cha lugha ambacho hutokana na muunganiko wa vipashio mbalimbali vya lugha kuanzia fonimu hadi mofimu au viambishi huru au tegemezi kutegemeana na muundo wa lugha. Katika lugha ya Kiswahili, tungo-neno huweza kuundwa kwa *silabi, mofimu au viambishi*. Hebu tuone mpangilio wa vipashio hivyo:


**Tungo-Neno Kutokana Mpangilio wa Silabi**

- Maneno yanayoundwa na silabi ya **irabu peke** yake. Mfano, $**u**$ + $**a**$ = Ua, $**a**$ + $**u**$ = Au, n.k.
- **Muundo wa konsonanti pekee (K)** – Kiswahili hakina maneno mengi yanayoundwa na silabi konsonanti pekee isipokuwa maneno machache ambayo huwa ni ya nazali /m/ na /n/. Nazali hizo hujitokeza ama mwanzoni au katikati ya neno. Mfano; $**m**$ + $bwa$ = mbwa, $**n**$ + $chi$ = nchi n.k.
- **Muundo wa konsonanti na irabu (KI)** – Katika muundo huu konsonanti hutangulia irabu. Mfano; $ma$ = ma, $na$ = na, n.k.
- **Muundo wa konsonanti, konsonanti, kiyeyusho na irabu (KKkI)** – Muundo wa namna hii hujitokeza katika maneno machache. Mfano; $chu$ + $***ngw***a$, $shi$ + $***ndw***a$, n.k.
- **Muundo wa IK**– Muundo huu hujitokeza katika maneno machache ambayo huwa ya mkopo. Mara nyingi silabi hizi huishia na konsonanti. Mfano; **Al**+fa+ji+ri = $**Al$ + $**fa$ + $ji$ + $ri$, n.k.
- **Muundo wa KIK** – Muundo huu pia hujitokeza katika maneno machache ambayo huwa ya mkopo. Mara nyingi silabi hizi huishia na konsonanti. Mfano; $**lab$** + $da$ = ***Lab***da.

**b) Tungo Kirai**

Massamba na wenzake (2009: 84) wanafasili dhana ya kirai kuwa ni kipashio cha kimuundo chenye neno moja au zaidi lakini ambacho hakina uhusiano wa kiima-kiarifu. Habwe na Karanja (2004) wao wanasema, kirai ni neno au maneno ambayo aghalabu hujumuisha neno kuu na maneno mengine.

Hivyo, tunaweza kusema kwamba kirai ni neno au fungu la maneno linalotawaliwa na neno kuu kutegemeana na kategoria ya neno. Maneno yanaweza kuwekwa katika makundi mawili: maneno makuu ambayo hujumuisha nomino, vivumishi, vitenzi, vihusishi, na vielezi; na maneno madogo hujumuisha viwakilishi, viunganishi na vihisishi. Maneno makuu ndiyo yanayounda aina za vishazi. Kirai huwa na sifa zifuatazo: (i) Kipashio cha msingi katika kikundi cha kirai huitwa neno kuu au kichwa cha kirai. (ii) Aina ya neno ndilo linalotambulisha aina ya kirai. (iii) Huzingatia upatanisho wa kisarufi. Mfano;





**Aina za Virai**

**i) Kirai Nomino (KN)**


Kirai nomino ni neno au kifungu cha maneno ambacho neno lake kuu ni nomino. au kiwakilishi. Hivyo, katika kirai nomino ni lazima nomino au kiwakilishi kijitokeze mwanzoni mwa kirai.

**Muundo wa KN**


**Nomino pekee (N). Mfano,**





**Kiwakilishi pekee (W)**





**N + U + N**





**N + V/ KN**





**N + KTg**



**N + V + KTg**




**N + KH**





**ii) Kirai Kitenzi (KT)**


Kirai kitenzi ni neno au kifungu cha maneno ambacho neno lake kuu ni kitenzi.

**Muundo wa KT**


**Kitenzi pekee (T). Mfano,**





**Kitenzi na kirai nomino (T + KN)**





**Kitenzi na kitenzi (Ts + T)**




**Kitenzi na kirai kielezi/ kielezi (T + KE/E)**



**Kitenzi na kirai kihusishi (T + KH)**





**iii) Kirai Kivumishi (KV)**


Kirai kivumishi ni neno au kifungu cha maneno ambacho neno lake kuu ni kivumishi.

**Muundo wa KV**

**Kivumishi pekee (V). Mfano,**




**Kivumishi na nomino au kirai nomino (V + N/ KN)**





**iv) Kirai Kihusishi (KH)**

Kirai nomino ni neno au kifungu cha maneno ambacho neno lake kuu ni kihusishi.

**Muundo wa KH**

**Kihusishi na nomino (H + KN). Mfano,**





**v) Kirai kielezi (KE)**


Kirai nomino ni neno au kifungu cha maneno ambacho neno lake kuu ni kielezi.

**Muundo wa KE**

**Kielezi pekee (E). Mfano,**




**Kielezi na kielezi (E + E). Mfano,**




**3. Tungo Kishazi**

Kishazi ni neno au kifungu cha maneno ambacho huwa na kitenzi kiwe kitenzi kikuu, kisaidizi au kishirikishi. Ni kipashio muhimu sana katika sentensi. Kwa kawaida kishazi huweza kusimama peke yake kama sentensi yenye maana kamili, au kishindwe kusimama peke yake mpaka kitegemee neno au kifungu kingine cha maneno ili kukamilisha maana.

**Aina za vishazi**

Kuna aina kuu mbili za vishazi; *kishai huru* na *kishazi tegemezi*.

**i) Kishazi Huru**

Ni aina ya kishazi ambacho huwa na kitenzi kamili. Ni kishazi ambacho hutoa taarifa kamili. Mfano, **Bibi ametua mzigo wake.**
KK

**ii) Kishazi Tegemezi**

Ni tungo ambayo haiwezi kusimama peke yake. Hivyo hutegemea kishazi huru ili iweze kukamilika kimaana. Kwa kawaida kishazi tegemezi huwa na kitenzi kisicho kamili ambacho huwa na muundo tegemezi wenye virejeshi kama vile -ye-, -zo-, n.k. kutegemeana na nomino inayorejelewa. Mfano,

Ng’ombe ali**ye**zeeka ... (afanywe nini?)

Ng’ombe ali**ye**zeeka (achinjwe/ auzwe n.k).

**4. Tungo Sentensi (S)**

Sentensi ni tungo yenye kutoa taarifa kamili. Ni tungo yenye kutoa taarifa kamili kwa kuwa ina kitenzi chenye maana kamili. Sentensi ndicho kipashio kikubwa katika mfumo wa mawasiliano ya mwanadamu. Kuna vigezo viwili vinavyotumika kuanisha sentensi; kigezo cha maana na kigezo cha muundo.

**a) Aina za Sentensi kwa Kigezo cha Uamilifu (Kisemantiki)**

Matinde (2012: 160) anaeleza kuwa uainishaji wa sentensi kwa kigezo cha uamilifu huzingatia ujumbe unaowasilishwa na sentensi husika. Anabainisha aina nne za sentensi kwa kigezo hiki.

**i) Sentensi Arifu (Taarifa au Maelezo)**

Hii ni aina ya sentensi ambazo hutoa taarifa au ujumbe fulani. Sentensi hizi huishia na kituo kikuu (nukta (**.**). Mfano,

*Mtoto anaimba.*

**ii) Sentensi Swalifu (Ulizi)**

Hii ni aina ya sentensi ambayo hufikisha ujumbe kwa njia ya kuuliza swali. Sentensi hii huishia kwa alama ya kuuliza (**?**). Mfano, *Nani anaimba?*

**iii) Sentensi Amrishi (Amri)**

Hii ni aina ya sentensi ambayo hufikisha ujumbe kwa njia ya kutoa amri. Humwamrisha mtu afanye jambo fulani. Sentensi amrishi huundwa na kitenzi cha kuamuru ambacho hujitokeza upande wa kiarifu tu. Kwa kawaida sentensi hii hubainishwa kwa kituo kikuu au alama ya mshangao. (**.** / **!**). Mfano, *Ondoka hapo haraka!*

**iv) Sentensi Mshangao**

Hii ni sentensi ambayo hubainisha mshangao wa msemaji kuhusu jambo au hali fulani. Sentensi ya mshangao huishia na alama ya mshangao (**!**). Mfano, *Ameshindwa kuimba!*

**b) Aina za Sentensi kwa Kigezo cha Kimuundo (Kisintaksia)**

Hiki ni kigezo cha kuainisha sentensi kwa kuzingatia muundo wa vipashio vinavyounda sentensi hiyo. Kimuundo, kuna aina tatu za sentensi:

**i) Sentensi Sahili**

Ni sentensi ambayo ina kishazi kikuu kimoja. Mara nyingi sentensi hii huwa na pande mbili; kikundi nomino (KN) na kikundi kitenzi (KT). ina hii ya sentensi huwa na miundo ifuatayo:

**Kitenzi kikuu pekee:**

*Anakimbia*
T

**Kitenzi kisaidizi (+ kitenzi kisaidizi kimoja au zaidi) na kitenzi kikuu:**

*Walikuwa wanapanda mahindi.*
Ts T

*Walikuwa wanapenda kwenda mjini*
Ts Ts Ts T

**Kitenzi kishirikishi:**

*Watoto wangali shuleni.*
t

*Babu yu mgonjwa*
t

*Mchagua jembe si mkulima*
t

**ii) Sentensi Changamani**

Hii ni aina ya sentensi ambayo ina kishazi kikuu kimoja na kishazi tegemezi ambacho kinaweza kuwa kimoja au zaidi. Kishazi tegemezi hukitegemea kishazi kikuu ili kukamilisha taarifa.

**Miundo ya Sentensi Changamani**

**Muundo wenye vishazi rejeshi:**

Gari lili**lo**haribika limetengenezwa.
K/Tg KK

**Muundo wenye vishazi tegemezi viwili:**

*Miti i**ngali**mwagiliwa kwa wakati ~~[Miti]~~ isi**ngali**kauka*
K/Tg KTg

**Muundo wa kishazi tegemezi na kishazi kikuu:**

*Walisema kwamba watasoma kwa bidii*
K/Tg KK

**iii) Sentensi Ambatani**
Hii ni aina ya sentensi ambayo huwa na vishazi viwili au zaidi vilivyounganishwa kwa kutumia viunganishi kama: na, lakini, au. Pia, huweza kutumia alama ya mkato. Sifa kuu ya sentensi ambatani ni kuwa na muunganiko wa vishazi vikuu.

**Miundo ya sentensi ambatani**

**Sentensi sahili mbili: S-sahili + S-sahili**
*Alienda chuoni* ***ingawa*** *alikuwa anaumwa.*
**S-sahili$_1$ U S-sahili$_2$**

**Sentensi sahili changamani na sentensi sahili: S-changamani + S-sahili**
*Ndizi zilizooza zilitupwa jalalani lakini watoto waliziokota.*
**S-changamani U S-sahili**

**Sentensi changamani pekee: S-changamani + S-changamani**
*Aliyekikimbilia hakukiokota* ***lakini*** *aliyekiokota hakukila.*
**S-changamani$_1$ U S-changamani$_2$**

**Muundo wenye vishazi visivyounganishwa kwa viunganishi**
Miundo ya vishazi vyote huishia na virai vitenzi vyenye kiambishi tamati **'e'**. Kwa mfano,
*Waambie waache*
*Mwache aende*

**5. Kuchambua Sulubu za Miundo ya Lugha ya Kiswahili**

Miundo ya lugha ya Kiswahili imegawanyika katika makundi makuu mawili: *Miundo sahili* na *Miundo changamani*.

**a) Miundo Sahili**
Hii ni miundo yenye sentensi ambazo huweza kusimama peke yake bila kutegemea sentensi nyingine. Mfano,

**Sentensi sahili:** *Wanafunzi wamo darasani.*

**b) Miundo Changamani**
Hii ni ile inayohusisha tungo isiyoweza kusimama peke yake. Kwa mfano, *miundo ya sentensi zenye uchamko.* Uchamko kuwa ni sifa ya kisarufi inayowezesha sentensi nyingi zisizo na kikomo kuweza kutungwa kutokana na kanuni fulani. Uchamko uko wa aina mbili; *uchamko wa ambatizi* na *uchamko tegemezi* (Philipo, 2013: 106-111).

**i) Uchamko Ambatizi**

Ni muundo wa sentensi mbili au zaidi zenye hadhi sawa, ambapo kila sentensi huambatana na sentensi nyingine ili kuunda sentensi moja kwa kutumia viunganishi kama vile *na*, *au, lakini*, n.k. Mfano,

*[Baba analima] [Mama anapika][Dada anachota maji]*.

Katika uchamko ambatizi, sentensi hizo tatu zitakuwa kama ifuatavyo:

*Baba analima* ***na*** *mama anapika* ***lakini*** *dada anachota maji.*

**ii) Uchamko Tegemezi**

Ni muundo wa sentensi ambazo zinafanya kazi kama viambajengo katika muundo wa sentensi zinazojitegemea ambazo huunganishwa na kuwa sentensi moja (Philipo, 2013: 111). Mfano,

*[Mwalimu anadhani]*. *[Wanafunzi wamo darasani]*.
*[Mwalimu anadhani wanafunzi wamo darasani]*

**iii) Uchamko Wenye Vishazi Rejeshi**

Urejeshi ni dhana inayofafanuliwa na Massamba na wenzake (1999:). Uchamko huu huwa na kiambisha cha **-o- rejeshi** kilichojitokeza katika kitenzi: kuwa ni. Mfano,

*[Vijana walianzisha miradi]*. *[Vijana wapewe mikopo]*.
*[Vijana wali****o****anzisha miradi midogomidogo wapewe mikopo]*.

**iv) Uchamko wenye Vijalizo**

Ni miundo changamani yenye kuunganisha sentensi kwa kutumia vijalizo kama vile *kuwa, kwamba, na kama*. Mfano,

*[Mwalimu alisema]* *[Wanafunzi wakae kimya]*.
*[Mwalimu alisema]* ***kuwa*** *[wanafunzi wakae kimya]*.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, ni imani yetu kuwa baada ya kujifunza somo hili, umeweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Sasa basi, hebu chukua kalamu yako na daftari ufanye zoezi fupi ili kupima uelewa wako kuhusu mambo uliyojifunza katika somo hili.

1. Unazielewaje nadharia za sintaksia?
2. Unazielewa tungo za lugha ya Kiswahili?
3. Unaelewa sulubu za lugha ya Kiswahili? Eleza.

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Fafanua dhana zifuatazo:
   a) Sintaksia
   b) Kiima
   c) Kirai
   d) Kishazi
2. Eleza nadharia mbalimbali za sintaksia.
3. Chambua tungo za lugha ya Kiswahili.
4. Tumia mifano kuonesha miundo mbalimbali ya sentensi za lugha ya Kiswahili.

# Somo la Saba

## Kutumia Semantiki na Pragmatiki

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita tulijifunza kutumia sintaksia ya lugha ya Kiswahili. Katika somo hili utajifunza kutumia semantiki na pragmatiki. Tutaanza kufafanua dhana za semantiki na pragmatiki, na kufuatiwa na kufafanua dhana za msingi katika semantiki na pragmatiki. Kisha, tutaeleza uhusiano kati ya semantiki na pragmatiki. Pia, tutaeleza viwango vya maana na kufafanua aina za maana. Mwisho, tutachambua nadharia za maana. Mpendwa mwanafunzi, naamini baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili.

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana za semantiki na pragmatiki;
- Kufafanua dhana za msingi katika semantiki na pragmatiki (utajo, urejeleo, fahiwa, n.k.);
- Kufafanua uhusiano na umuhimu wa semantiki na pragmatiki;
- Kuchambua viwango vya maana;
- Kufafanua aina za maana; na
- Kuchambua nadharia za maana.

## Dhana ya Semantiki na Pragmatiki

### a) Maana ya Semantiki

Lugha hujengwa kimuundo na pia kimaana. Hata hivyo, maana ndio kipengele cha muhimu zaidi kwa kuwa ndicho kinachorahisha mawasiliano baina ya watu katika jamii. Dhana ya maana ni kipengele kinachochunguzwa katika taaluma ya semantiki.

Semantiki ni nini? Semantiki ni dhana iliyotokana na maneno mawili ya Kigiriki: **sema** yaani ishara (maana), na **ntic** yaani sayansi. Hivyo tunaweza kusema semantiki ni taaluma ya isimu au tawi la isimu linalochunguza maana katika viwango mbalimbali

vya lugha ya mwanadamu. Viwango hivyo ni mofu, neno au sentensi.

### b) Maana ya Pragmatiki

Akitumia dhana ya isimu amali, Matinde (2012: 284) anasema, pragmatiki ni utanzu wa isimu unaochunguza maana ya msemaji katika muktadha fulani kulingana na namna msikilizaji anavyotafsiri. Pragmatiki huhusisha uchaguzi wa lugha maalumu.

## Dhana za Msingi katika Semantiki na Pragmatiki

Licha ya kuelezwa kama dhana zinazohusu pragmatiki bado dhana hizi pia zinaweza kuhusishwa na semantiki kwa kuwa taaluma zote zinachunguza maana ingawa semantiki huchunguza maana ya msingi wakati pragmatiki huchunguza maana kwa kuzingatia muktadha. Baadhi ya dhana hizo ni kama zifuatazo:

**a) Udhanilizi** – Hii ni dhana inayotokana na msemaji kudhani msikilizaji au wasikilizaji wake wanafahamu kitu au jambo analosema (Matinde 2012: 293). Matinde anagawa udhanilizi katika pande kuu mbili, udhanilizi wa kisemantiki na udhanilizi wa kipragmatiki (tutakaohusika nao). Kwa mujibu wa Matinde, udhanilizi za kipragmatiki/ isimu amali umegawanyika katika aina kuu sita. Baadhi ya udhanilizi huo ni:

**i) Udhanilizi Ukweli**

Huu hutokana na matumizi ya maneno ambayo hueleza jambo la kweli. Kwa mfano, sikudhani kama watu wangejaa vile (Ni kweli kuwa watu walijaa katika mazishi ya Maalim Seif).

**ii) Udhanilizi Kinzani**

Huu ni udhanilizi unaobainisha si tu uongo bali pia unabainisha jambo kinyume na matarajio ya mtu. Kwa mfano, Ningekuwa na ndege ningekupeleka Uingereza (Ukweli ni kuwa sina ndege hivyo si rahisi mimi kukupeleka Uingereza).

**b) Utajo** - Ni dhana inayotokana na kitenzi ‘taja’. Hivyo, dhana hii inahusishwa na kitu au mtu yeyote anayetajwa. Kwa mfano,

ukitaja Asha, Mwajuma, Ali, n.k. Au kutaja kitu kama vile kiti, meza, dawati, n.k.

**c) Urejeleo** - Ni dhana inayotumika kueleza kitu au mtu na kitu au mtu halisi aliyeko kwenye jamii. Ni kuona kitu au mtu kwa uwazi kwa kuzingatia sifa zake kama ni mweusi, mweupe, mrefu, mfupi, n.k. Hata hivyo, kuna vitu au dhana ambazo hatuwezi kuviona hivyo si rahisi kujua jinsi kilivyo.

**d) Taswira** – Ni picha iliyomo kwenye akili ya mtumiaji wa lugha kuhusu kitu kinachotajwa. Unaposema kila mtu amchore Malaika, basi kila mtu atachora picha ya Malaika kwa kadiri ya mtazamo wake. Matinde (2012: 255) anasema taswira huweza kujengwa kutokana na uelewa wa mtu binafsi, mielekeo na imani yake, uzoefu alionao kuhusu vitu vilivyomo ulimwenguni kwa ujumla. Hata hivyo, kuna ugumu wa kujenga taswira ya sentensi kwa kuwa sentensi ni muunganiko wa maneno mengi. Pia maneno huweza kuwa na taswira tofauti mfano mbuzi, taa, kaa, paa, n.k.).

**e) Fahiwa** - Ni dhana inayotumika kuelezea mahusiano yaliyopo baina ya maneno yanayounda kikoa au kundi fulani la maneno yenye kuwakilisha maana fulani. Fahiwa zinazojulikana sana ni uhomonimia, usinonimia (usawe), upolisemia, uantonimia (unyume), n.k.

## Uhusiano na Umuhimu wa Semantiki na Pragmatiki

### a) Uhusiano

Zote zinachunguza maana katika viwango mbalimbali. Semantiki huchunguza maana ya msingi, wakati pragmatiki huchunguza maana kutegemeana na muktadha.

### b) Umuhimu wa Semantiki na Pragmatiki

Semantiki na pragmatiki zote zikiwa taaluma zinazochunguza maana zina umuhimu unaoweza kufanana na kutofautiana pia.

1) Semantiki ni kiini cha mawasiliano. Hii ina maana kwamba semantiki ni taaluma inayosaidia kurahisisha mawasiliano. Bila maana basi lugha haina maana au faida yoyote.

2) Semantiki ni kiini cha usahihi wa kisarufi katika nyanja mbalimbali za isimu. Kwa mfano,

(a) Baba mrefu anatembea barabarani.

(b) Mrefu barabarani anatembea baba.

3) Pragmatiki husaidia kutunza siri kwani mawasiliano hufanyika kati ya mtu na mtu bila kuwahusisha watu wengine hata kama watakuwa karibu na wazungumzaji.

## Viwango vya Maana

### a) Maana Katika Kiwango cha Neno

Maana katika kiwango cha neno hujitokeza zaidi kwenye uhusiano wa maneno (Uhusiano wa kifahiwa). Huu ni uhusiano wa maneno unaozungumzia maingiliano yaliyopo baina ya maneno. Uhusiano utakaoongelewa hapa ni wa sinonimia, antonimia, homonimia, polisimia na hiponimia.

**i) Sinonimia:** Ni uhusiano wa kileksika au kimsamiati ambapo maneno huwa na maumbo tofauti lakini maana zake ni sawa Habwe na Karanja (2004:208) wanaeleza mambo yafuatayo yanayosababisha kutokea kwa sinonimia:

- **Ukopaji wa msamiati:** Kukopa msamiati husababisha kutokea kwa sinonimia. Mfano, neno **'shati'** latika lugha ya Kiswahili limekopwa kutoka lugha ya Kiingereza **'shirt'**
- **Jinsi:** Sinonimu nyingine hutokana na visawe vinavyorejelea jinsi za kike na kume. Kwa mfano, hali ya kuwa na sura nzuri hurejelewa kwa kisawe cha "urembo" kwa wanawake na **"ujamali"** au **"umaridadi"** kwa wanaume.
- **Dini:** Dini tofauti huwa na maneno tofauti kuelezea dhana zinazolingana. Kwa mfano dhana inayorejelea mahala pa kuabudia kwa waisilamu huitwa **msikitini**, na kwa Wakristo ni **kanisani**.
- **Tofauti za kimaeneo**: Wazungumzaji wa lugha moja wanapoishi katika maeneno tofauti, lugha zao pia hutofautiana kimuundo na kimsamiati ili kukidhi mahitaji ya mazingira yao. Baadhi ya matamshi ya msamiati hubadilika na msamiati mpya

huzuka. Kwa mfano, aina ya usafiri wa gari ndogo, **daladala** (Dar es Salaam), **vifodi** (Arusha).

- **Tofauti za kilahaja**: Dhana moja huweza kutajwa kwa maneno yenye matamshi tofauti. Kwa mfano eneo ambalo watu huenda kuchota maji kwa Kiswahili cha Tanzania Bara huitwa **bombani** lakini kwa Kiswahili cha Zanzibar hujulikana kama **mferejini**.
- **Taaluma:** Visawe vya kitaaluma huitwa istilahi. Mfano wa sinonimu za aina hii ni **aya** katika riwaya na **ubeti** katika ushairi vinavyorejelea kitengo katika mfululizo wa maandishi**.**
- **Wakati:** Baadhi ya sinonimu za lugha huzuka kutokana na mabadiliko ya kihistoria. Kwa mfano, kwa mfano, **mnyonyaji → mlanguzi→ fisadi**.
- **Utaalamu au urasmi:** Urasmi pia husababisha kutokea kwa usinonimia. Mfano, hatusemi Waziri wa Hela bali Waziri wa Fedha.
- **Utamaduni:** kuzingatia maadili na miiko katika jamii. mfano, msalani, maliwato, (chooni).

Mpendwa mwanafunzi, yatupasa kujua kuwa hakuna usinonimia wa asilimia mia moja. Usinonimia unategemea muktadha. Maneno yanayokaribiana maana yanaweza kutumika pamoja katika muktadha fulani lakini jambo hilo lisiwezekane kabisa katika muktadha mwingine.

**ii) Antonimia**

Ni uhusiano wa neno moja kuwa na maana ya kinyume na neno jingine. Yaani, maana zinazopingana. Kuna unyume wa aina tofauti. Matinde (2012:264-266) akitumia dhana ya unyume, anabainisha aina zifuatazo za antonimia:

***Antonimia za utoano***

Ni aina ya unyume ambao upo katika jozi. Kwa mfano: ajuza - shaibu, baba - mama, kijana - mzee, simama - kaa, mwalimu - mwanafunzi, tabibu - mgonjwa, n.k.

*Antonimia za vidato*

Ni vinyume vinavyorejelea uhusiano wa maneno kwa kukadiria. Kwa mfano: moto - baridi, ujana - uzee, nyingi - chache, mrefu - mfupi, n.k.

*Antonimia za uelekeo*

Ni unyume wenye kuonesha uelekeo wa upande tofauti. Kwa mfano katika Kiswahili: mashariki - magharibi, mbele - nyuma, nenda - rudi, n.k. Au katika Kiingereza: up - down, n.k.

*Antonimia za utenduzi*

Ni unyume unaohusisha kutengua jambo lililotajwa awali. Kwa mfano, funga - fungua, panga - pangua, ezeka - ezua, anika - anua, n.k.

**iii) Homonimia**

Huu ni uhusiano wa maneno mawili au zaidi kuwa na maumbo sawa lakini hutofautiana kimaana. Maneno hayo huwa hayahusiani kabisa. Hata kwenye kamusi huingizwa kama vidahizo tofauti. Hii ina maana kuwa kila homonimu huwa ni neno kuu linalojitegemea. Kwa mfano neno *"ada"* (TUKI, 2013: 2):

ada$^{1}$ nm kanuni, mila, au desturi

ada$^{2}$ nm malipo yanayotolewa ili kupata huduma k.v. elimu, uanachama au tiba

**iv) Polisemia**

Kwa mujibu wa Habwe na Karanja (2004:213) "polisemia ni hali ya neno huwa na maana zaidi ya moja". Katika polisemia maneno huwa yana uhusiano wa kihistoria. Huu ni uhusiano unaohusu umbo moja la neno kuwa na maana mbalimbali. Mfano,

Mguu (a) -wa binaadamu


(b) -wa gari

Kwenye kamusi maana hizi hubainishwa kwa namba zilizopangwa kiulalo na kukolezwa wino. Kwa mfano; **mdomo$^{1}$** nm **1**... **2** ...

Mara nyingi, neno moja kuwa na maana nyingi hutokea kwa sababu kunakuwa na sifa fulani ya ufanano katika vitajwa viwili. Kwa mfano, kuna uhusiano kati ya mguu wa mtu na mguu wa gari, kwa kuwa kazi ya mguu ni kusimamia na kutembelea.

### v) Uhiponimia

Hiponimia ni neno ambalo maana yake imejumuishwa katika maana ya neno jingine. Hivyo, uhiponimia ni ni uhusiano wa maana ya neno kujumuishwa katika maana ya neno jingine. Neno lenye maana kubwa huitwa *maana jumuishi* na maneno yenye maana ndogo huitwa *hiponimu*. Kwa mfano neno, Kwa mfano, **Wanyama:** ni **hiponimu kuu** (maana jumuishi) na aina mbali mbali za wanyama huwa **hiponimu nyenza**. Uhusiano huu unaweza kuoneshwa katika mchoro kama ifuatavyo:




### vi) Umeronimia

Huu ni uhusiano wa kitu kizima na vijenzi vyake. Kwa mfano:

**Nyumba:** *Mlango, kuta, dirisha, paa, n.k.*

**Darasa:** *Mwalimu, wanafunzi, kalamu, daftari, ubao, chaki.*

### vii) Monosemia

Huu ni uhusiano wa neno moja kuwa na maana moja isiyo na utata. Hata hivyo, maneno haya ni machache sana. Kwa mfano, unapotaja neno mke au mume huwa unarejelea dhana moja tu. Mke = mwanamke aliyeolewa au mume = mwanaume aliyeoa. Au ukitaja rangi nyeusi hakuna atakayeonesha rangi hiyo kwa kuitaja nyeupe, n.k.

### b) Maana Katika Kiwango cha Sentensi

Ni uhusiano unaojitokeza kati ya neno moja na mengine katika sentensi. Maana katika ngazi ya sentensi huzingatia mahusiano yafuatayo:

**i) Usawe**

Ni uhusiano wa kimaana baina ya sentensi mbili au zaidi ambapo sentensi hizo huwa na maana moja ya msingi. Kwa mfano;

1) *Watoto wanacheza **barabarani***, 2) *Watoto wanacheza **njiani***

**ii) Utata**

Ni hali ambapo sentensi moja huwa na maana zaidi ya moja au huweza kueleweka kwa namna zaidi ya moja. Utata huu unaweza kuwa wa kileksika (kimaana) au kimuundo (Hutokana na mpangilio wa maneno). Kwa mfano, ***Tumeshindia chai.***

**iii) Ukinzani**

Huu ni uhusiano wa mtu au kitu kupewa sifa tofauti na mtu au kitu hicho kilivyo. Mara nyingi ukinzani huu huwa na sababu maalumu hususani kwenye kazi za kifasihi. Kwa mfano,

*Miti yote ilimchekea kwa upendo.*

**iv) Upotoo/ Anomali**

Ni uhusiano wa kimantiki unaotokea pindi dhana mbili zinapopotoshwa katika kuelezea jambo fulani. Kwa mfano: ***Kaka yake amejifungua*** (Mwanaume hawezi kubeba ujauzito hivyo dhana ya mwanaume kujifungua ni upotoo/upotoshi).

## Aina za Maana

Kimsingi kuna aina kuu mbili za maana ; **maana ya msingi** na **maana ya ziada**. Maana ya msingi ni ufafanuzi unaooneshwa kwenye kamusi kwa kuhusisha maneno ya kategoria mbalimbali. Lakini maana ya ziada inategemeana na matumizi ya neno kulingana na hisia za mtu katika muktadha fulani. Hata hivyo, **G. Leech** (1974) anabainisha aina saba za maana kama ifuatavyo :

### a) Maana ya Msingi

Maan aya msingi *(conceptual meaning)* ni ile maana halisi ya neno. Maana hii pia hujulikana kama maana ya kikamusi. **Kwa mfano, Bibi ni mama wa baba au mama**. Maneno ya msingi huweza kutofautiana kimuundo au kwa sifa bainifu (hukinzana) kwa kuwa kila neno lina sifa inayolitofautisha na neno jingine. Kwa mfano mama na baba hutofautiana katika sifa zifuatazo: **Mama** *{+Binadamu, +Mtu mzima, +Mwanamke,-Mwanaume}* na **Baba** *{+Binadamu, +Mtu mzima, +Mwanaume, - Mwanamke}*. Alama

ya (+) hutumika kuonyesha neno kuwa na sifa fulani na (–) huonyesha neno hilo halina sifa hiyo.

### b) Maana ya Ziada/Maana ya Kimatlaba/Ashirifu

Maana ya ziada *(Connotative Meaning)* hutokana na maana ya msingi ambapo neno hupewa maana ya ziada kwa kulihusisha na maana ya msingi. Kwa mfano; **Kupe.** Maana ya msingi ya neno **kupe** ni mdudu anayenyonya damu. Maana ya ziada ya kupe ni mnyonyaji. Maana ya pili imetokana na **maana ya msingi** yaani "mdudu anayenyonya damu".

### c) Maana ya Kimtindo

Maana ya kimtindo *(Stylistic Meaning)* ni maana inayotokana na matumizi ya lugha kulingana na mazingira halisi ya wakati wa mazungumzo. Kinachozingatiwa zaidi ni nani anazungumza na nani? Wanazungumza nini? (Mada) kwa namna/ njia ipi? (Maandishi/ mazungumzo, ana kwa ana/simu, muhadhara/ mjadala), wako katika hali gani? (Furaha, ugomvi, utani n.k), wakati gani? n.k. Ni katika mazingira gani unaweza kutumia neno fulani. Maana hii hujitokeza katika rejista mbalimbali kama vile *kanisani, msikitini, hotelini, sokoni*, n.k. Kwa mfano,

**Mhudumu:** "Nani wali ng'ombe?"

**Mteja:** "Mimi hapa."

### d) Maana Akisi/ Mwangwi

Maana akisi *(Reflective Meaning)* ni maana inayopewa kitu au mtu kwa kufananisha na kitu au mtu mwingine. (tafuta mifano).

### e) Maana Dhamirifu

Maana dhamirifu *(Thematic Meaning)* ni maana yenye kuonesha umuhimu wa jambo. Mara nyingi maana hii huwekwa mwanzoni mwa sentensi ili kuonesha umuhimu wake kutegemeana na malengo ya mtu.

"Kaka, **samaki wako** wameliwa na mbwa"

"Kaka, **mbwa** amekula samaki wako."

Sentensi hizi mbili zinaonesha kuwa, maneno yaleyale yaliyomo ndani mwake yakipangwa kwa namna tofauti yanaweza kuleta maana tofauti. Katika sentensi ya kwanza msisitizo upo kwenye

**samaki** (kitendwa), lakini katika sentensi ya pili umuhimu umewekwa kwenye **mbwa** (mtenda).

### f) Maana Hisia

Maana hisia *(Affective Meaning)* ni maana inayotokana na mtazamo chanya au hasi alionao mzungumzaji au mwandishi juu ya jambo au kitu. Hata hivyo, uteuzi wa neno litakalotumika unategemea na maana ambayo mtumiaji wa lugha anataka hadhira yake waipate. Nahau nyingi zinaingia katika aina hii ya maana. Kwa mfano;

**Rushwa** inaweza kupewa sifa nzuri kwa kuitwa takrima zawadi, au kuwa na maana ya jambo baya sana ambayo hutambulika kama hongo au mlungura.

### g) Maana/Tangamano/ Endefu

Maana tangamano *(Collocative Meaning)* ni maana ambayo hupatikana kwa kuangalia jinsi maneno yanavyofuatana au kuambatana kuchaguana kwa utaratibu maalumu. Kwa mfano;

*-Msichana mrembo anatembea kwa madaha (na sio msichana mtanashati)*

*-Mvulana huyu ni mtanashati (na sio mvulana mrembo)*


## Nadharia za Maana

Ipo mitazamo mbalimbali inayoelezea dhana ya maana

### a) Nadharia ya Maana kama Kitajwa au Kirejelewa

Nadharia hii pia hujulikana kama nadharia ya urejeleo ambayo iliasisiwa na Ogden na Richard (taz. Lyons, 1981). Nadharia hii huielezea maana kwa kuhusisha umbo la kitu linaloonekana. Ni maana inayoelezea kitu halisi kinachowakilishwa na neno. Ina maana kwamba unapotaja kitu basi ni lazima kiwepo kitu halisi kinachoonekana kama vile **"mbuzi", "chungwa", "mti", n.k.**

Waasisi wa nadharia hii waliibuka na dhana ya embe tatu ili kuelezea nadharia yao kama ilivyotafsiriwa hapa chini:




**Udhaifu**

- Baadhi ya maneno huwa na maana zaidi ya moja (kama neno mbuzi: mnyama, kifaa cha kukunia nazi), hivyo, mtu huenda asielewe kinachorejelewa ni kipi.
- Baadhi ya maneno huwa hayana virejelewa. Kwa mfano viunganishi na, au ambayo hutumika tu katika mawasiliano

## b) Nadharia ya Maana Kama Dhana/ Taswira

Haya ni mawazo yanayohusishwa na neno linalotajwa. Ni ile hisia au picha unayoipata au unayoijenga kichwani baada ya kusikia au kusoma neno au jambo fulani. Kwa mfano, watu watatu tofauti wakisikia neno 'nyumba' kila mmoja atajenga taswira tofauti kichwani mwake kulingana na mazingira na uzoefu wake. Taswira zinazoweza kujengwa kuhusu nyumba (ya tembe, ghorofa, udongo, miti, bati, n.k.). Hii husababisha maana ya maana za maneno kuwa telezi.

**Udhaifu**

- Neno huweza kuwa na maana nyingi kwa kuwa watumiaji wa lugha huweza kuwa na mawazo tofauti kuhusu neno moja linalotajwa.

## c) Nadharia ya Maana kama Mwitikio wa Msikilizaji

Nadharia hii inachambua maana kwa kuhusisha na jinsi mtu anavyoweza kulitafsiri neno alilolisikia. Leonard Bloomfield na Charles Morris wanasema kwamba maana ya neno ni ile hisia itakayoibuliwa na msikilizaji baada ya kusikia kitajwa au neno linalotajwa. Hivyo, nadharia hii huchukulia kuwa maana ni kichocheo cha msemaji na mwitikio wa msikilizaji. Hii ina maana kuwa ili neno liwe na maana basi ni lazima pawepo na msemaji na msikilizaji. Wanasaikolojia Skinner na Watson wao wanadai kuwa maana ya neno au dhana hufafanuliwa katika hatua tatu:

**kichocheo --------- Tamko ----------mwitikio wa msikilizaji**

Panya leta gongo mwingine atakimbia na mwingine atakimbilia lakini mwingine atakimbia (tamaduni zinatofautiana)

**Udhaifu**

- Binadamu tunatofautiana kiutamaduni, hivyo miitikio nayo ni tofauti. Kichocheo kimoja kinaweza kusababisha utokeaji wa viitikio viwili au zaidi tofauti.
- Si katika mazingira yote au wakati wote msikilizaji anaweza kuwa karibu na msemaji.

## d) Nadharia ya Maana Kama Matumizi

Hii ni nadharia inayoelezea maana kwa kuangalia jinsi neno linavyotumika katika jamii. Nadharia hii inaelezwa na mwanafalsafa Ludwing Wittegenstain katika miaka ya 1930. Yeye anaeleza kuwa maana ya neno lazima ipatikane kulingana na muktadha wa matumizi ya hilo neno. Kwa mfano, muktadha wa kidini, shuleni, sokoni, n.k. ambako neno pamoja na sentensi hutumika kwa kiasi kikubwa.

**Udhaifu**

- Jamii hutofautiana, hivyo neno huweza kuwa na maana katika jamii hii lakini likakosa maana katika jamii nyingine.

## e) Nadharia za Masharti ya Ukweli za Maana

Matinde anasema, maana ni ukweli wa kinachosemwa. Hata historia ya mambo yaliyotokea katika jamii, nchi au duniani. Inaweza kuwa miaka ya kuanzishwa jambo fulani, kuzaliwa kwa mtu n.k.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, natumai umejifunza vipengele vya somo hili kwa ufanisi na kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili. Kabla ya kuendelea na somo linalofuata, fanya tafakuri kwa kujibu maswali yafuatayo:

1. Unaweza kuzitofautishaje aina za maana?

2. Nadharia zipi zinatumika kuelezea maana?

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Tofautisha dhana za semantiki na pragmatiki.
2. Chambua nadharia zinazoelezea dhana ya "maana".
3. Fafanua uhusiano wa kifahiwa ufuatao:
    a) Polisemia
    b) Homonimia
    c) Antonimia
    d) Sinonimia
4. Eleza uhusiano wa maneno katika ngazi ya sentensi.

# Somo la Nane

## Kutumia Lugha ya Kiswahili katika Miktadha Mbalimbali

### Utangulizi

Mpendwa mwanafunzi, katika somo lililopita tulijifunza kutumia semantiki na pragmatiki. Tulifafanua dhana za semantiki na pragmatiki, kuwa semantiki ni taaluma ya isimu inayochunguza maana katika viwango mbalimbali, na pragmatiki ni taaluma ya isimu inayochunguza maana kimuktadha. Katika somo hili, tutajifunza matumizi ya lugha ya mazungumzo na maandishi katika mawasiliano. Katika kufanikisha somo hili, **tutafafanua maana ya lugha ya mazungumzo na maandishi.** Pia, **tutafafanua stadi zinazohusika katika lugha ya mazungumzo na maandishi,** pamoja na **kuchambua mada zinazohusika nazo.** Mwisho, **tutafafanua alama zinazotumika katika uandishi.** Tunaamini kuwa baada ya kujifunza somo hili, utaweza kuyafikia matokeo mahususi ya kujifunza yaliyokusudiwa katika somo hili.

## Matokeo

Baada ya kukamilisha somo hili utaweza:

- Kufafanua dhana ya lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi;
- Kufafanua stadi za lugha ya mazungumzo na maandishi;
- Kuchambua mada za lugha ya mazungumzo na maandishi; na
- Kufafanua alama za uandishi.

### Dhana za Lugha ya Mazungumzo na Maandishii

Mpendwa mwanafunzi, mwanzoni mwa moduli hii tulielezwa kwamba, lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa na binadamu katika jamii kwa lengo la kufikisha ujumbe kwa binadamu mwingine. Zipo njia nyingi zinazoweza kutumiwa na mtu ili kufikisha ujumbe wake kwa mlengwa. Kwa muktadha wa moduli hii, tutajifunza njia ya **lugha**. Wataalamu wa mawasiliano wanaigawa lugha katika pande kuu mbili; **lugha ya mazungumzo** au **lugha ya maandishi**.

### a) Maana ya Lugha ya Mazungumzo

Lugha ya mazugumzo ni maongezi ya watu wawili au zaidi bila kutumia maandishi. Lugha hii ya mazungumzo ilianza punde tu binadamu alipoanza kukabiliana na mazingira yake. Ndio kusema, hii ni lugha kongwe zaidi ya lugha ya maandishi. Lugha hii, hutumia maneno yaliyo rasmi au yasiyo rasmi kutegemeana na wahusika wa mazungumzo, jambo linaloongelewa, n.k. Wakati wa kuzungumza mtu huweza kupandisha au kushusha sauti anasema sentensi swali au mshangao, n.k.; na pengine kuchezesha viungo vya mwili.

Kuna aina mbalimbali za lugha za mazungumzo kwa kuzingatia:

(i) Mazingira rasmi

(ii) Mazingira yasiyo rasmi,

(iii) Utambulisho wa kijamii kama vile: matabaka, hadhi yake.

(iv) Utambulisho wa kimuktadha, kwa mfano; lugha ya siri na yenye mipaka, kucheza na maneno, miviga.

#### i) Lugha ya Mazungumzo Katika Mazingira Rasmi

Mazingira rasmi ni yale ambayo hutumia lugha rasmi ambayo ni lugha iliyosanifiwa na kukubalika itumike katika shughuli za serikali, bunge, mahakamani, kwenye elimu n.k. (Msanjila na wenzake, 2009). Lugha rasmi imeandikwa kwenye vitabu vya taaluma mbalimbali, kamusi. Lugha hii ina istilahi za kutosha zinazowezesha jamii kuitumia kwenye mawasiliano mapana. Kwa mfano, nchini Tanzania lugha zinazotumika kwenye mazingira rasmi ni Kiingereza na Kiswahili. Katika lugha rasmi tunapata aina mbili za lugha ya mazungumzo ambazo ni *jagoni* na *rejesta*.

***Jagoni****:* Ni aina ya lugha inayotumika katika taaluma fulani. Lugha hii hufahamika na watu wa taaluma hiyo au wenye maarifa kuhusu taaluma hiyo. Taaluma kama vile isimu, sayansi, uhandisi, n.k. Mathalan, katika isimu kuna istilahi kama fonolojia, mofolojia, n.k.

***Rejesta****:* Habwe na Karanja (2004) wanafasili rejesta kama mtindo wa lugha kutegemeana na kazi au shughuli. Katika muktadha rasmi rejesta hurejelea upande mmoja kama vile, msamiati wa kiufundi na matumizi ya lugha fasaha. Kuna rejesta za hospitalini, mahakamani, uhasibu, elimu, n.k. Mfano wa rejesta za hospitalini:

**2 x 3 x 3/7** ikiwa na maana ya **meza vidonge viwili kwa siku kwa siku tatu kati ya saba za juma**.

**ii) Lugha ya Mazungumzo Katika Mazingira Yasiyo Rasmi**

Hii ni lugha ambayo hutumia msamiati ambao si rasmi. Kwa kawaida lugha ya mazungumzo katika mazingira yasio rasmi huwa si sanifu. Katika mazingira haya tunapata aina zifuatazo za lugha ya mazungumzo: *misimu*, *agoti*, *rejesta* na *lahaja*.

***Misimu****:* Ni aina ya misemo katika lugha ambayo huzuka na kutoweka. Wakati mwingine, misimu huweza kudumu na kuwa sehemu ya lugha. Mfano neno daladala ambalo kwa sasa ni aina fulani ya magari ya usafiri hususani Dar es Salaam, nchini Tanzania; katika miaka ya sabini lilimaanisha *kiasi cha nauli inayolipwa na abiria*. Misimu hutofautiana kulingana na eneo la mazungumzo na kundi la watu.

***Agoti****:* Ni lugha inayotumiwa na kundi dogo la watu katika mazingira yasiyo rasmi kwa lengo la kuficha maovu yao ili yasifahamike katika jamii wanamoishi. Mfano, watumiaji wa madawa ya kulevya hutumia neno *"sembe"* likiwa na maana ya *madawa ya kulevya*.

***Rejesta****:* Ni mazungumzo katika mazingira yasiyo rasmi ambayo hutumia msamiati usio rasmi, matumizi ya misimu na ukatizaji wa maneno pamoja na udondoshaji wa baadhi fonimu. Kuna rejesta za vijiweni, sokoni, n.k. Mfano, kwenye daladala kondakta humwambia dereva *"nyoosha mguu"* akiwa na maana *aendeshe kwa kasi*.

***Lahaja:*** Kwa mujibu wa Massamba (2016: 63), hii ni lugha mojawapo kati ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lugha moja isipokuwa zinatofautiana katika *lafudhi* au *msamiati usiokuwa wa msingi*.

## b) Maana ya Lugha ya Maandishi

Hii ni njia inayotumia maandishi katika kufikisha ujumbe kwa jamii. Kwa kawaida lugha ya maandishi huhusisha mtu mmoja au kikundi kutegemana na jambo linaloandikwa. Mara nyingi lugha hii, hutumia maneno yaliyo rasmi. Tofauti na lugha ya mazungumzo, lugha ya maandishi huhusisha matumizi ya alama za uandishi. Alama hizo ni kama vile herufi kubwa, kituo kikuu, mkato, funga na fungua semi, n.k.

## Stadi za Lugha ya Mazungumzo na Maandishi

Stadi ni ujuzi wa kuweza kufanya jambo. Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013:63) stadi za lugha ni maarifa au ujuzi unaotumiwa na watu katika kuwasiliana kwa kutumia lugha. Wanaendelea kusema kuwa, kuna stadi nne kuu za lugha ambazo ni kusikiliza, kuongea (kuzungumza), kusoma na kuandika; na kwamba kila stadi ina nafasi yake maalum katika mchakato wa mawasiliano lugha.

### a) Stadi za Lugha ya Mazungumzo

*Stadi ya mazungumzo ni ujuzi wa mtu katika kujieleza kwa mdomo.* Lugha ya mazungumzo ina stadi kuu mbili: **kusikiliza** na **kuzungumza/ kuongea**.

### b) Stadi za Lugha ya Maandishi

*Stadi katika lugha ya maandishi huweza kuelezwa kama ujuzi wa mtu katika kujieleza kwa kuandika.* Lugha ya maandishi basi, ina stadi kuu mbili. Stadi hizo ni **kusoma** na **kuandika.**

## Mada za Lugha ya Mazungumzo na Lugha ya Maandishi

### a) Mada za Lugha ya Maazungumzo

Mpendwa mwanachuo, hapa tunazungumzia mada za mazungumzo rasmi. Mada za lugha ya mazungumzo ziko nyingi. Baadhi ya mada hizo ni *hotuba, risala, n.k.*

**i) Hotuba**

Hotuba ni taarifa inayosomwa mbele za watu kwa ajili ya kuwafahamisha jambo fulani. Mtu anayesoma hotuba lazima achague maneno rasmi na yenye kubeba ukweli wa jambo analozungumza.

**Mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba**

**Kabla ya Hotuba**

- Soma vyanzo mbalimbali vinavyoelezea jambo unalotaka kulitoa kwa jamii kwa njia ya hotuba. Tambua watu watakaohusika kukusikiliza (zingatia utamaduni wao), n.k.

- Andaa muhtasari wa hotuba. Muhtasari huu utasaidia kufanya tathmini na kurekebisha jambo kabla hujalifikisha kwa watu.
- Bainisha njia utakayotumia kuhutubia. Kwa mfano, kukariri hotuba au utasoma moja kwa moja.
- Fanya mazoezi ya kuongea bila kuhusisha watu ili kupata uzoefu na kuondoa hofu.

**Wakati wa Hotuba**

Kwa kawaida hotuba ina vipengele vikuu vitatu: Utangulizi, kiini cha hotuba, na hitimisho

***Utangulizi*** **-** Hii ni sehemu ya mwanzo ya hotuba. Mara nyingi hotuba huanza na kumshukuru Mungu kwa kutujalia uhai. Katika sehemu hii pia, mtoa hotuba hutambulisha lengo la hotuba hiyo kwa ufupi. Pia, huwa na hadithi fupi yenye kuhusisha jambo linalozunumzwa.

***Kiini*** **-** Sehemu hii hubeba hotuba nzima. Inapendekezwa iwe na hoja kuu nne. Hoja hizo huchukua asilimia kubwa ya hotuba. Hoja za kwenye hotuba ni vema zipangwe kwa mtiririko unaoeleweka, kuanzia hoja rahisi hadi hoja ngumu. Wakati wa kusoma hotuba, lazima msomaji afafanue kwa kina hoja moja baada ya nyingine kwa kuonesha.

***Hitimisho*** **-** Sehemu hii huhusisha utoaji wa muhtasari yale yaliyosomwa mbele ya hadhara. Pamoja na hilo, mtoa hotuba huwaasa washiriki kuzingatia waliyoambiwa.

## b) Mada za Lugha ya Maandishi

Mada za lugha ya maandishi ni nyingi. Baadhi ya mada hizo ni *uandishi wa barua, uandishi wa tawasifu, uandishi wa kumbukumbu za mikutano au vikao, ratiba, uandishi wa kadi*.

**i) Barua**

Barua ni aina ya nyaraka ambazo huandikwa na kupelekwa kwa walengwa kwa lengo la kuwasiliana kimaandishi.

**Aina za Barua**

**a) Barua za kirafiki** - Ni nyaraka ambazo huandikwa na mtu na kutumwa au kupelekwa kwa ndugu, rafiki, wazazi au walezi kwa

lengo la kusalimiana au kueleza jambo binafsi. Barua za kirafiki huwa na sifa zifuatazo:

i) Huandikwa kwa ndugu, wazazi, jamaa, marafiki, n.k.

ii) Huwa na anwani moja upande wa kulia.

iii) Utangulizi huwa na salamu za maamkizi.

iv) Jina la mwandishi huandikwa mwisho wa barua

**b) Barua rasmi** - Ni nyaraka ambazo huandikwa na mtu na kutoa mwaliko, kuomba kazi, kutoa maoni, kutoa malalamiko, kushukuru, n.k.

**ii) Tawasifu**

Kwa mujibu wa Wanjala na Kavoi (2013: 123), tawasifu ni maelezo ya jumla ya mtu na ambayo huandikwa na mhusika mwenyewe. Tawasifu huandikwa kwa ajili ya kuweka kumbukumbu ya taarifa binafsi. Huonesha kwa ufupi kuhusu historia ya mtu wakati wa kuomba kazi, n.k.

**Sehemu Kuu za Tawasifu**

Tawasifu ina sehemu kuu saba (maelezo kwenye mabano ni yangu).

a) ***Maelezo binafsi*** - kuonesha majina, jinsi (kama ni kike au kiume, tarehe ya kuzaliwa, dini (sio muhimu sana), hali ya ndoa (kama ameoa au kuolewa), lugha anayozungumza (hususani lugha rasmi kama vile Kiswahili, Kiingereza, Kiarabu, n.k.), anwani (sanduku la barua na mahali lilipo) pamoja na namba ya simu na barua pepe.

b) ***Elimu*** - huonesha shule na vyuo alivyosomea tangu elimu ya msingi; kwa kuzingatia miaka na mahali vilipo.

c) ***Majukumu*** - huonesha kazi alizofanya kazi iwe ya kudumu au kujitolea. Hapa pia huandika taasisi alizozifanyia kazi kwa mfuatano wa miezi au miaka. Hii itasaidia kuonesha uzoefu alionao kuhusu kazi au nafasi ya kazi anayoomba.

d) ***Mafanikio*** - Huonesha mafanikio aliyopata katika majukumu aliyofanya. Kwa mfano, kuhudhuria makongamano ya kitaifa na kimataifa katika sehemu mbalimbali duniani.

e) ***Matarajio*** - Unatarajia uwe mtu mwenye ujuzi gani katika maisha yako ya kazi. Kwa mfano, kuwa mwalimu bora wa lugha ya Kiswahili.

f) ***Mapendeleo*** - Hueleza jambo unalopenda kufanya katika muda wako wa ziada mfano unapomaliza majukumu yako ya kikazi. kwa mfano, kusoma vitabu, kucheza mpira wa miguu/ pete, n.k.

g) ***Wadhamini*** - Ni watu wanaokufahamu vizuri, ambao wataweza kueleza zaidi sifa ulizonazo endapo wanaotaka kukuajiri watapenda kukufahamu. Utaandika jina lake, cheo alichonacho, anwani yake pamoja na namba ya simu. Kwa mfano:

PROF./ DKT...

Mkuu wa Chuo/ Shule ya...

S. L. P...

Dodoma.

**iii) Kumbukumbu za Mikutano**

Kumbukumbu za mikutano ni muhtasari wa majadiliano na makubaliano yaliyofikiwa katika kikao rasmi. Kumbukumbu hizo huandaliwa na katibu wa kikundi au ofisi inayohusika.

**Aina za Mikutano/ Vikao**

***a) Mkutano rasmi:*** Huu ni mwito au mkusanyiko wa kawaida uliowekwa kwenye kalenda ya ofisi, taasisi au kikundi. Wajumbe huelezwa tarehe ya mkutano unaofuata. Mkutano au kikao rasmi huweza kuwa cha kwanza, cha pili na kuendelea.

**Vipengele vya Kumbukumbu za Mikutano**

**Kichwa cha habari** - huanza na neno kumbukumbu za... au muhtasari wa... ambapo ndani yake huelezwa jina la kikundi kilichofanya kikao, mahali kikao kilipofanyika, tarehe pamoja na muda/ saa. Kwa mfano:

**a) Mahudhurio -** Hii ni orodha ya washiriki wote wa kikao. Huwa na sehemu tatu: (a) Waliohudhuria, (b) Wasiohudhuria (i) kwa udhuru (ii) bila udhuru, (c) Waalikwa

**b) Ajenda -** Ni masuala yaliyojadiliwa katika kikao. Kwa kawaida ajenda huandaliwa na kusambazwa kabla ya kikao ili

wajumbe wapitie mapema. Lakini, kama ni kikao cha dharura, ajenda husemwa wakati wa kikao husika. Ajenda hizo hupangwa kwa mtiririko ufuatao: Kufungua kikao, kupitia kumbukumbu za kikao kilichopita ili kuzithibitisha au kuzirekebisha, Yatokanayo (mambo yaliyojadiliwa katika kikao cha kwanza, na ambayo yalihitaji utekelezaji. Huletwa kwenye kikao cha pili/tatu, n.k.), Ajenda mpya (mambo yanayohitajika katika kikao husika), Mengineyo, kufunga kikao.

c) **Hitimisho -** Ni sehemu ya Mwenyekiti na Katibu kuweka sahihi zao.

**Mambo ya Msingi katika Uandishi wa Kumbukumbu za Mikutano Rasmi:**

***Kabla ya Mkutano:*** Toa taarifa kwa watu watakaohusika katika mkutano kuhusu ***siku***, ***mahali***, na ***muda*** wa mkutano kwa kubandika matangazo kwenye mbao za matangazo, kwa njia ya simu, na hata vyombo vya habari endapo mkutano utawahusisha watu kutoka sehemu tofauti. Pia, andaa ajenda za kujadiliwa kwenye kikao.

***Wakati wa Mkutano/Kikao:*** Kama Mwandishi, pitisha karatasi ya mahudhurio ili kila aliyeshiriki ajjiorodheshe. Kisha, mwongoze Mwenyekiti kuendesha mkutano kwa kumsomea ajenda zilizoandaliwa, moja baada ya nyingine ili zijadiliwe na wajumbe. Pia, kumbuka kuandika mambo muhimu yatakayojadiliwa ili kuweka kumbukumbu kwa siku za baadaye.

***Baada ya Mkutano/ Kikao:*** Andaa vizuri kumbukumbu za mkutano na kuzihifadhi kwa ajili ya kusomwa kwenye mkutano/ kikao kitakachofuata.

***b) Mkutano usio rasmi:*** Huu ni mwito au mkusanyiko wa dharura ambao kwa kawaida hauna maandalizi ya ajenda.

**Faida za Kumbukumbu za Mikutano/ Vikao**

- Ni kumbukumbu ya mipango ya ofisi, taasisi au kikundi inayohitaji ufuatiliaji.

- Hutunza kumbukumbu ya maafikiano katika mkutano kwa faida ya wanajamii husika
- Hubainisha mtu au kikundi kilichopewa kazi ya kufuatilia.
- Husaidia mtu ambaye hakuwepo kujua kilichojadiliwa kwenye mkutano.

## Alama za Uandishi

Uandishi bora hupimwa kwa matumizi sahihi ya alama za uandishi (pia hujulikana kama **alama za uakifishaji**). Wanjala na Kavoi (2013: 128) wanasema, matumizi ya alama za uakifishaji huwa na lengo la kufikisha ujumbe uliokusudiwa. Alama hizo ni kama zifuatazo:

***a) Alama za Mtajo au Alama za Usemi (“na” au ‘na’):*** Alama hizi huwa na maana sawa ila tofauti iko kwenye asili ambapo **“na”** zina asili ya Marekani na **‘na’** asili yake ni Uingereza. Mbunda (1992: 64) anasema kuwa matumizi ya alama za mtajo huambatana pia na alama za vituo ili kumsaidia msomaji anayesoma. Wanjala na Kavoi wanasema, alama hizi hutumika kutenga maneno yaliyosemwa na mtu mwingine. Mfano,

*Waziri Mkuu aliagiza: “ ”*

Aidha, hutumiwa kufungia vichwa vya hadithi, makala, mashairi mafupi, vipindi vya runinga pamoja na dondoo fupi kama vile nahau, misemo au katika sentensi. Mfano: *Hadithi yenye kichwa cha habari, “ ”*

***b) Nukta (.):*** Hiki ni kituo kinachoonesha mwisho wa sentensi ambayo kwa kawaida hubeba wazo kuu. Kwa mfano;

*Wanafunzi wa kisomo wamemaliza mafunzo yao.*

***c) Mkato ( , ):*** Hii ni alama inayotumika kuonesha kituo kidogo wakati wa kusoma, au kutenganisha maneno yaliyoorodheshwa. Kwa mfano;

*Alikwenda kununua matunda, mchele, sukari na chumvi.*

***d) Nukta Mbili/ Nukta Pacha (:):*** Alama hii hutumika kutenga sentensi mbili iwapo ile ya pili hufafanua jambo lililoelezwa katika sentensi ya kwanza (Wanjala na Kavoi, 2013:129). Pia, hutumika kuonesha mazungumzo kati ya watu wawili au zaidi yaliyo kwenye maandishi. Kwa mfano;

***Mwalimu:*** *“Hamjambo wanafunzi?”*

***Wanafunzi:*** *"Hatujambo, shikamoo mwalimu."*

***Mwalimu:*** *"Marahaba!"*

***e) Nukta-mkato/ koma (;)***: lama hii hutumika kutenga maelezo yaliyofuatana ili kutofautisha maelezo madogo na makuu. Mfano,

| |
|---|
| *Ndugu Mgeni Rasmi (Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima); Naibu Mkurugenzi Taaluma na Ushauri; Naibu Mkurugenzi Fedha, Mipango na Utawala; Wakuu wa Idara; ...* |

Pia, hutumika kuunganisha sentensi mbili zenye uzito sawa wa mawazo. Mfano, *Nimemaliza kusahihisha kazi za wanafunzi wangu; napaswa kutoa matokeo yao.*

Vilevile, hutumika kuunganisha vishazi vikuu ambavyo havijaunganisha na viunganishi. Mfano, *Wingu jeusi limetanda anga nzima; punde kutanyesha mvua kubwa. 131)*

***f) Alama ya kuuliza (?):*** Alama hii hutumika kuonesha sentensi yenye maulizo. Kwa maana kwamba sentensi hiyo huhitaji jibu au majibu. Kwa mfano; ***Kwa nini ulitoroka?***

***g) Alama ya kushangaa (!):*** Alama hii Hutumiwa mwishoni mwa sentensi ama fungu la maneno kwenye sentensi kuonesha mshangao. Mfano, ***Ametoroka!***

***h) Parandesi au mabano ( ( ):*** Alama hizi hutumika kwenye maneno yanayofafanua kauli iliyotangulia, hasa katika sentensi. Kwa mfano;

Mkutano ule ulihudhuriwa na watu wote (wake kwa waume. (Wanjala na Kavoi, 2013:132).

***i) Kistari kirefu*** *(　):* Alama hii hutumika kuvunja muundo au mtiririko wa sentensi ndefu.

***j) Kistari kifupi (-):*** Alama hii hutumika kuunga maneno mawili au kukata neno hasa unapokuwa umefika mwishoni mwa mstari wakati wa kuandika. Katika lugha ya Kiswahili neno hukatwa kwa kuzingatia muundo wa silabi. Mfano,

**Neno lililoungwa:** *tiba-matamshi*

**Neno lililokatwa:** (Pi-cha) kama katika jedwali

| |
|---|
| ***Spektogramu*** *ni mchoro wa mashine unaaonesha pi-cha ya sauti katika vipengele vyake vya kasi mawimbi.* |
| ***Maana kutoka: Massamba (2016:118)*** |

***k) Alama ya ritifaa ( ' ):*** Alama ya uandishi iliyo kama alama ya mkato, lakini yenyewe huwekwa kwa juu pembeni kidogo ya neno lenye kuhitaji ritifaa. Ritifaa hutumika kwenye maneno ya ving'ong'o. Mfano, *ng'ombe*. Pia, ritifaa hutumika kufupisha maneno kwenye shairi ili liweze kuimbika.

**l) Herufi kubwa (A/B/E):** Hutumika mwanzoni mwa sentensi au baada ya alama za kuuliza, kushangaa na nukta. Herufi hizi pia hutumika tunapoandika nomino za pekee hata kama ziko katikati ya sentensi. Mfano,

> ***S**tadi za **L**ugha*
>
> ***H**aya ni maarifa au ujuzi unaotumiwa na watu katika kuwasiliana kwa kutumia lugha. **K**una stadi nne kuu za lugha ambazo ni kusikiliza, kuongea (kuzungumza), kusoma na kuandika. **K**ila stadi ina nafasi yake maalum katika mchakato wa mawasiliano lugha.*
>
> **Kutoka: Wanjala na Kavoi, (2013: 63)**

***m) Alama ya mdokezo (...):*** Alama hii hutumika kuonesha kukatizwa kwa kauli au kuachwa kwa neno au kirai fulani. Mfano,

**n) Kinyota (*):** Alama hii hutumiwa kwa lengo la kumtahadharisha msomaji kuwa maelezo ya ziada yametolewa kuhusu jambo lililoandikwa.

***o) Mstari wa mshazali au mkwaju (/):*** Chiraka (2017: 130) anasema, alama hii hutumika kutenga Orodha ya vitu, tarehe, namba ya kumbukumbu, na badala ya au. Mfano,

**Tarehe:** 30/08/2021

**Namba ya Kumb:** PF/ /2021

**Badala ya:** Ada/desturi

Mpendwa mwanafunzi, tumeona kwamba lugha iwe ya mazungumzo au kuandika ni nyenzo ya msingi katika mawasiliano. Kwani, bila lugha hatuwezi kufikisha ujumbe tunaoukusudia.

## Tafakuri ya Somo

Mpendwa mwanafunzi, Sasa tumemaliza kujifunza moduli ya ***Misingi ya Lugha na Isimu ya Lugha ya Kiswahili***. Moduli hii ilikuwa na masomo manane. Naamini masomo uliyojifunza katika moduli hii yatakuwa na faida kwako binafsi na kitaaluma, pamoja na kuisaidia jamii inayokuzunguka. Sasa basi, hebu chukua kalamu yako na daftari ufanye zoezi fupi ili kupima uelewa wako kuhusu mambo uliyojifunza katika moduli hii.

1. Unaweza kuchambua mada zipi za lugha ya mazungumzo na maandishi?

2. Unazitumiaje alama mbalimbali za uandishi?

## Zoezi la Somo

Jibu maswali yafuatayo; kisha weka kazi yako katika mkoba-kazi:

1. Wewe pamoja na wanafunzi wenzako mmemaliza mafunzo katika programu ya "Shahada ya Elimu ya Watu Wazima na Mafunzo Endelevu." Mnataka kumwalika Mkuu wa Mkoa chuo kilipo awe mgeni rasmi katika mahafali yenu.
    a) Andaa hotuba itakayotolewa na mgeni rasmi.
    b) Andaa risala itakayosomwa na mwanachuo mwenzenu katika mahafali hayo.
    c) Andaa barua za mwaliko pamoja na ratiba ya shughuli nzima.
2. Andika barua ya maombi ya kazi ya Mwezeshaji wa moduli ya Kiswahili katika Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima mahali ulipo. Pamoja na barua hiyo, andika na kuamtanisha tawasifu yako.

# Marejeleo

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. DUP: Dar es Salaam.

Habwe, J. na Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Phoenix Publisher

Khamis, A. M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam.

King'ei, K. (2010), *Misingi ya Isimujamii*, Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Lyons, J. (1968), Introduction to Theoretical Linguistics, Cambridge: Cambridge University Press.

Matei, K. A. (2008). *Darubini ya Sarufi Ufafanuzi Kamili wa Sarufi*. DUP: Dar es Salaam.

Matinde, R. S. (1991). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia*. DUP: Dar es Salaam.

Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam

________ (2002), *Historia ya Kiswahili 50 BK hadi 1500 BK*, The Jomo Kenyatta Foundation: Nairobi.

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA), Sekondari na Vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Dar es Salaam

Massamba, D. P. B., Kihore, Y. M. na Msanjila, Y. P. (2004). *Fonolojia ya Kiswahili Sanifu (FOKISA), Sekondari na Vyuo*. Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Dar es Salaam.

Mekacha, R. D. K. (2011), *Isimujamii: Nadharia na Muktadha wa Kiswahili*), Taasisi ya Taaluma za Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Mgullu, R. S. (1999). *Mtaala wa Isimu: Fonetiki na Fonolojia ya Kiswahili*, Nairobi Longhorn Publishers. Nairobi Longhorn Publishers: Nairobi.

Msanjila, Y. P., Kihore, Y. M., na Massamba, D. P. B. (2009), *Isimujamii Sekondari na Vyuo*, Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Educational Publishers and Distributors Ltd: Dar es Salaam.

Philipo, Z. T. T. (2013), *Sintaksia ya Kiswahili: Misingi na Nadharia za Uchanganuzi wa Kiswahili*, Chuo Kikuu cha Dodoma: Dodoma.

Rubanza, Y. I (1996), *Mofolojia ya Kiswahili*, Chuo Kikuu Huria cha Tanzania: Dar es Salaam

Wanjala, F. S. na Kavoi, J. M. (2013). *Stadi za Mawasiliano na Mbinu za Kufundishia Kiswahili Kwa Wanafunzi, Walifunzi, na Walimu*, Serengeti Educational Publishers (T) Ltd: Mwanza.

Weber, H. (1985), *A Dictionary of Phonetics and Linguistics,* Heinemann Educational Books: London.